

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Nne – Tarehe 11Aprili, 2011

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA UJENZI:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Fedha za Barabara kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 [*The Annual Report and Audited Accounts of The Roads Fund Board for the Financial year 2008/2009*].

MASWALI NA MAJIBU

Na. 46

Utaratibu wa Kuandikisha wapiga Kura

MHE. RIZIKI OMAR JUMA aliuliza:-

Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ambayo ni wakala wa Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) inatumia Sheria inayohitaji vitambulisho vya ukazi katika kuandikisha wapiga kura jambo ambalo ni tofauti na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Je, Serikali haioni kwamba kutumia sheria mbili tofauti kwa uchagua mmoja wa Jamhuri ya Muungano ni kuwanyima fursa wananchi wengine?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) imeanzishwa chini ya Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na majukumu ya *NEC* yameanishwa katika ibara hiyo kuwa pamoja na mambo mengine itakuwa na jukumu la kusimamia Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Tume ya Uchaguzi Zanzibar (*ZEC*) imeanzishwa chini ya Katiba ya Zanzibar na majukumu yake yameainishwa katika Katiba hiyo kuwa ni kusimamia uchaguzi wa upande wa Tanzania Zanzibar (Rais wa Zanzibar na Wawakilishi wa Baraza la Mapinduzi).

Kutokana na ukweli huu, siyo sahihi kusema kwamba *ZEC* ni wakala wa *NEC*. Hivi ni vyombo viwili tofauti vyenye majukumu tofauti na kila chombo kina mamlaka kamili juu ya majukumu yaliyoainishwa kwenye sheria husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 12(a) cha sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kama ilivyorekebishwa mwaka 2010 kinaipa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) mamlaka ya kutumia daftari la wapiga kura lililoandaliwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar lakini pia kifungu hicho hicho kinaipa *NEC* mamlaka kuandikisha wapiga kura watakaompigia kura Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao hawakuandikishwa na *ZEC*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kifungu cha 12(a) hakuna mwananchi anayenyimwa haki za kupiga kura kwa sababu kama mtu hakuandikishwa na *ZEC* atakuwa ameandikishwa na *NEC*.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ambayo mimi binafsi hayakuniridhisha. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, unapofika wakati wa uchaguzi wapiga kura wa Zanzibar wanatumia daftari la *ZEC* ambalo ni lazima uwe na kitambulisho cha ukazi ili uweze kuandikishwa kuwa mpiga kura. Lakini bahati mbaya sana watu wengi walinyimwa hiyo haki kutokana na kisingizio cha cheti cha kuzaliwa hata kama umri wa miaka 80. Wapiga kura hao ambao waliachwa na daftari la *NEC* walipokuja kuandikisha wapiga kura wa kumchagua Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wale walipewa nafasi ya kumchagua Rais tu wale ambao wameachwa kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano hawakupewa fursa ya kumchagua Mbunge, je, Mbunge wa Geita na Mbunge Kojani wanatofauti gani mpaka wachaguliwe na sheria mbili tofauti? (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inasemaje sasa kuhusu kurekebisha sheria hiyo ili wapiga kura wote au Watanzania wote wawe na haki ya kuchagua Wabunge wao kwa usawa?

SPIKA: Mtaona kwamba leo picha hazionekani huku kwa sababu kuna *technical faulty* fulani hivi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Katika zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la wapiga kura *NEC* Tume ilifanikiwa kuongeza idadi ya wapiga kura waliojandikisha kufikia milioni 20,137,303 kutoka idadi ya awali ya milioni 15,935,493 ikiwa ni ongezeko la wapiga kura milioni 4,201,801. Idadi ya wapiga kura katika uchaguzi huo kwa bara ilikuwa ni asilimia 42.8 kwa Zanzibar waliompigia Rais ni asilimia 84, nilitaka kuweka hizi takwimu tu. Lakini kwa ufupi sana ni kwamba sheria ya *NEC* na *ZEC* ni tofauti, *ZEC* kuna masharti kadhaa ambayo yanatakiwa ili watu wawe wapiga kura kwa uchaguzi wa viongozi wa Zanzibar lazima wawe na hivyo vitambulisho.

Lakini sisi kwa sheria ya Jamhuri ya Muungano hivyo havihusiki, kwa hiyo kilichofanyika kwa utaratibu ni kwamba wale waliosajiliwa kwa daftari la *ZEC* wote waliweze kumpigia kura Rais lakini wale waliokuwa na sifa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge hili amba waliachwa kwa sababu hawana sifa ya kumchagua Rais wa Zanzibar walisajiriwa kwenye daftari ya *NEC*, na hivyo wote wawili walikuwa na sifa ya kupiga kura za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hizi ni sheria mbili tofauti nataka hata bila daftari la *ZEC*, *NEC* ingeweza kuandikisha wapiga kura wakumpigia Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa sheria ya *NEC* iliyotungwa na Bunge hili kwa hiyo ndiyo tofauti. Lakini nakubali ushauri wako kwamba imefika wakati wa *ku-harmonize* sheria hizi.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuwa shauri hili tulilijulisha Serikali mapema, kabla ya uchaguzi tulimwandikia Mwanasheria Mkuu, Waziri Mkuu na hata Spika aliyeppita analifahamu vizuri, lakini Serikali imelipuuza kwa makusudi, hawaoni walivunja Katiba ya ile haki ya raia kuchagua na kuchaguliwa na kwamba uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unasimamiwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inasimamiwa na Sheria ya Uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni kwanini Serikali ilipuuza wakati wote na wakati wakijua kabisa kuna uvunjaji wa Katiba wa makusudi? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad, kama ifuatavyo:-

Mimi sioni kama kulikuwa na uvunjivu wa Katiba, uchaguzi umeendeshwa kwa mujibu wa sheria hizo mbili, Wabunge waliomo humu ndani waliochaguliwa katika uchaguzi huo ni Wabunge halali, na Wabunge waliochaguliwa na Baraza la wa Wakilishi ni wajumbe halali kwa mujibu wa sheria hizi mbili. Mimi nafikiri kama kuna hoja sheria

hii ya ZEC haibadilishwi humu ndani sheria ya ZEC inabadilishwa Zanzibar tunao wawakilishi wenzetu wa vyama vyetu kule tuwapelekee ili waweze kurekebisha hii sheria ifanane na ya kwetu huku, kwa sababu huku kwetu sasa kwenye Bunge na Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuna marekebishesha ya sheria mama ya Katiba ambayo ningewaomba sana Waheshimiwa Wabunge mtumie muda wenu vizuri katika marekebishesha yanayokuja ya Katiba, ili Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iondoshe hizo dosari ambazo mnaziona hivi sasa.

Na. 47

Wilaya ya Kasulu

MHE. AGRIPINA ZAITUNI BUYOGERA aliuliza:-

Kumekuwepo na mkanganyiko wa uelewa juu ya Wilaya ya Kasulu kuwa ni Halmashauri ya Mji au ni Mamlaka ya Mji mdogo; kiasi cha kuathiri utendaji:-

- (a) Je, Serikali inatoa tamko gani la ufanuzi juu ya jambo hili?
- (b) Je, ni hatua zipi zilizotumika kufikia kutoa taarifa juu ya wilaya ya Kasulu hatakusababisha mkanganyiko huo?

SPIKA: Hili ni kosa la Spika kukuandika wewe Viti Maalum unasi mama nikashangaa kabisa, kwa hiyo ninaomba ujibu swali huyu ni Mbunge wa Kasulu Mjini.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa sura Na. 288 kifungu cha 8(1) ilitoa Tangazo Na. 379 la kusudio la kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji mdogo Kasulu kuwa Halmashauri ya Mji wa Kasulu. Kwa kuzingatia sheria hiyo muda wa Tangazo uliotolewa na siku sitini (60) ili kuwapa fursa wananchi wanaohusika na maeneo hayo kutoa maoni yao endapo kuna pingamizi au ushauri wowote juu ya azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na uchambuzi wa pingamizi, maoni na ushauri uliopokelewa kutoka kwa wadau mbalimbali pamoja na kuandaa Hati ya kuanzisha Halmashauri za Miji mbalimbali nchini ikiwemo Kasulu. Kwa mujibu wa sheria ya Serikali za Mitaa Sura 288 kifungu cha 5(1) inafafanua kuwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa atatoa tangazo la kuanzisha Halmashauri za miji ikiwemo Kasulu.

(b)Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI tarehe 20 Januari, 2011 ilimuandikia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, ahakikishe wananchi wengi wanapata taarifa ya kusudio hilo na kutoa maoni yao kwa lengo la kuleta dhana ya ushirikishwaji.

Mheshimiwa Spika, mkanganyiko uliojitokeza ulisababishwa na tafsiri isiyokuwa sahihi ya tangazo la kusudio la kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Kasulu. Kwa maelezo hayo Halmashauri ya Mji wa Kasulu itaanza rasmi pale Tangazo la Serikali litakapotolewa rasmi. Mwongozo na maelekezo ya kuanzisha mamlaka hizo yatatolewa na OWM-TAMISEMI.

MHE. AGRIPINA ZAITUNI BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza, kutokana na majibu ya Naibu Waziri na ninajua kabisa tatizo na mgogoro wa Kasulu anauelewa vizuri kwa sababu mimi nilikuwa Diwani katika kipindi kilichopita na yeye amekuwa akifanya ziara kuja Kasulu anakutana na malalamiko haya.

Kwa kuwa nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na tulishiriki katika chaguzi za Serikali za Mitaa tukijua Kasulu Mjini tuna Mamlaka ya Mji Mdogo na tukachagua vitongoji hatimaye wenyeviti wa vitongoji hawakupewa fursa ya kutumikia wananchi wao waliowapigia kura na kuleta barua nyingi za kutulalamikia ofisini kwako bila majibu.

Je, leo unaelekeza nini katika Halmashauri za wilaya Kasulu ili kumaliza mgogoro huu?

Kwa kuwa umekiri kwamba Halmashauri ya Mji wa Kasulu bado haijatangazwa rasmi, lakini kuna maelekezo kwamba kuna uchaguzi kuna kata ambazo zimeongezwa katika Halmashauri za mji wa Kasulu, ninaomba uwaelekeze wananchi ni lini zoezi hili litakamilika ili kuwapa fursa ya kutumikia na kuleta maendeleo haraka ya wilaya ya Kasulu ahsante sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, na samahani sana kwa jinsi tulivyokuwa tumeweka pale tuliona kule ofisini kama ifuatavyo.

Kwanza niseme tu kwamba hili la mamlaka la mji mdogo tatizo ni hilo nililolieza hapa kwamba wenzetu tulipopeleka kusudio pale wao walichukulia kwamba ndipo sasa Halmashauri ya mji imeanzishwa.

Sasa Halmashauri ya mji ilikuwa haijaanzishwa kwa sababu tulitaka tupate mawazo yao, sasa tukirudi tena kwenye Halmashauri ya Mji mdogo tunarudi nyuma, Halmashauri ya Mji mdogo ni kipindi cha mpito kuelekea Halmashauri ya Mji na ndicho kinachotokea pale.

Anazungumzia Kata, Kata ambazo zitaingia katika Halmashauri ya mji huu zitakuwa ni Kata 14 sasa hivi tunapozungumza wanazo Kata nane, na jambo hili kama anavyolisema ni kweli kabisa hata Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe amekwenda mpaka Kasulu na ameeleza kuhusu kusudio la kuanzisha mamlaka ya mji wa Kasulu.

Kwa hiyo sasa hizo sita anazozizungumza wakati tutakopokuwa tumetamka rasmi kwamba sasa tunayo mamlaka ya Kasulu humo ndani zitakuwepo pia hizo Kata sita. Sasa ameuliza ni lini, zoezi hili halifanyiki kwa ajili ya Kasulu tu, linafanyika kwa ajili ya nchi nzima Tanzania kwa hiyo pale tutapokuwa tumemaliza mchakato huo *immediately* na hili jambo sasa hivi tunapozungumza linafanyiwa kazi tutakuwa tumekamilisha zoezo hilo.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa, baraza la mamlaka ya mji mdogo wa Kasulu halijawahi kufanya kazi hata siku moja tangu uchaguzi wa Serikali za Mitaa zilipomalizika mwaka 2009.

Je, Waziri anatamka nini kuhusiana na hali hiyo kwa sababu sio hali ya kawaida kuona kwamba baraza na wajumbe wake halali wapo lakini hawajaweza kufanya kazi na afisa wa mamlaka ya mji mdogo yupo anaendelea kufanya kazi ofisini bila kuwa na watu ambao wanaweza wakapanga na kueleza maslahi ya wananchi, Waziri anatamka nini juu ya hali hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moses Machali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda nieleze vizuri hapa tuelewane kwamba mamlaka ya mji mdogo ni sehemu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, ni *integral part* hata Bajeti yake inapotengenezwa inatengenezwa mle.

Najua kabisa Mheshimiwa Mbunge anachozungumza. Hapa anazungumza kwamba kulikuwa kuna afisa mtendaji na mle ndani wanaingia wenye viti wa vitongoji pamoja na madiwani wengine wawili ambao wanaazimwa kutoka kwenye Halmashauri wanaingia mle ndani. Na kwamba kwa kipindi chote hiki tunachozungumza hapa hakuna jambo ambalo limekuwa linafanyika kwa maana ya utendaji.

Sasa hayo yamepita sasa kwa maana hatuwezi kusema basi kaeni sasa kama Halmashauri ya mji mdogo ili tuanze ku-*function* hivyo sisi tunachojuwa ni kwamba sasa tunakwenda kwenye hatua kubwa zaidi kuliko hii inayozungumza hapa.

Ni mapungufu nakiri kwamba ni mapungufu lakini sasa twende kwenye hatua ya mbele zaidi, *otherwise* tutakachosema hapa ni kusema basi tukakae kama Halmashauri ya mji mdogo kitu ambacho kwa maoni yangu na maoni ya ofisi ya Waziri Mkuu kitakuwa tunakirudisha nyuma.

Kwa hiyo mimi naomba tusimame hapa kwa kusema kwamba tunataka kuunda sasa Halmashauri ya mji, Halmashauri ya mji itakuwa na bajeti yake yenyewe na itasimama yenyewe bila kuhitaji sasa kutegemea Halmashauri ya Kasulu.

Na. 48

Usindikaji na Ukusanyaji wa Maziwa – Arusha.

MHE. NAMELOCK E. M. SOKOINE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatafuta mwekezaji wa kujenga kiwanda cha kusindika maziwa na kuweka vituo vya kukusanya maziwa kwa wafugaji wa Arusha ili kuwapunguzia adha ya kutembea na maziwa umbali mrefu wakitafuta masoko?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalí la Mheshimiwa Namelock Edward Moringe Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo;

Mkoa wa Arusha una viwanda vya kusindika maziwa vya kati, viwanda ambavyo ni vya *Arusha Dairy* na *International DairyProducts* vyenye uwezo wa kusindika lita 5,000 za maziwa kila kimoja kwa siku na *New Nothern Creameries* chenye uwezo wa kusindika lita 45,000 kwa siku. Aidha, mkoa huo una viwanda vinne vdogo vya Orkonei Pastoralist Association (ILARAMATAK) vilivyopo Naberera (*Simanjiro*), *Terat* (*Simanjiro*), Orkesmet (*Simanjiro*) na Longido vyenye uwezo wa kusindika lita 500 kila kimoja kwa siku. Mkoa pia una vikundi takribani 15 vilivyopo Wilayani Arusha na Arumeru ambavyo vinakusanya na kusindika maziwa takribani lita 200 kwa siku kila kimoja.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kusindika maziwa vya Mkoa wa Arusha hupata maziwa kutoka kwenye vikundi vya wafugaji wa Ng'ombe wa kisasa wa Wilaya za Arusha, Arumeru na baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Kilimanjaro. Kwa upande mwengine viwanda vya Engiteng hutegemea maziwa kutoka kwenye kundi la Ng'ombe wa asili walioko kwenye maeneo karibu na viwanda hivyo. Hata hivyo, baadhi ya viwanda hivyo hufanya kazi chini ya uwezo wake kwa 30% hususani kutoptana na uchache wa maziwa hasa wakati wa kiangazi na umbali wake mkubwa ambao maziwa hupatikana. Hivyo, uwezo wa kusindika maziwa siyo tatizo bali ni ukusanyaji na usafirishaji wa maziwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kushawishi sekta binafsi hususani Mashirika na Taasisi binafsi zilizomo Mkoani Arusha zinazojishughulisha na uzalishaji na ukusanyaji wa maziwa. kwa mfano *Heifer Project Tanzania*, *Orkonei Pastoral Association* (ILARAMATAK) na *Land O'Lakes* kusogeza shughuli zao karibu zaidi na wafugaji ili waweze kuwasaidia kukusanya mazinwa kwa ukaribu zaidi kuliko ilivyo sasa. (*Makofî*)

MHE. NAMELOCK E. M. SOKOINE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini pamoja na hayo ni na swali moja dogo la nyongeza. Je, Wizara yako iko tayari kusaidia usafiri katika hayo maeneo ambayo maziwa yanakwenda kukusanya kwani maziwa siyo tatizo bali tatizo ni usafiri.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Namelock E. M. Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitatumia mfano mzuri wa *Tanga Fresh* ambao wana ushirika unaotwa *TDCU* ambapo wana vikundi takribani 12 katika mkoa wa Tanga na wanakusanya lita 30,000 za maziwa kila siku.

Kwa hiyo, ninapenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge awashawishi wafugaji waunde vikundi vidogovidogo ambavyo vitaweza kubuni mradi na kuomba fedha kutoka *DADPS* ili wapatiwe gari la kusambaza na kukusanya maziwa lakini pia kupata matanki makubwa yanayoitwa *cooling tanks* ambayo yanauzwa shilingi milioni 20.

Hii itawasaidia sana kwa sababu Serikali haisaidii moja kwa moja kwa maana ya kutoa fedha Serikalini bali inasaidia kupitia kwenye mipango ya maendeleo ya Wilaya.

Lakini pia ningeomba watu ambao wana viwanda waweze kuchakata maziwa yao kwa kutumia *Ultra heat treatment (UHT)* ambayo maziwa yanadumu kwa muda wa miezi sita badahala ya kugandisha maziwa ambayo yanadumu kwa siku tatu au nne yanaharibika. UHT ni *technology* ambayo inasaidia maziwa yadumu kwa muda mrefu na hivyo kusaidia maziwa yaweze kupelekwa maeneo ya mbali kuuzwa na watumiaji wengi wanaiamini zaidi.

Kwa hiyo, ningeomba mashirika kama *Land Lakes* pamoja na *Heifer Project International* waweze kusaidia katika ukusanyaji wa maziwa wakati wanavikundi wanajiandaa kuomba fedha kutoka *DADPS*.

MHE. JITU VLAJLAR SONI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza kwamba je, Serikali ina mpango gani kuwawezesha wafugaji wapate mikopo kwa riba nafuu ili waweze kuijendezeza kwa kupitia dhamana yaani mifugo yao ndiyo iwe dhamana ili waweze kuijendezeza kwa ufugaji bora na waweze kupata manufaa wao pamoja na Taifa letu. Kwa hiyo, kwa sasa hivi wafugaji hawapati mikopo ya aina yoyote.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jitu Soni kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, njia ya kwanza ni wananchi hawa kuijunga kwenye *SACCOS*, *SACCOS* zinaaminika zaidi kuliko mtu mmojammoja na kuomba mikopo kutoka kwenye Benki za Biashara.

Lakini njia ya pili kuna Benki ya Raslimali ambayo sasa hivi ina dirisha la kutoa fedha kwa ajili ya kilimo na ufugaji. Nawashauri wakulima hao waweze kupata access na Benki ya Raslimali yaani TID ili waweze kupata mikopo.

Lakini sasa hivi Serikali iko katika mchakato wa kuandaa Benki ya Kilimo kwa hiyo wakulima ambao wangependa mikopo mikubwa zaidi na ya muda mrefu kusema kweli mchakato huu ukikamilika Benki ya Kilimo Tanzania ndiyo itakuwa mfumbuzi wa mkulima na mfugaji.

Na. 49

Tamko la Kuwahamisha Wananchi Karibu na WMA ya Makao Wilayani Meatu

MHE. JEREMIAH M. OPULUKWA aliuliza:-

Hivi karibuni Serikali ilitoa tamko kuitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga kwamba wananchi wa maeneo yanayozunguka *Wildlife Management Area (WMA)* ya Makao Wilaya ya Meatu wahame ifikapo tarehe 30/6/2011 baada ya tarehe hiyo nguvu itatumika.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kusitisha zoezo hilo hadi hapo itakapofanya utafiti wa kina kuhusu suala hilo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jeremiah Meshack Opulukwa, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo.

Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamaporini yaani *Wildlife Management Areas (WMAs)* nchini huanzishwa na wananchi wenyewe katika Ardhi ya vijiji vyao baada ya kutenga eneo husika kulingana na Mpango wa Matumizi Bora ya ardhi ulioandalishiwa na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa kijiji husika.

WMA ya makao ambayo ilianzishwa mwaka 2007 kwa mujibu wa Kanuni za WMAs za mwaka 2005 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Namba 369 la tarehe 20/11/2009, ni kati ya vijiji saba vya wananchi vilivyoungana na kuunda Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamaporini yaani (*JUHIWAPOMA*) iliyoko Wilayani Meatu na imepewa haki ya Matumizi ya Raslimali ya Wanyaporini (*Wildlife Resources User Right*) tarehe 29/03/2010 kwa mujibu wa Sheria ya Kuhifadhi Wanyamaporini Na. 5 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa kuunda Jumuiya hiyo ya Hifadhi, wananchi wa eneo la Makao, kwa ridhaa yao wenyewe waliamua kutenga eneo hilo, hivyo, wananchi hao hawawezi kuondoka katika eneo husika linalozunguka WMA kwa vile ndiyo wahuksika katika ulinzi na manufaa yanayotokana na matumizi ya raslimali za eneo hilo watafaidika. Wananchi wanaotakiwa kuhamishwa kwa Serikali ni wale

waliovamia eneo lililotengwa kwa ajili ya WMA kulingana na Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Vijiji Wanachama. Hivyo, si kweli kuwa wananchi walioko ndani ya WMA ambao wataondolewa bali ni wale tu waliovamia kutoka kwenye maeneo mengine na kuweka makazi na kilimo kwenye maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya WMA.

MHE. JEREMIAH M. OPULKWA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo kwa kiwango kikubwa hayakuweza kujibu swali langu, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, nitapenda kumpa utangulizi kidogo Mheshimiwa Waziri.....

SPIKA: Isiwe hotuba sana.

MHE. JEREMIAH M. OPULKWA: Mheshimiwa Spika, Waziri anasema kwamba hawa watu ni wavamizi, wamevamia maeneo yanayozunguka au kandokando ya WMA ya Makao, lakini ukiangalia WMA ya Makao ilianzishwa mwaka 2007 na hawa watu wamekaa tangu mwaka 1999 wako pale. Kwa hiyo, WMA imeewakuta wanakijiji wakiwa pale. Lakini kwa sababu Serikali haitaki kuwasikiliza hawa watu na kwa sababu Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga baada ya uchaguzi wa mwaka 2005 alikwenda kule na kuwashamisha watu kwa nguvu na baadaye yeye mwenyewe akaenda kuchukua baadhi ya maeneo yale kwa ajili ya uwekezaji kwa faida yake binafsi.

Je, sasa Waziri haoni kwamba kuna umuhimu sasa wa kusitisha zoezi la kuwashamisha watu hawa kwa sababu kulikuwa na ubabaishaji wa kuanzishwa WMA ya Makao na ndiyo maana vijiji vyote kasoro kimoja tu cha Mwangudo, Sapa, Iramba Ndogo, Mbushi, Mwanjoro na Wamagimu wamesema hawataki WMA ni mpaka hapo Wizara itakapokubaliana nao jinsi ya kuweza kutatua tatizo hilo.

Swali la pili, kama Mheshimiwa Waziri Mkuu baada ya kuona bomoa bomoa ya Magufuli imezidi na akaamua kusitisha zoezi la bomoa bomoa kandokando ya hifadhi ya barabara za Taifa.

Je, Serikali au Waziri haoni umuhimu sasa ili kuondoa tatizo na kero itakayowapata wananchi hao kusitisha bomoabomoa au uhamishaji wa hawa watu ambao wako katika maeneo yanayozunguka WMA ya makao kwa sababu wamesema hawako tayari kuhama na hawako tayari kufanya lolote ni mpaka hapo tutakapoweza kuwasaidia kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SPIKA: Ahsante, lakini swalii lako ni refu mno, Mheshimiwa Waziri jibu kwa kifupi sana, ujifanye Magufuli hapo katikati haya! (*Kicheko*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya rafiki yangu sana Mheshimiwa Opulkwa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ningetamani sana Mheshimiwa kungekuwa na muda wa kutosha, lakini kwa kuzingatia angalizo lako. nitajitahidi kufanya hivyo.

Kwanza, mchakato huu kama nilivyosema ulianzishwa kwa ridhaa ya wanavijiji wenyewe. Niseme kwamba Mheshimiwa Mbunge amesema ni vijiji sita katika vijiji saba, tuseme kwamba sisi katika Wizara hatuwezi tukatoa *User Right* au kukubali kusajiri *WMA* kama hatuna *minutes* za vijiji waliokaa wakakubaliana.

Kwa hiyo, naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba vijiji vyote saba walikubaliana hivyo. (*Makofi*)

La pili ni kwamba hatutoi vijiji vizima, wanapokubaliana kuanzisha *WMA* wanatenga ardhi tunazungumzia suala la *land use plan*, linakuwepo eneo ambalo wamelitenga kwa ajili ya makazi na kwa ajili ya shughuli hiyo.

Kwa hiyo, si kweli kwamba wananchi wanaondolewa isipokuwa kwenye lile eneo tu ambalo wao wenyewe walikubaliana lifanyike kwa ajili ya uhifadhi na ni kwa manufaa ya vijiji vyenyewe. Kwa hiyo, hakuna kijiji kinachoondolewa isipokuwa kutekeleza makubaliano ambayo vijiji vyenyewe vimekubaliana.

Tatu niseme kwamba Mheshimiwa Opulukwa ameomba kwamba zoezi hili lisitishwe, lakini naona kama kuna *contradiction* kwa sababu tarehe 29 Desemba, 2010 Mheshimiwa Opulukwa pamoja na Wabunge wengine walifanya kikao kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, walikubaliana mambo nane mojawapo, nitalinukuu kwamba “waliolima katika maeneo tengefu wapewe muda wa miezi sita tu kutoka Desemba, waorodheshwe kijiji kwa kijiji na waeleze wana mifugo kiasi gani, tusiruhusu wapya kuhamia. Kamati maalum za Wilaya, Kata na vijiji zisimamie zoezi hili na baada ya hapo waondolewe.”

Hizi ni *minutes* ambazo Mheshimiwa Opulukwa alishiriki. Kwa hiyo, ninaomba tu kwamba kwa ajili ya kulinda maslahi ya wanavijiji wenyewe kwa mujibu wa Katiba yao ya kuanzisha *WMA* ninaomba tu Mheshimiwa Opulukwa arejee kwenye haya makubaliano na tusaidiane kuwasaidia wananchi wa Meatu. (*Makofi*)

Na. 50

Kivuko cha MV. Geita

MHE. DKT. CHARLES JOHN TIZEBA aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wakati wa kuzindua Kivuko cha MV. Misungwi alieleza kuwa Kivuko cha *MV. Geita* kifanyiwe ukarabati ili kiweze kuhudumia wananchi wa Kisawa cha Maisome na aliporudi tena Sengerema wakati wa kampeni za Uchaguzi aliahidi kuwa

kivuko hicho kitafanyiwa ukarabati wa dharura ili kianze kutumika mara moja na kwamba Serikali itanunua kivuko kipyga ndani ya miaka hii mitano.

Je, ni lini ahadi zote hizi zitatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Eng. Charles Tizeba, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya ukarabati wa kivuko cha *MV. Geita* pamoja na kununua Kivuko kipyga cha Maisome wakati wa kampeni za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ahadi hiyo ya ukarabati wa Kivuko cha *MV. Geita* na ununuzi wa Kivuko kipyga cha Maisome itaanza kutekelezwa kwa kutenga fedha katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 na 2012/2013 kwa ajili ya ukarabati wa kivuko cha *MV. Geita* na ununuzi wa Kivuko kipyga cha Maisome. Hata hivyo, utekelezaji halisi utategemea kiasi cha fedha kitakachoidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na 2012/2013.

MHE. DKT. CHARLES JOHN TIZEBA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, ikumbukwe kwamba Naibu Waziri nilikwishawasiliana naye kuhusu hili jambo na kumwonyesha ugumu uliosababishwa na makadirio ya juu sana ya ukarabati wa kivuko cha *MV. Geita* jambo ambalo linasababisha usitekelezwe kama Rais alivyowaahidi wananchi kwa maana ya dharura. Hivi leo wananchi wanaendelea kuteseka na Makadirio yaliyotolewa kwanza katika bodi ya barabara ya Mkaoa yalikuwa karibia takribani bilioni moja jambo ambalo linasababisha sasa Wizara izungumzie kusubiri Bajeti.

Mheshimiwa Spika, utafiti wangu unaonyesha kwamba Makadirio ya halisi ni ukarabati huo si zaidi ya shilingi milioni 200.

Je, Wizara sasa iko tayari kwamba tuunde katume ka kuthibitisha Makadirio yale yaliyotengenezwa na Wizara na yale ambayo wauzaji wa hiyo mitambo wanaitoa kwa wanunuzi wengine?

SPIKA: Wakiunda Tume watatumia fedha zaidi! Afadhali uende mwenyewe tu ukathibitishe inaonekana mnataka kutumia hela nyingi kuliko inavyohitajika.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ni kweli kabisa tulishawasilisha na Mheshimiwa Mbunge na taarifa alizotupa tunazifanya kazi kama Serikali. Sasa tusingependa mchakato wa kiutendaji wa kufanya kazi hayo aliyotupa tuenze sasa kuyajadili hapa.

Ninapenda tu kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba utekelezaji wa ahadi ya Rais kama vile ambavyo tunatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ni kwa muda wa miaka mitano, awe na subira tutatekeleza.

Na. 51

Meli ya MV. Clarias

MHE. SALVADOR M. NALUYAGA aliuliza:-

Wakati wa Ukerewe wanategemea sana usafiri wa meli kwenda na kutoka nje ya Wilaya yao, na kwamba meli inayotumika sasa ni MV. Clarias ambayo imechoka sana na inaweza kuhatarisha maisha ya wasafiri kama hatua zipasazo hazitachukuliwa mapema.

Je, ni lini Serikali itapeleka meli mpya kunusuru maisha ya wakazi wa Ukerewe?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu sasa swali namba 51 la Mheshimiwa Salvatory Naluyaga, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Meli ya MV. Clarias ilijengwa mwaka 1961, hadi sasa ina umri wa miaka 50. Hata hivyo, meli hiyo imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya mara kwa mara (*Routine Maintenance*) na pale inapoharibika hufanyiwa ukaguzi na SUMATRA ili kupewa Hati ya Ubora wa Meli (*Seaworthiness Certificate*) kabla haijaruhusiwa kutoa huduma za uchukuzi ziwani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi hizo Serikali ina mkakati wa kuzifanyia ukarabati mkubwa meli za Kampuni ya Huduma za Meli ili kupunguza matatizo yaliyopo ya uchakavu wa meli. Aidha, Serikali ina mpango wa kununua meli mpya katika ziwa Victoria.

Ili kutekeleza mpango huo, Serikali imeomba ufadhlili wa Serikali ya Denmark, kufanya upembuzi yakinifu kuhusu matengenezo hayo na aina ya meli zinazofaa kununuliwa.

Kwa kuanzia, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012, Wizara yangu itatenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa meli moja. Aidha, pamoja na juhudhi hizo za Serikali, bado tunaendelea kushirikisha sekta binafsi kutoa huduma za uchukuzi katika Ziwa Victoria. Hivi sasa kuna meli ya MV. Nyehunge inayofanya safari kati ya Mwanza na Ukerewe.

MHE. SALVADOR M. NALUYAGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kwa niaba ya wananchi wa Ukerewe kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara inasema kwamba ina mpango mkakati wa kununua meli mpya katika Ziwa Victoria itakayoelekea Ukerewe; namwomba Mheshimiwa Waziri atwambie hiyo meli ina ukubwa kiasia gani, itabeba abiria wangapi na magari mangapi na lini itakuja Ukerewe?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu anapoongea hii leo meli za *Marine* hazipo Ukerewe, hazipo zimekufa zote; MV. Clarias imesimama haipo imekufa, MV Butiama haipo imekufa kwa mantiki hiyo wameitekeleza Ukerewe. Wizara naomba itwambie ni lini Meli itakuja Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika nashukuru. Ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salvador M. Naluyaga, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kama nilivyooleza kwenye jibu langu la msingi Serikali ya Denmark inatusaidia kufanya upembuzi yakinifu, tutajua hiyo meli itakuwa na ukubwa gani na uwezo wake wa kubeba abiria na magari mangapi.

Lakini pia nimetamka kwamba MV. Nyahunge bado inatoa huduma na mimi nilikuwa Mwanza niliikaguwa ile meli mpaka kwenye *engine room*. Hii meli ya MV. Clarias bado inafanyakazi ila tu baadhi ya wananchi wanaotumia meli ile wanachukua yale maboya wanapotoka wanaweka kwenye mabegi wanatoka nayo. Ningeshauri Mheshimiwa Mbunge tushirikiane kwa sababu ya usalama wa chombo kile, yale maboya yabaki kwenye meli wananchi wanapotoka. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Synthia Ngoye swali lingine la nyongeza, sijui hilo la Ukerewe litakuwaje.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa matatizo ya usafiri wa meli kwa wananchi wa Ukerewe yanafanana sana na matatizo ya wananchi waishio mwambao wa Ziwa Nyasa katika Wilaya za Kyera, Ludewa na Mbinga kiasi hata Mheshimiwa Rais aliahidi kununua meli mpya.

Je, katika mpango mkakati wa Wizara hii meli hiyo mpya itanunuliwa lini?

SPIKA: Jamani mmetutoa Mwanza mpaka huko kwingine, Naibu Waziri majibu kama yapo.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais aliahidi na iko kwenye Ilani ya Uchaguzi kwamba Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika kila moja litapata meli mpya. Lakini utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ni miaka mitano, namwomba Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, avute subira tu, tutahakikisha pia meli mpya inapatikana katika Ziwa Nyasa katika kipindi hiki cha miaka mitano kama Bajeti itakavyoendelea kuturuhusu na Bunge lako Tukufu likathibitisha.

SPIKA: Naona wakiati wa kuvuta subira hapo ni wananchi, si Mheshimiwa Ngoye peke yake. Haya tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Na. 52

Mawasiliano ya Simu – Busega

MHE. DKT. TITUS KAMANI aliuliza:-

Mawasiliano ya Simu katika ulimwengu wa sasa ni muhimu sana kwani ndio kichocheo cha maendeleo kwa wananchi.

Je, ni lini mawasiliano ya simu yatafikishwa Kata za Shigala, Kiloleli, Badugu, Nyaluhande na Mkula katika Jimbo la Busega?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
aijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mbunge wa Jimbo la Busega, napenda kutoa maelezo ya ufanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu katika maeneo yote nchini. Hata hivyo, asili ya kijiografia ya maeneo mbalimbali, idadi ya wananchi katika maeneo husika kutowiana na gharama za kuwekeza mitambo ya mawasiliano, uhaba wa miundombinu ya barabara na nishati ya kutosha yenye gharama nafuu kwa ajili ya kuendesha mitambo ya mawasiliano imekuwa ni kikwazo kikubwa kwa makampuni ya simu kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufanuzi huo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizoko ambazo nimezieleza hapa awali, hivi sasa Serikali inayashawishi makampuni ya simu nchini kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*Universal Communication Access Fund (UCAF)*) ili kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2012 zaidi ya 90% ya Watanzania wawe wamefikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu.

Aidha, Kampuni ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi ya *Airtel* ina mpango unaoanza Machi, 2011 hadi Machi, 2012 kufikisha huduma ya mtandao wa mawasiliano ya simu za mkononi katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliomba.

MHE. DKT. TITUS KAMANI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri yanayotia moyo ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa hivi kuna Mkongo wa Taifa ambao umepitishwa ndani kabisa ya Jimbo la Busega ukipitia vijiji vya Kiloleni, Nasa, Kalemela na Lamadi na kuna kituo kimejengwa pale Nasa kwa ajili ya kutoa huduma .

Je, ni lini wananchi wa jimbo la Busega wataanza kunufaika na Mkongo huu wa Taifa? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kabisa Mheshimiwa Dkt. Kamani kwa kutambua kwamba Mkongo wa Taifa umefika na umepita katika Jimbo lake kwa sababu pale Nasa lile jengo ni la zamani lakini kituo cha mawasiliano ya Mkongo wa Taifa kimewekwa kule ndani lakini ameweza kuitambua, kwa hivyo ni suala ambalo ningependa nimpongeze sana.

Mheshimiwa Spika, nimfahamishe tu Mheshimiwa Dkt. Kamani kwamba kituo kile kwa sasa kinatumika kama kituo cha kuwezesha mawasiliano au huduma ya Mkongo kuongeza yale mawimbi ya mawasiliano kupata nguvu zaidi.

Lakini katika awamu yetu ya tatu sehemu hiyo ya Nasa kituo hicho kitaweza kuwa na vitambuzi (*intelligent gargets*) ambavyo vitaweza kufikisha mawasiliano katika sehemu zingine kama pale Magu na Bunda.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nipende tu kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika hali ya sasa hivi wananchi wa Busega wanazidi kupata nafuu ya mawasiliano kupitia makampuni mbalimbali ya simu kwa mfano Kampuni ya *Airtel* sasa hivi katika kutambua na kutumia Mkongo wa Taifa imeweza kushusha gharama za mawasiliano katika *internet* kutoka ilivyokuwa kwa 50% kwa hiyo sasa hivi wananchi wa Busega wanapata *internet* kwa punguzo la 50% na katika awamu ya tatu itafikisha huduma hizo katika wilaya na wananchi wengi wataweza kupata faida zaidi.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa matatizo ya Busega yanafanana sana na matatizo ya Kibakwe ambako kata za

Ipela, Wota, Mbuga na Malolo hazina kabisa mawasiliano ya simu za mkononi. Mheshimiwa Naibu Waziri tuliongea nae na tuna mipango ya kwenda huko.

Je, mpango ule bado uko palepale ili tukaone hali ilivyo mbaya na kwamba mawasiliano hakuna?

SPIKA: Itabidi siku hiyo abebe simu. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi kwamba utakwenda tu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na yeze kwamba kweli mawasiliano katika vijiji alivyovitaja yana matatizo. Lakini kama nilivyosema katika jibu la swali la kwanza kabisa ni kwamba *UCAF* mfuko ambao utasaidia wananchi wote waweze kupata mawasiliano unajipanga vizuri ni kati ya vijiji 230 nchini ambao utahakikisha kwamba katika Tanzania kwa 90% wananchi wanafikiwa na mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, mazungumzo yetu yako palepale na akipenda anialike nitamtembelea kule jimboni kwake ili tuweze kuangalia hali anayoisema.

SPIKA: Si umesikia amekualika!

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ni kweli kwamba mawasiliano ya simu ni muhimu sana katika ulimwengu wa leo, na kwa kuwa hivi karibuni tulipitisha Sheria ya Usajili wa mambo ya Simu, lakini kwa kuwa Sheria ile haikuzingatia baadhi ya mambo ambayo leo athari tunaiona pamoja na kwamba Wabunge tuliichangia kuhusu mambo hayo yaingizwe hasa kwa mfano; kama lile tangazo linalooneshwa katika runinga na HakiElimu.

Je, Wizara yako sasa itakuwa na mpango gani wa kuiboresha Sheria ili baadhi ya makundi kama wanafunzi wanaotumia simu ambazo zinasababisha hata usikivu wao katika masomo kupotea na kusababisha majanga mengine makubwa kwa nchi hii. Je, Wizara yako sasa iko tayari kuiboresha Sheria ile ili kukidhi haja ya kundi lile ili Walimu wasipate tabu?

SPIKA: Kuiboresha ni wajibu wetu ila yeze anatakiwa kuleta mabadiliko sasa.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ye ye kwamba mabadiliko siku zote lazima yatokee, na yakinoteka kwa sababu ya muda ni vyema na Serikali yetu ni sikivu siku zote itazingatia na kuona kwamba sasa hivi muda umebadilika na kwa hali hiyo Sheria iliyopo haiendani na wakati huu, hivyo itabdalishwa. Kwa hiyo, tuko tayari wakati wowote tutakapoona kwamba Sheria imepitwa na wakati tutaitela hapa Bungeni ili tuweze kuibadilisha.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 53

Hitaji la Mawasiliano ya Simu - Mlalo

MHE. BRIG. JEN. HASSAN NGWILIZI aliuliza:-

Je, ni lini Kata za Shume, Manola, Rangwi na Mbaramo katika Jimbo la Mlalo zitapatiwa mawasiliano ya simu za mkononi, hasa ikitiliwa maanani kuwa eneo hilo lina wakazi wengi na shughuli nyingi za kibiashara na uchumi.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwapo kwa uhaba wa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi katika maeneo mengi nchini yenye shughuli za kibiashara na uchumi kama ilivyo katika Kata ya Shume, Manola, Rangwi na Mbaramo katika jimbo la Mlalo.

Jitihada zinaendelea za kisera ambazo lengo ni kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanafikiwa na huduma za mawasiliano. Serikali kwa kushirikiana na makampuni ya simu ipo katika hatua za mwisho za kuanza kutekeleza miradi ya majaribio ya huduma za mawasiliano itakayoshirikisha makampuni ya simu na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*).

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa yapo maeneo yanayokosa huduma za mawasiliano kutokana na kukosa mvuto kwa wawekezaji, kuititia mfuko huu, Serikali inatoa ruzuku kwa makampuni yatakayokuwa tayari kwenda kuwekeza katika maeneo kama hayo.

Vile vile mfuko huu utatumika kama chombo cha kuongeza chachu ya uwekezaji katika huduma za mawasiliano nchini, yakiwemo maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Brig, Jen. Hassan Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo. Aidha, Kampuni ya Mawasiliano ya Simu

za Mkononi ya Airtel ina mpango unaoanzia Machi, 2011 hadi Machi, 2012 kufikisha huduma ya mtandao wa Mawasiliano ya simu za mkononi katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

MHE. BRIG. JEN. HASSAN NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, nina swali moja dogo tu la kumwuliza Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na vilevile niimpongeze Kampuni ya *Airtel*. Lakini kwa vile kule Mlalo na Wilaya nzima ya Lushoto ni maeneo ya milimani na kampuni za *Voda*, *Tigo* na *Zantel* vilevile zina minara kule.

Je, Serikali itakubali kuwahimiza wawekezaji wengine ili waweze kusambaza huduma katika maeneo hayo ya Shume, Rangwi, Manola na Mbaramo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kama nilivyojibu katika swali la awali, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema na akiangalia mnara wowote kwa mara nyingi unakuwa na antena kule juu, lakini kwa hali ya kijiografia ilivyo katika eneo la Lushoto ni la mabonde na milima. Lakini wanateknolojia wanasema kwamba kuna njia watakayoifanya ambayo wanasema kufanya *optimazation*. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mawasiliano kama nilivyoeleza katika jibu langu la awali yatafikia maeneo yote ifikapo mwaka 2012.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matatizo ya mawasiliano katika jimbo la Mlalo yanafanana sana na matatizo ya mawasiliano katika jimbo la Lupa, hasa katika Kata za Kambi Katoto, Mafyeko, Matwiga, Mtanila, Mamba na Ifumbo na hapa Mheshimiwa Naibu Waziri anasema Kampuni ya *Airtel* ina mpango wa kurekebisha mawasiliano katika sehemu nyingi Tanzania ifikapo mwaka 2012.

Je, atawaambiaje wananchi wa jimbo la Lupa kuhusu mpango huo wa *Airtel*?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi ila vijiji hivyo sina hakika kama unavijua.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jimbo la Lupa pamoja na vijiji alivyovitaja vina matatizo yanayofanana na vijiji vyote katika nchi yetu. Tumefanya uhakiki kwa kutumia teknolojia ili kuona maeneo yote nchini ni yapi ambayo hayafikiwi na mawasiliano kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mwambalaswa kwamba katika huu mpango wa *Airtel* maeneo hayo aliyoyataja yamo katika vile vijiji ambavyo vitashughulikiwa na makampuni hayo ya simu wakishirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Watanzania Wote.

Na. 54

Athari za Mgao wa Umeme Nchini

MHE. GRACE S. KIWELU aliuliza:-

Matatizo ya uhaba wa umeme uliosababisha mgao kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yameathiri Pato la Taifa na Pato la Wananchi kwa ujumla:-

Je, hadi sasa Serikali inaweza kulieleza Bunge imepoteza mapato yake stahiki kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Grace Sindato Kiwel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, matatizo ya uhaba wa umeme, yamesababisha kuwepo kwa mgao wa umeme, ambapo unaweza kuleta athari katika Pato la Taifa na Pato la Mwananchi mmoja mmoja kwa ujumla. Aidha, ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Kodi za Ndani na Ushuru wa Forodha ambao hutegemea sana uzalishaji na kuwepo kwa umeme kwa ajili ya matumizi ya teknolojia ya kompyuta ili kuboresha ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli huo, mwenendo wa makusanyo ya mapato katika kipindi cha mgao wa umeme kuanzia mwezi Desemba, 2010 hadi Februari, 2011, umekuwa wa kuridhisha bila ya kuonesha athari za wazi kulingana na makisio ya mapato yaliyokuwa yamekusudiwa kukusanywa katika kipindi hiki. Makisio ya makusanyo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), Ushuru wa Bidhaa, Kodi za Makampuni, Kodi za Watu Binafsi (*PAYE*) na Ushuru wa Forodha kwa kipindi cha mwezi wa Desemba, 2010 hadi Februari, 2011 yalikuwa ni shilingi trilioni 1.24, ambapo makusanyo halisi yalifkia kiasi cha shilingi trilioni 1.22, sawa na asillimia 98 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado ni vigumu kuhusisha kushuka kwa makusanyo ya mapato kwa asilimia mbili katika kipindi cha Desemba, 2010 hadi Februari, 2011 na mgawo wa umeme, kwani ukusanyaji wa mapato huathiriwa na mambo

mengine zaidi ya umeme ikiwa ni pamoja na ukuaji wa uchumi, Biashara za Kimataifa na uhiari wa kulipa kodi yenyewe.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri, lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Kamishna wa Kodi ya Mapato TRA aliiambia Kamati ya Fedha kwamba ifikapo Aprili kama mgao wa umeme utaendelea watashindwa kukusanya shilingi bilioni 810 na mgao bado unaendelea. Je, kauli ipi ni ya kweli; ya Kamishna wa TRA ambaye ndiyo anakusanya kodi au ya Waziri? (*Makofit*)

(ii) Kwa kuwa nchi yetu ilikuwa ikikodisha mitambo kwa gharama kubwa mfano IPTL; je, Serikali ya Chama cha Mapinduzi haionti sasa umefika wakati wa kununua mtambo wenyewe na kupunguza tatizo la mgao wa umeme? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, ni kweli Kamishna Mkuu wa TRA aliahidi kwamba, mapato yataweza kukusanya kwa asilimia kubwa zaidi kama umeme ungekuwa ni wa kutosha; lakini kwa sababu umeme hautoshi na niliposema kwamba sehemu kubwa ya umeme haiwezi kuathiri pekee makusanyo ya umeme; kwenye jibu langu la msingi nimesema kwamba, kuna mambo mengi ambayo yanaathiri ukusanyaji wa umeme yakiwemo kukuza uchumi wa Taifa, Biashara ya Kimataifa na watu kulipa kodi kwa hiari yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wa TRA alipotamka hivyo, haina maana kwamba, juhudzi za kukusanya mapato zimekufa kabisa. Juhudi ziko pale pale na kama nilivyosema kwamba, bila kujali mgao wa umeme, kwa mwezi wa Desemba makusanyo yalikuwa ni makubwa sana. Hii ina maana kwamba, wale amba wanakusanya kodi na wale walipa kodi wenyewe hasa wale wakubwa, umeme kwa kiasi fulani hauwezi kuathiri kwa sababu wao wanatumia kununua jenereta na kuweza kuzalisha na hatimaye wanalipa kodi.

Kwa hali hiyo wasiwasi wa Mheshimiwa Mbunge kwamba, mapato yanaweza yakapungua na jibu langu la msingi kama nilivyosema si umeme tu bali kuna mambo mengine ambayo yanaweza yakaathiri kama vile ukuzaji wa uchumi, biashara za Kimataifa na hiari yenyewe ya kulipa kodi.

SPIKA: Samahani, Mheshimiwa Zitto kuna swali la pili; kwa nini Serikali isinunue mitambo yake badala ya kukodisha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la mitambo nafikiri ...

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahaaa sijakwita wewe; Waziri anaendelea kujibu, kwa hiyo unatakiwa ukae.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilikuwa ninapenda kuongezea majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Fedha, kwa maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Grace Kiwel.

Kwenye upande wa sehemu ya pili ya swali la nyongeza kwamba Serikali haioni umuhimu wa kununua mitambo yake; ninaomba kutumia nafasi hii kuwakumbusha Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, muda wote Serikali imekuwa ni ya dhati, kwa kipindi kati ya mwaka 2005 mpaka mwaka jana, tumefanikiwa kununua mitambo ya megawati 145. Dar es Salaam tulizindua mtambo wa megawati 100 mwaka 2008, lakini mwaka 2009 tukazindua mtambo unaojulikana kama WATSILA pale Tegeta wa megawati 45. Kwa kipindi hicho mpaka sasa, kama tusingepata matatizo ya uchumi kama tulivyosema, tulikusudia eneo la Kampuni ya ARTUMAS kule Mtwara, tuzalishé megawati 300, lakini muda huo uchumi utatuathiri.

Tusingepata matatizo ya ubinafsishwaji Mradi wa Kiwira, tungezalisha megawati 200, jumla tungkuwa na megawati 500, ukiongeza na megawati 145. Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, tungkuwa na megawati 645 ambazo zinamilikiwa na Serikali; lakini kwa sasa kipi kinaendelea?

Mwezi wa Desemba, mwaka huu, tunatarajia kuzindua mradi wa megawati 160; Dar es Saalam megawati 100, Mwanza megawati 60, lakini pia tunaendelea na Mradi wa Somangafungu megawati 230, eneo la kiwanja limeshapatikana ARTUMAS iliyokwama mwaka 2008 megawati 300 mwendelezaji ameshapatikana tuko kwenye hatua ya uendelezaji, inatarajiwa mwaka 2013 megawati 300.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, tuna Miradi ya Upepo lakini pia Kiwira tunaendelea na taratibu za kuhakikisha kuwa megawati 200 zinapatikana ndani ya gridi hii. Ahsante sana. (*Makofit*)

SPIKA: Nilimwita Mheshimiwa Zitto Kabwe, naomba uwe *very brief*.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, habari za Miradi tunazisikia kila siku na hazitekelezwi ...

SPIKA: Mheshimiwa Zitto, hili siyo swali la umeme ni la kodi.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Namwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kwamba; moja ya sababu inayosababisha mapato ya *TRA* kutokusanywa vya kutosha ni kutokukua kwa uchumi. Nishati ya umeme ni *ingredient* muhimu sana katika ukuaji wa uchumi; ni kwa vipi Waziri wa Fedha hana takwimu za kuonesha namna gani ambavyo mgao ambaao unaendelea mpaka hivi sasa umeathiri mapato ya Serikali?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, nimesema wazi kwenye jibu langu la msingi kwamba, mgao wa umeme pekee hauathiri makusanyo ya umeme. Nimesema kwamba, vilevile kuna mambo ambayo

yanaweza yakaathiri kama vile ukuzaji wa uchumi kwa maana kwamba, kama ukuzaji wa uchumi unapaa juu, *obviously*, hata mapato pia yataongezeka kwa maana *GDP* ya Mwananchi itaongezeka. Vilevile nimesema kwamba, Biashara za Kimataifa zinaathiri kwa maana sisi tunategemea *imports*, tusipopata Biashara ya Kimataifa na hatupati *imports* vilevile tutakosa mapato. Nimesema pia hiari ya watu wenyewe, Wananchi kuzoea kulipa kodi; watu hawajazoea kulipa kodi wanakwepa na haya ndiyo matatizo.

Na. 55

Ahadi ya Kupeleka Umeme Kata ya Kibedya na Chakwale

MHE. AHMED M. SHABIBY aliuliza:-

Jimbo la Gairo lina vijiji vingi na ongezeko kubwa la watu wenyewe uwezo na wanahitaji kupatiwa umeme kwani hata Mheshimiwa Rais alipofika jimboni hapo tarehe 28 Agosti, 2009 alilionna hilo na akaahidi kupatiwa umeme Kata za Kibedya na Chakwale haraka iwezekanavyo na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Wataalamu wake walipotembelea Kata hizo baada ya Mheshimiwa Rais na kuliona tatizo hili waliahidi kutekeleza mara moja ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais mapema iwezekanavyo:-

(a) Tarehe 21 Juni, 2010 akijibu swalı langu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini aliliambia Bunge kwamba TANESCO imeshafanya tathmini na utekelezaji wake uko mbioni; je, Serikali italihakikishia Bunge kwamba Mradi huo utakuwepo katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012?

(b) Kama tathmini imefanyika na kwa kuzingatia ahadi ya Mheshimiwa Rais na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Nishati kutekeleza ahadi hiyo kutokana na umuhimu waliouona kwenye Kata hizo; je, kama utekelezaji huo hautawekwa kwenye Bajeti ya Mwaka 2011/2012 sababu za msingi ni zipi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Ahmed Makhbut Shabiby, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Chakwale kilichoko Kata ya Chakwale, Wilayani Gairo, kiko takriban kilometa 12 kutoka Barabara Kuu iendayo Morogoro kutokea Dodoma. Mradi wa kupeleka umeme kwenye Kijiji cha Chakwale utawekwa kwenye Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na matokeo ya upembuzi yakinifu uliofanywa na TANESCO, ili umeme uweze kufika Chakwale, kunahitajika kujengwa njia ya umeme wa kilometa zipatazo 16 za msongo wa kV 33 kutoka Ibuti na kuchepukia Ingorori, kuwekwa transfoma sita na kujenga njia ndogo za msongo wa kV 0.4 kwa urefu

wa kilometra 12 kwenye Vijiji vya Ingiroli, Kibedya A, Kibedya B hadi Chakwale pamoja na Kijiji cha Mtumbatu. Gharama ya kazi hii ni shilingi 1,056,767,316.00. TANESCO imeshawasilisha kwa Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*), maombi ya kupatiwa fedha za ujenzi wa Mradi wa Kupeleka Umeme Chakwale.

Mheshimiwa Spika, kutekelezwa kwa Mradi huo kuanzia 2011/2012, kunategemea upatikanaji wa fedha.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa vile ahadi hii ya kupeleka umeme katika Kata za Chakwale na Kibedya ilikuwa ni ya Mheshimiwa Rais na baada ya kutoa ahadi hii alikuja Mheshimiwa Waziri pamoja na Wataalamu wake na kufanya mukutano wa hadhara na kuwaahidi Wananchi wa Chakwale kwamba watapeleka umeme mara moja katika Kata ya Chakwale; lakini jibu la leo, jibu la tarehe 21 Juni, 2006 na la mwaka 2010 yanafanana!

Je, haoni Mheshimiwa Waziri kuna kila sababu ya yeye kwenda tena pale kwenye Kata ya Chakwale na kuwaambia Wananchi kwamba zile ahadi alizokuwa anazitoa alikuwa anawafurahisha tu lakini hazitekelezeki? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Juni, 2010 tuliposimama hapa tulifafanua tatizo la Chakwale kwa sababu kulikuwa na suala la kufanya tathmini ya ule Mradi. Ninavyokumbuka ni kwamba, pia katika majibu yale kulikuwa na suala la kupeleka umeme kwenye Kata ya Rubeho. Kwa hiyo, majibu hayafanani.

Tulisema kwamba, Miradi ile miwili ambayo Mheshimiwa Mbunge alikuwa anataka kuipata kwa Kata ile ni Miradi ambayo tulikuwa tunatambua umuhimu wake kwa sababu Chakwale ni Kata ambayo ina ongezeko kubwa la watu, lakini pia ina ongezeko kubwa sana la *activity*, shughuli za kiuchumi. Kwa hiyo, tulisema tathmini ile iliyofanywa pale ikaoneshwa wazi kabisa kwamba tunahitaji kupeleka umeme Chakwale ni jambo ambalo tumeliweka kwenye kipaumbele.

Sasa tulichosema ni kwamba, tathmini ya kitaalamu, *project design*, zimefanywa na sasa hivi tunayo na gharama za fedha wakati ule tulikuwa nao tukasema kwamba, kwa mwaka huu wa 2011/2012 tutapeleka pesa *REA*. Sasa kulingana na upelekaji wa pesa *REA* ndiyo tutakamilisha huo Mradi.

Katika ahadi ile tulikuwa tumekubaliana kwamba, tungekwenda mimi na Mheshimiwa Shabiby au Mheshimiwa Waziri mwenyewe angekwenda; sasa hilo lingine la ahadi alilosema mimi ninaamini kabisa kwamba, ahadi ile ipo na imetolewa kwa sababu tunajua umuhimu wa kupeleka umeme Chakwale upo pale pale na ni sehemu ya ahadi ambayo imetolewa na Serikali ya CCM.

Ahadi za Kupeleka Umeme – Nkenge

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA aliuliza:-

Kumekuwepo na ahadi nyingi za muda mrefu za kupeleka umeme katika Kata ya Nsunga, Mtukula, Ishozi, Ishunju na Gera Buyango:-

Je, ni lini mkakati huo utaanza kwani Mtukula upande wa Uganda umeme huwaka lakini upande wa Tanzania huwa giza hivyo kuwa sehemu ya kujificha majambazi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TANESCO, ilishafanya upembuzi yakinifu kwa nia ya kupeleka umeme maeneo ya Mtukula, Nsunga, Ishuzi na Ishufu na kubaini kwamba, inahitajika kujengwa njia ya umeme yenye msongo wa kilovoti 33 ya urefu wa kilomita 26 kutokea Bunazi na kufunga vipoza umeme (*transfoma*) tano kwenye maeneo ya Kata hizo kwa gharama ya shilingi 1,433,119,757.53.

Mpango wa haraka na wa gharama nafuu wa kuipatia umeme Mutukula upande wa Tanzania ni kujenga laini fupi kutoka Mtukula upande wa Uganda wa Tanzania na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme upande wa Tanzania. Wizara ya Nishati na Madini imeagiza TANESCO kukamilisha mazungumzo kwa haraka na Kampuni ya *Uganda Electricity Transmission Company Limited (UETCL)* ili Mtukula (Tanzania) iweze kupatiwa umeme kutoka Uganda. Mawaziri wa nchi zetu mbili, tumekubaliana kukutana na Watendaji wa Mashirika yetu ya Umeme na wadau wengine ili kuhakikisha makubaliano ya kuwezesha kufikisha umeme maeneo haya yanafikiwa haraka.

Mheshimiwa Spika, Kata za Gera na Buyango zimejumuishwa kwenye Miradi ambayo imeainishwa kutekelezwa chini ya Wakala wa Nishati wa Vijijini.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa Mutukula kuna Mradi mkubwa wa Maji wa *UN Habitat* ambao hivi karibuni utakuwa unamalizika na utahitaji kutumia umeme; na kwa kuwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri anasema mpango wa haraka utakuwepo; na kwa kuwa sijui haraka ya wakati gani na ni lini; na ukizingatia kwamba umeme sasa hivi upo kilomita 20 tu kutoka pale kuelekea Mtukula; je, hiyo haraka itakuwa lini ili Wananchi wa Mtukula wapate kuondoka katika giza nene?

(ii) Kwa kuwa Kata ya Kitobo inao umeme ambao hautoshelezi na tayari watu walishatoa pesa zao kwa ajili ya kufungiwa umeme majumbani; je, huu siyo wakati mzuri wa kufunga hiyo transfoma ili watu waweze kufaidi na kuweza kupata umeme majumbani mwao na kuongeza Pato la Taifa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, swali lake nimejaribu kumweleza kwamba, *plan* ya kwetu sisi ni kupeleka pale ule Mradi kama tulivyouainisha, lakini kuna namna mbadala ya kupata umeme pale ambapo ni kuutoa Uganda. Tarehe 19 Mei, 2011 Mawaziri wa *East African Powerpool* wanakutana Kigali, Rwanda. Mimi nimeongea na Waziri wa Uganda wiki iliyopita na tumekubaliana mpaka tukifika tarehe 19 Mei, 2011 masuala yote yanayohusu *crossborder electrification* upande wa Tanzania na Uganda yawe yamekamilika tarehe 19 Mei, 2011 ili yapate kuzungumziwa na Mawaziri wa Tanzania na Uganda watakapokuwa pamoja Mjini Kigali. Hakuna haraka zaidi ya hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni kwamba, kilomita 20 anazosema siyo ndogo. Kwa kila kilomita moja wastani wa kupeleka umeme maeneo ya kule ni zaidi ya shilingi milioni 40. Kwa hiyo, ukichukua hizi na hiyo transfoma na kadhalika, hapa kuna Mradi wa karibu shilingi bilioni moja ukifanyiwa tathmni kamili. Kwa hiyo, siyo Mradi mdogo lakini Serikali imeahidi kwamba, kwa njia ya haraka tutazungumza na wenzetu wa Uganda, tuone kama tutautoa upande wa Mtukula na kuusambaza kule *notwithstanding* mipango hii ambayo sisi wenyewe tunayo.

Mheshimiwa Spika, ameuliza Kata ya Kitobo, labda nimwambie umeme upo Kata ya Kitobo na kuna mpango wa kupanua mtandao wa umeme chini ya Mpango wa TANESCO kwa mwaka 2011, ambapo itakuwa kujenga laini ya umeme wa msongo wa kilovoti kama kilomita 1.5 hivi kwa kiasi cha kama shilingi milioni 57 na kusambaza nyaya za umeme, *low transmision line*, kama kilomita mbili kwa gharama ya kama shilingi milioni 56 pamoja na tranfoma moja kwa shilingi milioni 20. Kwa hiyo, jumla yake ni kama shilingi milioni 35. Mpango huo upo, unatarajiwa uingie kwenye *plan* ya TANESCO, lakini Kitobo umeme upo. Kwa hiyo, hii ni kuboresha upatikanaji wa umeme.

Na. 57

Matumizi ya Bonde la Mto Mkomazi

MHE. STEPHEN H. NGONYANI aliuliza:-

(a) Je, ni lini Bonde la Mkomazi litaimarishwa ili liweze kutumika vizuri kwa kilimo cha umwagiliaji kwenye mashamba ya Kata za Mkomazi, Mazinde, Mombo, Makuyuni na Magamba Kwalukonge?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa uendelezaji wa Mradi huo utatimiza dhamira ya kuendeleza kilimo kuitia Mpango wa Kilimo Kwanza na kuboresha uchumi wa mkulima wa maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Bonde la Mto Mkomazi kwa wakulima katika Kata za Mkomazi, Mazinde, Mombo, Makuyuni na Magamba. Kwa nyakati tofauti tangu mwaka 1962, Serikali imefanya uchunguzi wa maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji pamoja na kufanya uchunguzi wa kitaalam kuhusu ubora wa maji na udongo kwa ajili ya umwagiliaji. Utafiti huo umeonesha kuwa, maeneo mengi yana matatizo ya chumvi nyingi katika udongo na hayafai kwa umwagiliaji. Aidha, kwa maeneo ambayo udongo wake unafaa kwa umwagiliaji, Serikali inaendelea kuyaboresha kwa awamu kwa kujenga skimu ndogondogo za umwagiliajia. Skimu ambazo zimejengwa ni pamoja na Mombo, Mazinde, Bagamoyo, Muhuza, Mazinde, Mafulea na Mswaha Darajani.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imekwishafanya uchunguzi kwa ajili ya ujenzi wa bwawa kubwa kwenye Mto Mkomazi katika Kijiji cha Mikocheni/Mitindiro kwa ajili cha umwagiliaji. Bwawa hili bado halijajengwa kutokana na gharama yake kuwa kubwa na pingamizi lililowekwa na Wananchi wa Manga Mikocheni, ambao mashamba yao na sehemu ya makazi yao vitamezwa na bwawa hilo pindi litakapojengwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu na Halmashauri ya Korogwe, itaendelea kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo yote yanayofaa kuitia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ya Korogwe.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yamenielewesha ila nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa Wananchi wa Mikocheni wamekubaliana kupisha ujenzi wa bwawa hilo; je, Serikali ipo tayari kutenga pesa kwa ajili ya ujenzi huo?

(ii) Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kwenda na mimi kujiona mwenyewe tatizo linalowapata Wananchi wa eneo hilo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, najibu kwa furaha kabisa kwamba, bwaha hilo sasa tutaliweka katika utaratibu kwa sababu hapo nyuma Wananchi walikuwa wameweka pingamizi mpaka walidiriki kwenda kwa *Sangoma* kuzuia lisijengwe. Sasa kama wamekubaliana, tutaanza mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimefurahi baada ya hapo nitakwenda naye na tutaangalia namna ya kuliweka kwenye mchakato.

SPIKA: Walikwenda kuroga kwa *Sangama*!! Sasa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda; samahani nimeruka, nimwite Mheshimiwa Josephine Joseph Genzabuke.

Na. 58

Miradi ya Umwagiliaji Kigoma

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Mkoa wa Kigoma ni mionganini mwa mikoa sita iliyoinishwa kuzalisha chakula kwa wingi. Mkoa huu umejaliwa mito mingi pamoja na Ziwa Tanganyika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendelza Miradi ya Umwagiliaji katika Mabonde ya Luiche, Mukuti, Titye, Rungwe Mpya, Mgondogondo, Ruguzye na kadhalika?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha umwagiliaji wa mazao ya biashara likiwemo Zao la Pamba hasa katika Mkoa wa Kigoma?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji wa Mwaka 2002 ulibaini hekta 538.800 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Kigoma. Serikali inatambua mchango wa Mkoa wa Kigoma katika uzalishaji wa mazao ya chakula na hivyo Mkoa umejumuishwa katika Mikoa sita yenye uwezo mkubwa wa kuzalisha chakula nchini. Mikoa mingine ni Mbeya, Iringa, Rukwa, Ruvuma na Morogoro.

Serikali imekwishaanza kutekeleza miradi midogo ya wakulima kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo (*DADPs*) katika Wilaya za Kigoma, Kasulu na Kibondo. Miradi inayotekelze wa ni Mkuti (120 hekta) katika Wilaya Kigoma na Nyaganya (200 hekta) iliyopo Uvinza. Titye (500 hekta), Rungwa Mpya (300 hekta), katika Wilaya ya Kasulu. Miradi mingine ni Mgondogondo (212 hekta) Ruguzye (145 hekta), Nyindala (160 hekta), Bugunga (140 hekta) Muhwazi (230 hekta), Mwiruzi (153 hekta), Ruhwichi (140 hekta), Katengera (207 hekta), Kahambwe (145 hekta), Nyendera (160 hekta) na Nyaronga (153 hekta) katika Wilaya ya Kibondo.

Kwa upande wa miradi mikubwa yenyе zaidi ya hekta 3145 katika mabonde ya Luiche na Ruguzye, Wizara yangu inatafuta fedha katika Mfuko wa Taifa (*National Irrigation Development Fund*) ili miradi hiyo itekelezwe kwa ufanisi zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa kitaalamu uliofanywa umeonesha kwamba, umwagiliaji maji unaweza kuongeza tija katika uzalishaji wa pamba kutoka tani 0.3 kwa hekta hadi tani 2.5 kwa hekta. Kwa kuwa Zao la Pamba lina mchangano mkubwa katika kuliletea Taifa fedha za kigeni na kuwaongezea kipato wakulima, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu inatarajia kuanzisha miradi ya mfano ya umwagiliaji wa pamba kwa njia ya matone (*Drip Irrigation*) katika Wilaya za Kibondo na Maswa. Miradi hiyo itasimamiwa kwa pamoja na Bodi ya Pamba na Ofisi za Umwagiliaji Kanda za Umwagiliaji Tabora na Mwanza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya kumwuliza:-

(i) Kwa kuwa ipo Miradi miwili iliyokwishaanzishwa katika Kijiji cha Titye na Rungwe Mpya na aliyekuwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Wasira pamoja na Waziri Mkuu wamewahi kutembelea Miradi hiyo na kuahidi kuwa pesa zitatolewa kwa ajili ya kuikamilisha; je, ni lini Serikali itatao pesa kwa ajili ya kukamilisha Miradi hiyo ili Wananchi waweze kulima kilimo chenye tija na kujiinua kiuchumi?

(ii) Je, wakulima watawezeshwa vipi ili waweze kukopa fedha katika mabenki kwa ajili ya kununua zana za kilimo kama pampu kwa ajili ya umwagiliaji?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nilipokuwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, niliitembelea Miradi hii miwili. Baada ya kukuta imezorota na fedha zilikuwa zinatumika vibaya, niliagiza fedha zile zisipelekwe tena mpaka ifanywe tathmini upya. Sasa tathmini imeshafanywa na kwa bahati kazi imekwishaanza na Mkandarasi yuko *site* na kazi katika Mradi wa Titye imefikia asilimia 65 na mwisho wa mwaka 2011 tunatarajia sasa Mradi huo utakuwa tayari. Mradi wa Rungwe Mpya kwa bahati pia alipotembelea Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi nilikuwepo, maelekezo yake yalitekelezwa na sasa Mkandarasi yuko *site* na kazi imefikia asilimia 70. Kwa hiyo, miradi hii inaendelea vizuri sasa na tunatarajia mwisho wa mwaka huu, itakuwa tayari na kuendelea kutumiwa na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uweshejaji, utaratibu ni uleule kwamba, tunapenda wakulima wajunge katika vikundi lakini pia ninapenda nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mfuko wetu wa Pembejeo, umeshaacha utaratibu wa kukopesha matrekta na mbolea. Sasa hivi hata zana za kilimo zinakopeshwa pamoja na pampu. Kwa hiyo, ninaomba Maafisa wa Kilimo wawasadie Wananchi kuandaa maandiko kwa ajili ya kuomba mikopo kwa ajili ya zana za kilimo cha umwagiliaji kutoka kwenye Mifuko ya Pembejeo.

Tatizo la Maji Mchinga

MHE. SAIDI M. MTANDA aliuliza:-

Tatizo la maji limewafanya Wananchi wa Vijiji vya Namkongo, Lihimilo, Likwaya na Kilolambwani kutumia zaidi ya saa nne kila siku kutafuta maji:-

(a) Je, Serikali itawezaje kutekeleza azma ya Mheshimiwa Rais ya ya maisha bora kwa kila Mtanzania bila upatikanaji wa maji?

(b) Je, Serikali iko tayari kufanya tathmini ya haraka na kuchukua hatua za dharura kutatua tatizo hilo la maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Mchinga, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuwapatia Wananchi wake huduma bora za jamii ikiwa ni pamoja na majisafi na usafi wa mazingira ili kuboresha maisha na kuleta maendeleo ya kiuchumi. Ahadi hiyo ya Serikali ilitolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa Uchaguzi wa Mwaka 2005. Ili lengo la kuwapatia Wananchi wa Vijijini majisafi litimie, mwaka 2005/2006l Serikali iliandaa Programu ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Programu hiyo inalenga kuboresha huduma ya majisafi kwa wakazi wa vijijini kufikia asilimia 65 ifikapo mwaka 2015 kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005.

Programu hiyo inatekeleza Mradi wa Vijiji Kumi vya Kipaumbele katika Halmashauri zote nchini. Halmashauri ya Wilaya ya Lindi katika kutekeleza Mpango huo, Vijiji vya Namkongo, Likwaya na Kilolambwani ni mojawapo ya vijiji kumi vya kipaumbele. Vijiji vingine ni Kiawa, Chikonji, Hingawali, Nyamagana, Litipu, Nahukahuka, Rondo, Mnazimmoja, Mingoyo na Namangale.

(b) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Miradi ya Vijiji Kumi katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi umefikia hatua ya kuridhisha. Mwezi Mei, 2009 Halmashauri ilimwajiri Mtaalam Mshauri, *Don Consult Limited*, kwa ajili ya kufanya utafiti wa vyanzo, upimaji na usanifu . Baada ya utafiti wa vyanzo vya maji kukamilika, mwezi Aprili, 2010 Halmashauri hiyo ilimwajiri Mkandarasi Ardhi, *Water Wells Ltd* na *Pumps International and Solar Ltd*, ambaye amekamilisha uchimbaji wa visima. Kazi inayoendelea na Mtaalam Mshauri ni kukamilisha usanifu wa miundombinu ya usambazaji maji. Ujenzi wa miundombinu hiyo utaanza Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi inashauriwa kukiweka Kijiji cha Lihimilo katika Mipango yake ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 ili kuikamirisha huduma ya maji katika kijiji hicho.

MHE. SAIDI M. NTANDA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Waziri yameonekana ni ya kinadharia zaidi ukilinganisha na hali halisi ya Mradi wa Maji wa Kilolambwani, Likwaya na Namkongo:-

(i) Je, Mheshimiwa Waziri wa Maji atakuwa tayari kwenda na mimi katika maeneo aliyoyataja ili kujionea hali halisi?

(ii) Kwa kuwa Mradi huu wa *World Bank* ulianza mwaka 2008 na umeshindwa kufikia hatma hadi leo hii na Wananchi wamekuwa hawana uwezo wa kupata maji katika eneo hilo. Je, Serikali iko tayari kuingilia kati na kuunusuru Mradi huu wa Maji katika Kijiji cha Kilolambwani, Likwaya na Namkongo badala ya kutegemea *World Bank* toka mwaka 2008 wameshindwa kuukamilisha Mradi kwa wakati?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba; si kwamba ni majibu ya kinadharia. Tunaelezea hali halisi, hatua ambayo imefikiwa. Tunasema Don Cosult amefanya usanifu na Mkandarasi ameshachimba visima. Kazi inayoendelea sasa ni kutengeneza miundombinu ili kusambaza yale maji. Ninakubali mwaliko wake wa kwenda kuangalia, nitakwenda na wataalam wangu tukaangalie hatua hiyo ambayo imefikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika swalii la pili, suala kwamba, *World Bank* wanachelewesha Miradi; hilo si kweli. Mradi huu wa Vijiji Kumi unatekelezwa na Serikali pamoja na *World Bank*. Kwa hiyo, Serikali ina majukumu yake, *World Bank* wao wanafadhili fedha, lakini kuna mambo ambayo tumekubaliana. Hatua moja ikiisha tunakwenda hatua ya pili; kwa hiyo, lazima twende kwa hatua ambazo tumekubaliana na hawa wafadhili amba wanatusaidia katika Miradi ya Sekta ya Maji.

Na. 60

Uhaba wa Maji – Manyovu

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Vijiji vingi katika Jimbo la Manyovu vina tatizo kubwa la maji, hivyo kuhitaji visima virefu:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili kuondoa adha ya maji katika vijiji hivyo?

(b) Je, Serikali inakubaliana kuwa kuna umuhimu wa kuongeza fedha katika Bajeti za Halmashauri ili ziweze kutosheleza?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Jimbo la Manyovu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jimbo la Manyovu lipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na lina jumla ya vijiji 34 na jumla ya wakazi wapatao 351,561. Hadi mwezi Desemba, 2010 wakazi 139,475, sawa na asilimia 40 wanapata huduma ya majisafi kuititia vyanzo mbalimbali vikiwemo mito, chemchemi, visima vifupi na virefu na matenki ya kuvuna maji ya mvua. Jitihada mbalimbali zimechukuliwa na Serikali kuhakikisha kuwa, Wakazi wa Jimbo hilo wanapata maji kwa kutumia teknolojia rahisi inayopatikana katika kijiji husika.

Ili kupunguzq tatizo la maji katika Jimbo la Mnyovu, mwaka 2007/2008, Serikali ilianza kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa kujenga Miradi yenye kuleta matokeo ya haraka, maarufu kama *quickwins*. Jumla ya shilingi milioni 214.3 zilipelekwa katika Halmashauri ya Kasulu na kutumika kujenga na kukarabati Miradi ambapo jumla ya Wananchi 13,752 wamenufaika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudini zilizofanyika, Serikali bado inaendelea kuboresha huduma ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa kutekeleza Mradi wa Vijiji Kumi ambapo vijiji sita ni vya Jimbo la Manyovu. Vijiji hivyo ni Mabunga, Nyamugali, Bulimanyi, Kirungu, Munzeze na Kigongwe. Mtaalam Mshauri, *M/S Engineering Research associates*, akishirikiana na *Hydraulic and Sanitation Consult Ltd* na *Water and Environment Sanitation Project Maintenance Organization*, aliajiriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Mtaalam huyo kwa sasa anafanya usanifu wa kina wa Miradi na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kupata Wakandarasi. Jumla ya shilingi milioni 263.5 tayari zimepelekwa katika Halmashauri hiyo kwa ajili ya kutekeleza Miradi iliyoitajwa.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kuwa, upo umuhimu wa Serikali kuziongezea bajeti Halmashauri za Wilaya katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 ili ziweze kutekeleza Miradi mingi zaidi. La muhimu ni Halmashauri kuweka Miradi ya Sekta ya Maji kweneye vipaumbele vya mipango yao ya maendeleo.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze maswali mawili ya nyongeza.

(i) Ninashukuru kwa majibu mazuri ingawa yamejaribu kuonesha kwamba ni vijiji sita katika vijiji 34 ambavyo angalau vinafikiriwa; lakini vilevile hivi vijiji vina matatizo ya maji na tumekuwa tukipewa majibu hayo hayo kwa muda mrefu sana. Sasa sitaki kubishana na yeye; ni lini hii Miradi hiyo itakamilika; na je, vijiji vingine ambavyo havikutajwa katika majibu yake Wananchi wa Jimbo la Manyovu unawaahidi nini juu ya maji?

(ii) Jimbo la Manyovu limebahatika kupewa Wilaya ya Buhigwe, Ile Wilaya maji yake hayatoshi. Je, Wizara ina mpango gani wa kuongeza maji kwa Wilaya inayoanza Julai?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anauliza ni lini Miradi hii itakamilika. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, katika kutekeleza huu Mradi wa Vijiji Kumi, tunakwenda hatua kwa hatua. Kwa hiyo, jinsi ambavyo tunafanya utekelezaji wa haraka na jinsi usanifu unapokuwa umekamilika na jinsi Wilaya inavyoweka kipaumbele katika kuzipangia fedha, kwa sababu lazima Halmashauri ya Wilaya iweke *allocation* ya fedha za kutosha kwa Miradi ya vijiji vile ili uweze kutekelezwa. Kwa hiyo, jinsi tatakavyokuwa tunaweka fedha za kutosha na hapa tumeahidi kwamba, Serikali itaongeza Bajeti ya Serikali, nina uhakika kabisa utekelezaji wake utakwenda kwa haraka zaidi. Azma ya Serikali ni kuhakikisha vijiji hivi vinapata maji ya kutosha ifikapo mwaka 2015.

Suala la pili kwamba, hiyo Wilaya mpya maji hayatoshelezi. Nakubaliana naye kwamba, hayatoshelezi. Tutafanya tathmini na kuona vyanzo ni vipi na kwa sababu Mtaalam Mshauri yupo kule, atatupa ushauri ni wapi tunaweza tukapata maji ya kutosha kwa ajili ya Wilaya hiyo mpya.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha tena umepita na maswali tuliyokuwa nayo yamekwisha. Ninao wageni katika *Speakers' Gallery*. Kwanza kabisa, tuna Afisa wa Bunge la Malawi, amekuja kwenye ziara ya mafunzo katika Bunge la Tanzania, Ndugu Steve Banda. Huyu ni Afisa wa Bunge la Malawi na sisi pia huwa tunakwenda kujifunza kwa wenzetu. Karibu sana na ufanye kazi vizuri. Halafu yupo Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Bi. Blandina Nyoni; karibu. Ninajua leo tuna Muswada wa Famasia, kwa hiyo, yeye ndiye muhusika.

Waheshimiwa Wabunge, wakati huo huo nina wageni wangu wengine kutoka mhimili mwingine wa Dola wa Mahakama; Kwanza kabisa, nina Mheshimiwa Jaji Fakhi Jundu (Jaji Kiongozi). Ahsante, karibu. Nina Mheshimiwa Jaji Mary Shangari (Jaji Mfawidhi - Dodoma); na Mheshimiwa Jaji Kipenka Mussa (Jaji Mfawidhi – Tanga), lakini huyu alikuwa Katibu wa Bunge, amefanya kazi sana na sisi na baadhi ya mapinduzi tuliyonayo kwenye Kanuni zetu alishiriki sana katika kufanya hiyo kazi. Ninakushukuru, karibu sana.

Wengine ni Mheshimiwa Jaji Mewanaisha Kwariko, yeye ni Jaji Mahakama Kuu Dodoma; Mheshimiwa Jaji Shivangilwa Mwages – Jaji Mahakama Kuu Dodoma; Mheshimiwa John Karyoza – Msajili Mahakama ya Biashara; Mheshimiwa Rutanisibwa – Msajili Mahakama Kuu; na Ndugu Mohamed Chengelwa – Msaidizi wa Jaji Kiongozi. Hawa wote wamekuja kushirikiana na sisi katika Muswada wa Utawala wa Mahakama katika *Public Hearing* watakuwepo wao na watu wengine pia watakuwepo. Kwa hiyo, mnakaribishwa sana, nadhani mtakuwa na sisi katika siku zinazofuata.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi: Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 5.00 asubuhi kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Msekwa B. Kamati ya Viwanda na Biashara mkutane leo saa 5.00.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa George Simbachawene, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo na Wabunge wote kwamba, Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo, itakuwa na Mkutano wa Kusikiliza maoni ya Wadau (*Public Hearing*), kuhusu Muswada wa Sheria ya Utawala wa Mahakama (*The Judicial Administration Bill, 2011*), leo tarehe 11 Aprili, 2011 katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia asubuhi saa 5.00. Wajumbe wa Kamati, mnaombwa kuhudhuria bila kukosa na pia Wabunge wengine mnakaribishwa kutoa maoni yenu kuhusu Muswada huo.

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema, tukiuangalia vizuri Muswada huu, utahusisha na Sheria yetu ambayo tumeanza nayo, lakini ninadhani tumeona upungufu wake. Kwa hiyo, mkiangalia vizuri hii itasaidia kufanya marekebisho katika sheria ile nyingine.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 5.00 asubuhi kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, yeye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 5.00 asubuhi kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Na. 227, Ghorofa ya Pili.

Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa January Makamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, kutakuwa na Kikao cha Kamati kuanzia saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 219.

Mheshimiwa Namelok Edward Moringe Sokoine, kwa niaba ya Familia ya Hayati Edward Moringe Sokoine, aliyekuwa Waziri Mkuu, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, *Edward Moringe Sokoine Trust* wanawatangazia Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote kwamba, tarehe 12 Aprili, 2011, Siku ya Jumanne, saa 9.00 alasiri, kutakuwa na Ibada Maalum ya kumwombea Hayati Edward Moringe Sokoine, aliyefariki kwa ajali ya gari tarehe 12 Aprili, 1984, Wami – Dakawa, Morogoro.

Ibada hiyo itafanyika katika Kanisa la Mtakatifu Paulo wa Msalaba (Kanisa Kuu la Katoriki Dodoma eneo la Uwanja wa Ndege); wote mnaombwa kuhudhuria. Haiwezekani, kwa sababu Kanisa Kuu liko Mlezi; sasa Uwanja wa ndege sijui kuna nini! Basi, mkihudhuria Kanisani mtajua kwamba kuna shughuli nyingine. Uwanja wa Ndege kuna shughuli gani Mheshimiwa Namelok?

MHE. EDWARD N. LOWASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni Kanisa Kuu.

SPIKA: Ni Kanisa Kuu, Uwanja wa Ndege hapa hakuna.

MHE. EDWARD N. LOWASSA: Ni makosa, ni Kanisa Kuu.

SPIKA: Kwa hiyo, Ibada saa 9.00 kesho katika Kanisa Kuu la *Roman*. Watu wote mnakaribishwa na kutakuwa na shughuli.

Halafu juzi nilitangaza kwamba, mtakuwa na Uchaguzi wa Viongozi wa *Bunge Sports Club*. Sasa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Idd Azzan, anaomba niwaeleze matokeo. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-

Viongozi waliochaguliwa ni Mwenyekiti, ambaye ni Mheshimiwa Idd Azzan, Makamu Mwenyekiti ni Mheshimiwa Amos Makala, Msimamizi Mkuu wa Mazoezi, Mheshimiwa Eng. Habib Juma Mnyaa na Kocha wa Mpira wa Miguu ni Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa.

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji yupo Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Habib Mnyaa, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mhehimiwa Mwanakhamis Said na Mheshimiwa Betty Machangu. (*Makofi*)

Halafu, kuna Kamati ya Ufundu na maeneo muhimu wanayotoka; yasikilizeni haya: Yupo Mheshimiwa Stephen Ngonyani, huyu anatoka Tanga, halafu anaitwa Profesa Maji Marefu; Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, huyu anatoka Bagamoyo; Mheshimiwa Hawa Ghasia, yeeye anatoka Mtware huko; Mheshimiwa Khalfan Aeshi, huyu anatoka Sumbawanga; Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, anatoka Pemba; Mheshimiwa Maria Hewa anatoka Mwanza; na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura anatoka Tunduru. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa sikilizeni mlezi wao; mlezi wa Kamati ya Ufundu na Timu ya Bunge anatoka Sumbawanga ni Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda. Kwa hiyo, naona wamekamilika. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa Sekretarieti: Yupo Ndugu Carlos Kidiru, Ndugu Michael Kadebe na Ndugu Waziri Kizingiti. Hao ndio Sekretarieti. Pamoja na hilo, ninaomba niwatangazie kwamba, Timu ya Yanga jana imetwaa ubingwa na kwa sababu ambazo sizifahamu, anasema nimweleze Mheshimiwa Ngeleja apate habari hii. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo yaliyokuwepo hapa. Kama mtakavyoona *Order Paper*, sasa tutaendelea na Miswada. Muswada utakaofuata ni Muswada wa Sheria ya Famasia wa Mwaka 2010.

Mimi nina shughuli yingine, nina wageni kama nilivyowataja, ninaomba Mheshimiwa Naibu Spika, anisaidie.

Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Timu ya Simba wamekuwa washindi wa pili! (*Kicheko*)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Famasi wa Mwaka 2010 (The Pharmacy Bill, 2010)

(Kusomwa Mara ya Pili)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa ninaomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii; karibu.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Famasi wa Mwaka 2010 (*The Pharmacy Act, 2010*), kama ulivyopangwa katika shughuli za leo, pamoja na Jedwali la Marekebisho, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuendelea na hoja yangu, ninaomba kutoa maelezo ya awali kuhusu chimbuko la Muswada wa Sheria ya Famasi. Mchakato wa uandaaji wa Muswada huu, ultokana na maamuzi ya Baraza la Mawaziri, kupitia Waraka Na. 17 wa Mwaka 2009/2010. Katika Waraka huo, Baraza, pamoja na mambo mengine, lilielekeza kutungwa kwa Sheria mpya ya Famasi itakayofuta Sheria ya Famasi, Sura Na. 311, ambayo ndiyo Sheria inayotumika hivi sasa.

Kutungwa kwa Sheria hii, kutaongeza uwezo wa Baraza katika kusimamia Taaluma ya Famasi, ikihusisha utoaji wa huduma za dawa nchini, utoaji vibali vya kusambaza dawa, maeneo ya maduka ya dawa muhimu (*Accredited Drug Dispensing Outlets – ADDO*) na kufuatilia wanataaluma katika sehemu wanazofanya kazi. Baraza la Mawaziri lilifikia maamuzi haya, kufuatia upungufu uliojitokeza katika utekelezaji wa Sheria ya sasa na usimamizi wa Taaluma ya Famasi, kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu uliwasilishwa katika Kamati ya Katiba, Sheria na Bunge ya Baraza la Mawaziri hapo tarehe 14 Aprili, 2010. Katika Kikao hicho, Muswada ulijadiliwa na mapendekezo yaliyotolewa, yalizingatiwa katika Muswada huu. Muswada ulichapishwa katika Gazeti la Serikali, Toleo Na. 16 la tarehe 16 Aprili, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu uliwasilishwa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, tarehe 19 Aprili, 2010 hapa Dodoma na maoni ya wadau mbalimbali yalipokelewa tarehe 20 Aprili, 2010. Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, iliwasilisha majibu ya hoja za Kamati na Wadau, tarehe 21 Aprili, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulitarajiwa kuwasilishwa katika Bunge la Tisa, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, tarehe 22 Aprili, 2010. Hata hivyo, haukuweza kuwasilishwa na kujadiliwa kama ilivytarajiwa kutokana na shughuli nyingi za Bunge na hivyo, kuahirishwa kwa uwasilishwaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchukua fursa hii, kuwashukuru Wajumbe waliopita wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, chini ya Uenyekiti wa aliyekuwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Haji Mwita Haji (Mb), kwa kukubali kuupokea na kuuchambua Muswada huu.

Vilevile, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya sasa ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Margaret Sitta, kwa kukubali kupokea Muswada na Maoni ya Wadau tarehe 23 na 24 Machi, 2011, Mjini Dar es Salaam na tarehe 8 Aprili, 2011 hapa Dodoma na hatimaye kukubali Muswada huu uwasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuzipongeza Kamati zote mbili, kwa kuchambua Muswada huu kwa kina na kutoa michango na maoni, ambayo yameniwezesha kuwasilisha Muswada huu, hapa Bungeni.

Jedwali la Marekebisho ni matokeo ya uchambuzi huo kutoka kwenye Kamati hizi. Ninapenda pia kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Jaji Frederick Werema, katika mchakato mzima wa kuandaa Muswada huu na Jedwali la Marekebisho ambalo limezingatia maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii pamoja na Wadau wote waliochangia katika kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niwatambue na kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika kutoa maoni yao mbele ya Kamati iliyopita, tarehe 20 Aprili, 2010 hapa Dodoma.

Wadau hao ni pamoja na SIKIKA, ambapo zamani ilikuwa Inajulikana Kama *Action Youth Volunteers*, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Mtakatifu John's - Dodoma, Dayosisi ya *Central Tanganyika, Upendo Pharmacy, Legal and Human Right Centre, Twins Pharmacy*, Hospitali ya Mkoa wa Dodoma na *Chamwino Pharmacy*.

Vilevile, ninapenda kuwatambua na kuwashukuru Wadau wote walioshiriki katika kutoa maoni yao mbele ya Kamati ya sasa, tarehe 23 na 24 Machi, 2011, Mjini Dar es Salaam.

Wadau hao ni pamoja na Hospitali ya Massana, Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shiriki Muhimbili (*MUHAS*), Dar es Salaam, *Tanzania Pharmaceutical Industry* - Arusha, Chama cha Wafamasia Tanzania, Chama cha Fundi Dawa Sanifu Tanzania, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam, *Catholic Relief Services, Veterinary Council of Tanzania, The Aga Khan Hospital*, Dar Es Salaam, Chama cha Hospitali Binafsi Tanzania, *Tanzania Association of Pharmaceutical Industry, Legal and Human Right Centre*, SIKIKA na Chuo cha Fundi Dawa Sanifu Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wadau wote hao, walitoa michango mizuri, ambayo kwa kiasi kikubwa, imechangia katika kuandaa Jedwali la Marekebisho. Sina budi kuwashukuru na ninaomba ushirikiano wao katika kuiendeleza Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nieleze chimbuko la Muswada huu. Chimbuko la mchakato wa kuandaa Muswada huu lilitokana na maamuzi ya Serikali kupitia Baraza la Mawaziri Mwaka 2009.

Uamuzi huo pamoja na mambo mengine, ulielekeza kutungwa kwa Sheria mpya ya Famasi, itakayofuta Sheria ya Famasi, Sura Na. 311 ya Sheria za Tanzania, ambayo ndiyo Sheria inayotumika sasa.

Uamuzi wa Serikali ultokana na upungufu uliojitokeza katika utekelezaji wa Sheria ya sasa na udhaifu katika usimamizi wa Taaluma ya Famasi kwa ujumla. Baadhi ya upungufu huo ni pamoja na:-

- Wigo mdogo wa udhibiti wa shughuli za kitaaluma. Kwa mfano, kutokuwa na vifungu vya kusimamia usambazaji wa dawa maeneo ya kutolea huduma za dawa, kama vile Famasi, Maduka ya Dawa Muhimu (*ADDO*) na kwenye vituo vya kutolea huduma za tiba.
- Vile vile mlolongo wa kuchukua hatua endapo Mwanataaluma atabainika amekiuka maadili ambapo hulazimu Baraza la Famasi kupata taarifa kutoka kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa ndipo liweze kuchukua hatua, na hivyo kuchelewesha uchukuaji wa hatua kwa wakati muafaka.
- Kutokuwa na uwakilishi mpana wa Wajumbe wa Baraza kwa kuhusisha wadau wengi.
- Kutokuwa na adhabu zisizolingana na uzito wa makosa ya kitaaluma.
- Kutokuwa na uwezo wa kisheria wa kuzitambua na kuzifutilia shughuli za kitaaluma za famasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upungufu huu umeathiri kwa kiasi kikubwa udhibiti wa taaluma ya Famasi katika utoaji wa huduma za dawa nchini katika maeneo yote husika kama ambavyo baadhi yameoneshwah hapo mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kutunga sheria mpya ya famasi ambayo pamoja na mambo mengine itafuta Sheria ya Famasi ya sasa ili kutoa uwezo wa Baraza la Famasi kudhibiti taaluma hii ya Famasi katika utoaji wa huduma za dawa nchini. Pia Muswada huu unapendekeza kulipa mamlaka Baraza ya kutoa vibali ikiwemo ya usambazaji wa dawa na kusimamia maeneo ya maduka ya dawa na yale ya *ADO*.

Kupanua uwakilishi wa Wajumbe wa Baraza kuainisha makosa na adhabu zitakazotolewa kwa wanataaluma wanaokiuka maadili au sheria na kuwatambua watoa

huduma za dawa kwa kubaini huduma za kitaaluma wanaokiuka maadili au sheria na kuwatambua watoa huduma za dawa kwa kubaini huduma za kitaalamu wanazozitoa.

Vile vile mpango wa maduka ya madawa muhimu *ADO* utaendeshwa chini ya Mamlaka ya Chakula na Dawa hadi utakapokamilika kusambaza Mikoa yote. Kwa sasa mpango huu upo katika hatua za mwisho za kusambazwa katika Mikoa yote kwa ufadhili kutokana na wadau wa maendeleo kupitia *TFDA*.

Katika usimamizi wa mpango huu ikiwa ni pamoja na usimamizi wa kazi za taaluma za Famasi, Baraza litateua wasimamizi (*supervisory officers*) katika ngazi ya Mko na Wilaya ambao ni Wafamasia wanaofanya kazi hizo kwa sasa chini ya Mamlaka ya Chakula na Dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama yafuatayo:-

- (a) Kujumuisha majukumu ambayo yanapaswa kusimamiwa na Baraza la Famasi, ambayo kwa sasa yanasmamiwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania;
- (b) Kuwa na uwakilishi wa Wajumbe wa Baraza la Famasi ambao utazingatia matakwa (*interest*) ya wadau mbalimbali;
- (c) Kuweka utaratibu wa uanzishaji, usajili na usimamizi wa huduma za usambazaji wa dawa kutoka kwa watengenezaji na waagizaji dawa, pamoja na wale wenye maduka ya dawa nchini;
- (d) Kutamka kupitia Gazeti la Serikali kada za wanataaluma watakosajiliwa, kuorodheshwa na kuandikishwa;
- (e) Kuainisha adhabu kulingana na aina ya makosa yanayofanywa na wanataaluma;
- (f) Kutoa uwezo wa Baraza la Famasi la kuteua wakaguzi wa huduma zinazotolewa na taaluma katika ngazi mbalimbali; na
- (g) Kuweka bayana utaratibu wa kutangaza orodha ya wanataaluma waliosajiliwa na kupewa leseni katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu sita na ibara 57 kwa mpangilio ufuatao:-

Sehemu ya Kwanza yenye Ibara ya (1) na (2) inahusu mambo ya utangulizi ambayo ni jina la sheria inayopendekezwa kutungwa, tarehe ya kuanza kutumika na sheria hiyo na tafsiri ya maneno mbalimbali katika Muswada wa sheria hii.

Sehemu ya Pili yenye Ibara (3) hadi ibara ya (13) inahusu masuala ya utawala kwa ujumla. Sehemu hii inaaniszha Baraza la Famasi, Mamlaka na kazi zake, uteuzi wa Wajumbe, uteuzi wa Msajili na Naibu Msajili na Mamlaka ya Baraza kuanzisha Kamati ndogo za Baraza kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza.

Sehemu ya Tatu yenye Ibara 14 hadi Ibara ya 33 inapendekeza masharti ya usajili kwa wanataaluma wa Famasi katika ngazi mbalimbali chini ya sheria inayopendekezwa, sifa za usajili, utaratibu wa Usajili na utoaji vyeti vya usajili chini ya sheria katika ngazi mbalimbali.

Sehemu ya nne yenye Ibara ya 34 hadi Ibara ya 44 inaweka utaratibu wa usajili wa biashara ya usambazaji wa dawa kutoka kwa watengenezaji na waagizaji wa nje pia wa majengo na utoaji vibali vya usimamizi wa taaluma katika biashara ya Famasi na maduka ya dawa muhimu (*ADO*).

Sehemu ya Tano yenye Ibara 45 hadi Ibara ya 55 inahusu masharti ya masuala ya ujumla kama vile makosa ya kitaaluma na adhabu zake, ukaguzi wa biashara za usambazaji dawa na Famasi, Kinga ya Mashtaka kwa Watekelezaji na sheria inavyopendekezwa.

Sehemu ya Sita yenye Ibara ya 56 hadi Ibara ya 57 inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura ya 219 ambayo inapendekeza kufuta kifungu cha 24, 26, 27, 48, 74 na kifungu cha 21(1)(c) kitarekebishwa ili sehemu inayohusu dawa iingizwe kwenye sheria mpya ya Famasi, kwani vinahusu masuala ya moja kwa moja yanayosimamiwa na taaluma ya Famasi. Pia kifungu cha 21(1)(b) kitarekebishwa ili sehemu inayohusu wanaonunua dawa kutoka kwa watengenezaji na waagizaji wa nje na kuzisambaza madukani ihamishiwe kwenye sheria mpya na kuitwa wasambazaji. Sehemu inayohusu watengenezaji na waagizaji watabaki kuwa chini ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vpodozi sura ya 219 kama biashara ya jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sura ya 219, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu pia kwamba baada ya kupitishwa Sheria hii, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itaandaa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi sura namba 219, marekebisho haya ni yale ambayo pamoja na sababu nyingine yanalenga kuzihusisha sheria hizi mbili, uandaaji huu utaandamana na utayarishaji wa Kanuni na Sheria zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, baada ya kutoa maelezo haya, kwa heshima na taadhima, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wajadili Muswada ulio mbele yetu na kuuridhia, hatimaye kuupitisha na kuwa Sheria ya Famasi ya mwaka 2010 (*The Pharmacy Act, 2010*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii za Bunge au Mwakilishi wake.

MHE. DR. FAUSTINE E. NDUGULILE (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusiana na Muswada wa Famasi wa mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Famasi ya Mwaka 2010, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara ya kwanza katika Bunge la Kumi kwa Kamati hii kutoa maoni Bungeni, natumia nafasi hii kwa niaba ya Kamati kukutakia wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, Katibu wa Bunge na watumishi wote kila la heri katika kutekeleza kazi na majukumu ya Bunge.

Natumia nafasi hii pia kutoa pole kwa Waathirika wa Milipuko ya Mabomu ya Gongo la Mboto na ajali za barabarani ikiwemo iliyohusisha Kikundi cha Taarabu cha *Five Stars*. Tunatoa pole pia kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliofiwa na ndugu na jamaa zao. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze Roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuwashukuru wananchi wa Kigamboni kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, uliipa kazi Kamati hii ya kufikiria, kujadili na kutoa maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Famasi ya Mwaka 2010. Ili kutekeleza jukumu hilo, tarehe 23 Machi, 2011, Kamati ilikutana katika Ofisi Ndogo ya Bunge - Dar es Salaam ambapo Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mheshimiwa Dr. Haji H. Mponda Mbunge, aliwasilisha maelezo ya Serikari kuhusu Muswada wa Sheria ya Famasia ya Mwaka 2010. Waziri, alieleza Kamati kuhusu chimbuko, shabaha, madhumuni na maudhui ya Muswada huu kuwa Muswada wa Sheria ya Famasi unakusudia kuweka masharti ya kudhibiti na kusimamia taaluma na maadili ya Wafamasia katika utoaji wa huduma zinazohusu taaluma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri aliendelea kueleza kuwa Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi sura

219 ili kuhamisha masharti yanayohusiana na taaluma ya Famasi ambayo chini ya Sheria hiyo yalikuwa yakisimamiwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa-TFDA na kuyaweka chini ya usimamizi wa Baraza la Famasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) na 114(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwaalika na kukutana na wadau mbalimbali waliohuduria kwenye kikao na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu. Wadau waliohuduria ni SIKIKA, *Legal and Human Rights Centre (LHRC)*, Chama cha Wafamasia Tanzania (*PST*), Chama cha Fundi Dawa Sanifu (*TAPHATA*), Vyuo vinavyofundisha Famasi (Muhibili na Hospitali ya Agakhani), Viwanda vya Kutengeneza Dawa, Baraza la Wafamasia, Baraza la Dawa za Mifugo, Hospitali za Rufaa (Dodoma), Hospitali Binafsi (Massana) na Asasi ya Famasi za Jamii na watu wengine binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kuwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii yalieleweka vema na vilevile maoni ya wadau yalisaidia Kamati kupendekeza mambo mbalimbali ya kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono hatua ya Serikali ya kuleta Muswada huu kwa lengo la kuwa na Baraza la Famasi ambalo litakuwa na jukumu la kusimamia taaluma na maadili ya wanataluma katika fani ya Famasia, kusimamia viwango vya ubora wa huduma za Famasia katika Taasisi za umma na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini changamoto iliyopo kwenye sehemu ya IV, Kifungu cha 37 (1) (b) cha Muswada kinachoipa Baraza la Famasi uwezo wa kutoa vibali (*permits*) vya Jumla (*wholesale*) vinavyohusisha uingizaji na utengenezaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba nchini, jukumu ambalo ni la Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi (*TFDA*) inayosimamia udhibiti wa ubora na usalama wa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano ya kina, Kamati iliishauri Serikali kuondoa kifungu hicho, jambo ambalo Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alikubaliana na Kamati na kuahidi kukifanyia kazi kifungu hicho kiondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 8 Aprili, 2011 Kamati ilikutana Dodoma na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ili kupata mrejesho wa ushauri uliotolewa na Kamati. Waziri alieleza Kamati kwamba Serikali imependekeza kwamba Kifungu hiki kinaweza kuendelea kujadiliwa na kurekebishwa katika utaratibu maalum hata baada ya Muswada huu kuwa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Waziri, Kamati iliendelea kushauri kwamba kifungu cha 37(1) (b) kiangaliwe upya ili jukumu la utoaji leseni za uingizaji wa jumla na utengenezaji wa dawa nchini libaki kuwa la mamlaka inayosimamia ubora na usalama wa chakula, dawa na vipodozi (*TFDA*). Kwa marekebisho hayo Baraza la Famasi litakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuendelea kusimamia Taaluma ya famasia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza kwamba Serikali ndiyo yenyeye jukumu la msingi la kudhibiti chanzo cha dawa, yaani kule zinakotoka (*source*) na ndiyo kazi ya *Regulatory Authority* ya kudhibiti bidhaa zinazoingia na zinazotengenezwa nchini kabla hazijasambazwa. *TFDA* ndio yenyeye jukumu la kudhibiti ubora na usalama wa chakula, dawa na vipondozi. Iwapo *TFDA* haitekelezi majukumu yake ipasavyo au itakwenda kinyume na maadili, Serikali inaweza kuichukulia Mamlaka hii hatua za kurekebisha na kuiwekea miiko ya kiutendaji. Hata hivyo, Kamati iliona kwamba siyo vema kutenganisha utoaji wa vibali na Mamlaka inayodhibiti ubora na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo, Kamati ilikichunguza Kifungu chote cha 37 cha Muswada, kinachokipa Baraza jukumu la kutoa vibali vya biashara ya rejareja, jumla, ya Taasisi za Famasi na ya aina yote itakayoridhiwa na Baraza la Famasi. Kamati ilibaini kwamba bado kuna umuhimu wa kuangalia upya utoaji wa vibali hivi ili kutenganisha majukumu ya msingi ya Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi na Baraza la Famasi ili kuondoa mwingiliano wa majukumu. Kamati inashauri Serikali kulifanyia kazi eneo hilo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kuwa kupitishwa kwa Muswada huu kuwa sheria kutaweka misingi sahihi ya matumizi endelevu ya taaluma ya Famasia na pia kutaweka mazingira sahihi ya kulinda afya za wananchi wanaohudumiwa na wafamasia kwenye Vituo vya Afya na sehemu nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuchambua kwa kina Maudhui ya Muswada huu, Kamati pia ilipitia kifungu kwa kifungu kwa kuhusisha michango ya wadau na hivyo inashauri Serikali kurekebisha maneno na sentensi kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kichwa kirefu cha Muswada (*long title*) Ili kuzingatia maana na madhumuni kama ilivyokusudiwa neno “*powers*” libadilishwe kwa kuweka neno “*profession*” na hivyo kusomeka kama ifuatavyo:-

“An act to establish the Pharmacy Council and to provide for the functions, management of the Council; to provide for regulation and control of the pharmacy profession and practice and for other related matters”.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ya Muswada katika tafsiri ya neno *pharmacy*, neno ‘*or*’ limetumika, jambo linalosababisha Sheria inayopendekezwa kuzingatia moja kati ya Watengenezaji na Wasambazaji badala ya kuwataja wote. Kamati inashauri kuwa neno ‘*or*’ libadilishwe na kuwa ‘*and*’ na hivyo kusomeka ‘*manufacturing pharmacy and wholesale pharmacy*.’

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya Muswada, katika kifungu cha 3(2) muundo wa sentensi iliyotumika unapaswa kuboreshwa ili kuwa na maana nzuri zaidi. Kamati inashauri kuwa liingizwe neno ‘*a*’ kati ya neno ‘*be*’ na ‘*body*, ’ hivyo kusomeka ‘*the council shall be a body corporate and shall..*’

Katika kifungu cha 5(b) Kamati ina maoni kuwa majukumu yanayoweza kukasimiwa na Baraza la Famasi hayabainishwi katika Sheria inayopendekezwa. Ili kuweka wazi mamlaka halisi ya Baraza yanayoweza kukasimiwa, kifungu hicho kiandikwe vema. Kuhusu uwezo wa Baraza kudhibiti kwa ufanisi taaluma na maadili ya Wafamasia, Kamati inashauri kwamba Kifungu cha 5(c) kitoe uwezo kwa Baraza kupeleka mtuhumiwa Mahakamani (kumshitaki mtuhumiwa).

Kwa upande wa Kifungu 6(1) kinachohusu Kamati ya Famasi, ni maoni yetu kuwa ni vema ziwepo Kamati mbalimbali za Baraza ikiwemo Kamati ya kuidhinisha vibali vya rejareja tu, Kamati vya ya Elimu na Mafunzo, Maadili, na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ya Muswada, Kamati ina ushauri kuhusu Kifungu 16, ambapo neno “*pharmaceutical*” liondolewe na kuweka neno “*pharmacy*”. Kifungu 17(i) kufuta sentensi “*such a period of time as be determined by the council*”, na kuweka sentensi “*for a period of one year up to two years*”. Ili kutoa muda kamili wa mafunzo kwa vitendo. Kifungu 22(3) kuongeza neno “*remove*” kati ya neno “*may*” na “*from*” na hivyo kusomeka “*the council may remove from the relevant....*”

Kifungu 31(2) Kipengele hiki kiandikwe upya (*recasted*) kutoa maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya IV ya Muswada, kifungu 3(c) Kamati inashauri kufuta neno “*determine*” na kuweka neno “*approve*” na hivyo kusomeka “*have powers to approve the location....*” Kifungu 36(2) neno *Council* libadilishwe na kuwa *Minister* na hivyo kusomeka: “*such fee as the Minister may prescribe.*” Kifungu 37(1) (b) neno “*wholesale*” lifutwe kutoa nafasi kwa utaratibu huu kufanya na Taasisi Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA). Kifungu 39 (3)a kufuta maneno “*veterinary,surgeon*” kila lilipoandikwa kwenye Muswada na kuweka neno “*veterinarian*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano ya Muswada, kifungu cha (6) na (7) kibadilishwe na kuwa kifungu cha (5) na (6) kwa kuzingatia upangaji wa namba. Kuingiza kifungu 46 na 47 vinavyofafanua Mamlaka ya kutangaza dawa na vifaa tiba. Hivyo, baada ya kuingiza kifungu 46 na 47, kifungu 46 kilichokuwepo kinabadilika kuwa 48 na kuendelea mpaka kumalizia na kifungu 59 baada ya marekebisho.

Kifungu 50 baada ya marekebisho, kutakuwa na nyongeza ya kifungu kidogo(3) kitakachosomeka, “*The council may appoint a senior pharmaceutical...*”

Katika kifungu 55, baada ya marekebisho (a) maneno “.... *In section 15, 16, 23 or 28 may be conducted*”, yatabadilika na kuwa “.....*in section 16, 24 or 28 may be conducted*” Kifungu 55 (l) neno “*registration*” litawekwa katikati ya neno *required for* na *enrolment* na hivyo kusomeka: “*the training, education or other qualifications required for registration, enrolment or enlistment of pharmacists, pharmaceutical technicians or pharmaceutical assistants.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita ya Muswada, Kifungu 59 baada ya marekebisho, baada ya neno “*repealing section*” litaingizwa neno “21 (i) (b) na (c)”, na hivyo kusomeka: “*The principal Act is amended by repealing section 21(1) (b) na (c), 24, 26, 27 and 28.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipengele cha *Schedule*, kifungu cha (3) kinachoelezea *tenure of office*, kifungu kidogo (2) kifutwe na hivyo kufanya kifungu kilichokuwa Na. 3 kuwa Na. 2 na kuendelea. Kifungu 3(3) maneno: “*the Chairman and Vice Chairman*” yafutwe ili kuondoa kurudia maneno (*repetition*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kupitia na kufikiria Muswada huu inatoa maoni ya jumla kwa Serikali katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kifungu cha 37(1)(b) katika Sura ya Nne ya Muswada kiangaliwe upya na kwa undani zaidi. Vile vile kifungu kizima cha 37 kifanyiwe kazi tena ili kubainisha vizuri majukumu ya *TFDA* na Baraza la Famasi. Aidha, Sheria zinazounda Taasisi hizi, yaani Sheria Na.1 ya Chakula, Dawa na Vipondozi ya Mwaka 2003 inayounda *TFDA* na Sheria Mpya ya Baraza la Famasi ziangaliwe upya kwa pamoja ili kuweka mipaka ya majukumu na mamlaka ya Taasisi hizi.

(b) Uingizaji na utengenezaji wa jumla wa dawa, vifaa na vifaa tiba nchini usimamiwe na Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) badala ya Baraza la Famasi. Hatua hii itawezesha kudhibiti ubora wa huduma hii na hivyo kumhakikishia usalama mwananchi ambaye ndiye mlengwa. Aidha, *TFDA* iimarishwe kwa kuongezewa uwezo na kupatiwa vitendea kazi bora vinavyokidhi mahitaji ya teknolojia ili iweze pia kukabiliana na dawa zinazoingia nchini kwa njia zisizo halali.

(c) Serikali ione umuhimu wa kuongeza idadi ya wajumbe wa Baraza la Famasi kwa kuzingatia uwakilishi kutoka kada zinazohusika na majukumu ya Baraza hili. Vigezo maalumu vitumike katika kupata wajumbe wa Baraza la Famasi. Aidha, katika kuunda Kamati mbalimbali za Baraza la Famasi, pamoja na nyingine ziwemo zinazolenga elimu, mafunzo na maadili.

(d) Serikali iweke utaratibu utakaowezesha kuanzisha na kuendeleza ushirikiano kati ya Baraza la Famasi na Baraza la Vetenari Tanzania ili kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi zao.

(e) Serikali iweke utaratibu wa wazi wa kudhibiti ubora wa dawa za mifugo za jumla na za rejareja.

(f) Kuwepo na utaratibu madhubuti na wa kudumu wa kukagua maduka ya dawa muhimu (*ADDO*) ili kubaini maduka yasiyokidhi viwango vya kutunzia dawa, halikadhalika dawa zilizokwisha muda wa kutumika, vifaa vilivyo chini ya kiwango, leseni bandia na wataalamu wa Famasi waliochini ya viwango.

(g) Serikali ifanye juhudini za makusudi za kuainisha utaratibu mzima wa upatikanaji wa dawa muhimu katika Hospitali zote. Maduka ya dawa ambayo kutokana na utaratibu wa kuwa na madaraja ya maduka ya dawa, baadhi ya dawa moto imekuwa jambo la kawaida kupatikana katika maduka ya dawa muhimu na kuuzwa kwa kificho jambo ambalo ni hatari sana kwa usalama wa dawa na watumiaji ikizingatiwa kuwa dawa ni sumu. Hivyo utaratibu ulionzishwa chini ya mpango wa *ADDO* ufanyiwe tathmini ili kama una manufaa utekelezwe nchini kote.

(h) Kwa vile Baraza la Famasi litakuwa na jukumu la kuangalia mitaala ya aina ya mafunzo katika fani hiyo, Kamati inashauri itazamwe upya ni Kada ipi itahusishwa kuuza dawa katika maduka ya dawa muhimu *ADDO*.

(i) Serikali itekeleze kwa vitendo azma ya kuimarisha huduma ya afya katika ngazi ya Kata, kwani Sekta ya Afya katika ngazi hii ina changamoto nyingi zikiwemo za ukosefu wa wafanyakazi na dawa.

(j) Serikali iweke utaratibu maalumu wa kupokea na kufanya kazi maoni ya watumiaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba nchini ili kuboresha utoaji huduma husika.

(k) Serikali iendelee kuimarisha udhibiti wa uingizaji nchini wa dawa kutoka nje ya nchi zikiwemo zile zinazosababisha watumiaji kubadilisha rangi ya ngozi na kuongeza ukubwa wa maumbile yao.

(l) Serikali iandae utaratibu maalumu wa kutafiti, kutambua na kudhibiti utumiaji wa dawa asili ili kusimamia viwango vya ubora wa dawa asili. Halikadhalika, wataalamu wa dawa hizi waweze kutambulika, shughuli wanazofanya na maeneo ya kazi zao.

(m) Kwa ajili ya kuweka mazingira sahihi ya kutekeleza Sheria hii, Serikali ikamilishe maandalizi ya Kanuni mapema ili kurahisisha utendaji kazi kwa kuondoa mianya ya kutowajibika. Kwa mfano, suala la matumizi ya vibali vya Famasi, ni vyema kanuni ifafanue ukomo wa matumizi ya vibali husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni ya Kamati. Napenda kumshukuru pia Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mheshimiwa Dr. Haji Mponda, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Katibu Mkuu - Ndugu Blandina S. J. Nyoni pamoja na wataalam wa Wizara hiyo kwa ushirikiano wakati Kamati ikijadili Muswada huu wa Sheria ya Famasi ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru na kuwapongeza wadau waliofika mbele ya Kamati kwani michango yao imeisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa walioutoa katika kufanikisha kazi hii. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Naomba nimirambua Mwenyekiti wa Kamati yetu Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Mheshimiwa Dr. Faustine E. Ndugulile - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Maua A. Daftari, Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera, Mheshimiwa Saidi R. Bwanamdogo, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mbunge, Mheshimiwa Dr. Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Lameck O. Airo, Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mheshimiwa Ali J. Haji, Mheshimiwa Annamarystella J. Mallac, Mheshimiwa Martha J. Mlata, Mheshimiwa Dr. Seif S. Rashidi, Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mheshimiwa Mch. Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Clara D. Mwatuka, Mheshimiwa Dr. Hamisi A. Kigwangala, Mheshimiwa Nyambari C. Nyangwine, Mheshimiwa Rashidi A. Omari, Mheshimiwa Said S. Suleimani, Mheshimiwa Stephan H. Ngonyani, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba, Mheshimiwa Faki H. Makame na Mheshimiwa Highness S. Kiwia. (*Makofī*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dr. Thomas D. Kashililah, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Stella Mlambo na Ndugu Happiness Ndalu, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge hili likubali kuridhia hoja hii ya Serikali kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofī*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Faustine E. Ndugulile kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii kwa kutusomea maoni ya Kamati hiyo kuhusiana na Muswada ulio mbele yetu wa Sheria ya Famasi wa Mwaka 2010. Sasa namwomba Msemaji wa Upinzani kwa Kambi ya Upinzani.

MHE. PAULINE P. GEKUL - MSEMADI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Famasi wa mwaka 2010, kwa mujibu wa kanuni za Bunge, kanuni ya 53(6)(c) Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa na kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani nikiwa kama Mwakilishi wa Msemaji Mkuu wa Wizara hii, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kusimama hapa leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Freeman Mboge - Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa imani yake kubwa kwangu kwa kunitua kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Famasia kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Wizara hii. Pia nakishukuru Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo kwa kunipa fursa ya kuwa Mbunge kwa tiketi yake. Namshukuru Kiongozi wa Upinzani na Naibu wake Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto

kwa uongozi wao thabiti wa Kambi yetu na miongozo mbalimbali wanayoitoa kwa Mawaziri Vivuli. (*Makofi*)

Sambamba na hilo, niwashukuru na kuwapongeza wanachama, wapenzi wote wa CHADEMA pamoja na wananchi wa Jimbo la Babati Mjini kwa imani yao kwangu na hivyo kunipa kura nyingi sana katika uchaguzi uliomalizika mwezi Oktoba mwaka 2010. Japo hazikutosha, lakini zimeniwezesha kufika hapa nilipo leo. Nawashukuruni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa pongezi za pekee ni kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa ushirikiano na umakini wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijatenda haki kama nitashindwa kuwashukuru watumishi wote walioko katika Sekta ya Afya, kwa kufanya kazi nzuri japokuwa mazingira yao ya kazi ni magumu sana kulinganisha na hali halisi ya huduma wanayoitoa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kuangalia baadhi ya mambo yaliyomo katika Muswada huu. Kwa ujumla, madhumuni ya Muswada huu ni mazuri, na yanatoa dhana nzima ya mgawanyo wa kazi na majukumu, jambo ambalo linakidhi na kuleta uwajibikaji katika tasnia nzima ya madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Muswada huu unahusu ufamasia, lakini katika Muswada haikutolewa tafsiri ya nani ni mfamasia. Badala yake wameeleza vigezo anavyotakiwa kuwanavyo huyo mtu anayeitwa mfamasia. Kambi ya Upinzani inaona kuwa tafsiri ya neno: “*Pharmacist*” kama “*health professional trained to the level of University degree in the art and or science of preparing and dispensing medicines*” liwekwe katika Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la jumla kuhusu nia ya Muswada, Muswada unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Famasi ya mwaka 2010, sasa ya mwaka 2011 kwa lengo mahususi la kuweka Masharti ya kudhibiti na kusimamia taaluma ya Wafamasia katika utoaji wa huduma zinazohusu taaluma hiyo. Ukisoma Muswada kwenye Madhumuni kwa Kiingereza, Muswada wenyewe ni wa lugha hiyo utaona yanatumika maneno ‘*to regulate the pharmacy profession in different levels*’ ambapo tafsiri yake siyo sawa na madhumuni kwa lugha ya Kiswahili kwamba ‘katika utoaji huduma zinazohusu taaluma hiyo’. Muswada huu unataka kuweka utaratibu wa kusimamia taaluma na biashara ya Famasi. Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya kina kabisa, ni kwa nini Chombo cha kitaaluma pia kiwe chombo cha kusimamia biashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la Muswada huu ni jambo la muhimu sana kufafanuliwa na Serikali kabla Bunge halijaamua kuupitisha Muswada huu. Muswada unafuta vifungu kadhaa vyta Sheria ya Madawa na Chakula Sura ya 219 na kuufanya pia

Muswada usomwe pamoja na Sheria hiyo kama ‘*The Principal Act*’. Vifungu vinavyofutwa ni namba 24, 26, 27, 47 na 74.

Vifungu hivi vyote vinahusu usimamizi wa biashara ya Famasi na wala siyo taaluma ya Famasi. Inawezekanaje Baraza la Wafamasia likadhibiti taaluma na wakati huo huo kusimamia biashara? Kwa nini Sheria inayopendekezwa isiwe sawa na vyombo vya kitaaluma kama Bodi ya Wahandisi, Bodi ya Wakandarasi au hata Baraza la Wauguzi? Ni kwa nini kazi ya kudhibiti na kusimamia biashara isibakie kwa *TDFA*? Kuna mapungufu gani yametokea katika utekelezaji wa Sheria ya *TFDA*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 4(d)(i) cha Muswada katika kazi za Baraza kinaonyesha kuwa Baraza liweke na kuendeleza pia kusimamia viwango kwenye mafunzo ya ufamasia na mfumo mzima wa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kifungu hiki kinaweza kuingilia sekta nyine ya Elimu ya Juu ambayo ndiyo yenyeye jukumu la kutoa elimu katika tasnia nzima ya ufamasia. Hivyo basi, tunaomba kuambiwa kama baraza ndilo litakuwa na jukumu la kutunga mitaala katika tasnia nzima ya ufamasia. Ukiangalia Sheria ya *Nurses and Midwives Registration* ya mwaka 1997 utaona kwamba Baraza ndio linatunga mitaala na hata mitihani ya wanataluma ya uuguzi. Kama Serikali ilikuwa na lengo hili na Kambi ya Upinzani haioni ubaya ni vema liwekwe wazi kwenye Sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 8(1) cha Muswada kinatoa nafasi kwa Baraza kuunda Kamati nyinezeo ndogo za kufanya kazi kwa niaba ya Baraza. Kambi ya Upinzani ingependa kujua hizo Kamati zinapewa madaraka kiasi gani na ukomo wake ni upi? Kamati hizo zitakuwa na idadi gani ya Wajumbe na wenye sifa zipi? Hii ni pamoja na muda wao wa kukutana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 10(4)(e) cha Muswada kinaonyesha jinsi gani taarifa ya mapato na matumizi ya Baraza yatakavyotunzwa na kutolewa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashauri Baraza kuwa na watalamu wallobobe katika masuala ya fedha na pia taarifa hizo zichapishwe katika gazeti la Serikali ili ifahamike kwa uwazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 10(5) cha Muswada kinachosema kuwa pale Waziri atakapobaini kuwa Baraza halitekelezi majukumu yake ya msingi atatoa maelekezo kwa kuliandikia barua ili kuhakikisha linatekeleza majukumu yake kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona hapa kuna matatizo na huu umekuwa ndio ugonjwa wetu kama nchi. Kama watu wanashindwa kutekeleza majukumu yao ya msingi ni kwa nini wasiwajibishwe? Kweli kuna haja ya kukumbushwa kufanya kazi yao katika mazingira ya sasa ambayo ushindani ni katika kila

sekta. Hivyo basi, tunaomba dhana nzima ya kifungu hicho iangaliwe upya ili iendane na dhana ya uwajibikaji kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 13(1) na (2) Muswada unataja Wajumbe wa Sekretarieti ya Baraza. Aidha, Msajili na Msaidizi wake wanatajwa bayana na kifungu hiki, na pia wanapendekezwa Wajumbe ambao Baraza litaona kama inafaa na wawe waajiriwa wa Serikali kwa ufanisi wa Baraza kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kujua ni idadi gani ya Wajumbe wanahitajika na je, inazingatia jinsia? Kwani idadi hii inaweza kuwa kubwa na isiwe ya manufaa kwa Baraza. Kambi ya Upinzani inashauri Sekretarieti hii iwe na Wajumbe wachache ambao watafanya kazi kwa ufanisi mkubwa na pia sifa zao zifafanuliwe na kueleweka bayana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 14(1) kinachosema kuwa Baraza litaendesa au kufanyisha mitihani ya kitaaluma katika usajili na uandikishaji kwa watahiniwa wote wa ufamasia katika madaraja mbalimbali. Aidha, kifungu cha 14(2) kinasema kuwa ikiwa mtu atatumma maombi ya usajili ya ufamasia kwa ngazi mbalimbali anatakiwa kulipa ada ambazo zinatakiwa kabla ya kusajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hoja ni kwamba kama Baraza linafanyisha watu mitihani ya kitaaluma katika kadha nzima ya usajili, wakati watu hao tayari wamekwishahitim u kwenye Vyuo vinavyotambulika katika kutoa mafunzo hayo: Je, kuna haja ya kujiandikisha mara ya pili kwa kutoa ada? Kambi inaomba ufanuzi kuhusiana na kifungu hicho cha 14 (1)na(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 17 cha Muswada kinaeleza kuwa Baraza halitamtambua mfamasia kama hajafanya “*internship*” kwa muda uliopangwa na Baraza.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani inapenda kujua kipindi hicho ni cha muda gani, na kama kikiongezwa na Baraza kadiri itakavyohitajika ni kwa muda gani? Aidha, suala la ada ambayo hulipwa wakati wa kuanza “*internship*” huwa ni kwa mujibu wa kanuni ipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 33(1) kinachosema kuwa pamoja na usajili, tangazo kwenye Gazeti la Serikali linatosha kutoa ushahidi kuwa mtu amesajiliwa au amefutwa pale jina lake linapokosekana katika gazeti hilo; Kambi ya Upinzani inaona kuwa usitishwaji wa usajili unapofanywa ni bora mhusika apatiwe taarifa rasmi, sababu za usitishwaji huo na huo ndio uungwana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ya Muswada inayohusiana na usajili wa maduka au sehemu za biashara na utoaji wa vibali kwa biashara ya madawa, kwa ujumla Kambi ya Upinzani inaiona sehemu hii kuwa inakwenda kinyume na dhumuni kuu la kufuta sheria ya zamani ya mwaka 2002 na kuanzishwa kwa Muswada huu. Kimsingi kuna haja gani kwa Baraza la Kitaaluma kusimamia (*regulator*) Biashara? Hili ndilo tatizo la kimsingi (*fundamental*) ambalo Kambi ya upinzani inahoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa madhumuni ya kutungwa upya kwa Muswada huu wa Sheria hii ni kuwa Baraza la Mafamasia liendelee kusimamia, kulinda na kudhibiti maadili ya taaluma ya ufamasia kwa wale wafamasia wote wanaofanya biashara ya madawa na katika masuala mengine yanayohusiana na madawa kwa tafisiri pana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana nyingine ni kwamba Baraza hili ndilo litakalokuwa msimamizi mkuu kwa wanataluma na hivyo linaweza kutoa adhabu kwa wafamasia wote wanaojihusisha na biashara ya madawa kama watakuwa wamekwenda kinyume na maadili ya taaluma hiyo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yanayohusu maeneo ya utoaji wa huduma, uzalishaji na biashara ya madawa yabakie kuwa ni jukumu la Mamlaka ya Udhibiti (*regulatory authority*) ambaye ni Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kuwa Baraza ndilo lenye uwezo wa kuhakikisha kuwa Watendaji walio katika tasnia ya madawa wanafuata maadili (*code of ethics or conducts*). Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) wao wanatakiwa kuelewa jinsi gani biashara ya madawa inafanyika na siyo vinginevyo. Aidha, tukumbuke kwamba kibali cha biashara ya madawa kinatolewa kwa mfamasia aliyesajiliwa na anatambuliwa na Baraza na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina mashaka makubwa sana na Muswada huu. Ni dhahiri huu Muswada haujafanyiwa tafakuri ya kutosha na ni kama unataka kuridhisha kikundi kimoja katika jamii. Kitendo cha kuweka Baraza moja kusimamia taaluma na Biashara ni kitendo ambacho kitakuwa na madhara makubwa sana hapo siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Muswada huu urejeshwe kwenye Kamati ili ufaniyiwe mabadiliko muhimu ya kuondoa vipengele vyote vinavyohusu usimamizi wa Biashara ya Famasi ili kutengeshanisha Biashara na Taaluma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Baada ya kuyasema hayo, nakushukuru sana, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Paulina Gekul Mbunge wa CHADEMA kutoka Mkoa wa Manyara ambaye amesoma maoni haya kwa niaba ya Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, sasa niwaambie tu ambao mnajua tunatunga sheria na ziko taratibu za utungaji wa Sheria, kwa hiyo, wale ambao wanajisikia kwa uzito wakati ule wa kufika kwenye kipindi cha kifungu kwa kifungu kwamba wana mambo ambayo wangependa yakae wanavyodhani yawe, basi ni vizuri wakawaona vijana wetu wa Idara ya Sheria ya Bunge kwa ajili ya kuwekana sawa mapema.

Sasa wachangiaji ni wengi kidogo, lakini tutaanza uchangiaji wetu, tutachukua kiasi ambacho kitaturuhusu na jioni tutaendelea. Matarajio yetu ni kwamba jioni tutamaliza suala zima linalohusiana na sheria hii. Katika wachangiaji, naomba na Mheshimiwa Dr. Augustino L. Mrema atafuatiwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kutoa shukrani na pongezi kwa Serikali kwa kuleta Muswada huu. Naona Muswada ni muhimu ni Muswada wa kutunga Sheria Mpya ya Famasia ya mwaka 2010. Najaribu kuangalia Muswada nikaona kwamba lengo kubwa ni kuboresha huduma za famasia mjini. Huko nyuma hizi huduma zilikuwa zinatolewa kienyeji au kiholela. Sasa nafikiri kama Wabunge kwa busara zao watakubali kupitisha Muswada huu, nina hakika huduma hizi zitakuwa zinatolewa kwa ufanisi na zitakuwa zinawasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuangalia huu Muswada, majukumu yameainishwa vizuri, nimeona kazi kubwa ya kwanza ya Baraza la Famasia itakuwa ni kusimamia watalaam wa kazi hiyo na kusimamia utendaji wao wa kazi wa kila siku. Kwa hiyo, Baraza hili litasaidia sana kusimamia kudhibiti Watendaji huko amba wamekuwa na matatizo. Huko nyuma kumekuwa na watalaam feki amba walikuwa hawaeleweki vizuri. Kwa hiyo, litadhibiti watalaam pia wanaojifanya wamesoma, watalaam bandia. Kwa hiyo, Baraza hili litasaidia kupata watalaam amba wana uzoefu na kazi yao. Kwa hiyo, ni maoni yangu kwamba Baraza la Famasia litaboresha huduma zitolewazo katika maduka ya dawa mjini. Litasaidia sana Famasi za jumla, litasaidia sana Famasi za Rejereja, maduka muhimu yanayohitaji kusimamiwa kwa mujibu wa utalaam unaotakiwa.

Pili, nimeona kwamba Muswada huu utaleta uwiano au *check and balances*. Kwanza kati ya majukumu ya *TFDA*, *TFDA* ndio Mamlaka ya Chakula na Dawa. Kwa hiyo, watahakikisha ubora na kusajili madawa.

Tatu, Baraza la Famasi watasimamia utendaji na uuzaaji wa madawa kwa kuzingatia kanuni za kifamasia. Kwa hiyo, sheria hii itaondoa baadhi ya vifungu kutoka *TFDA*, utaipa Mamlaka ya *TFDA* kushughulikia masuala ya ubora kikamilifu na pia utasaidia sana kuonyesha madawa bandia ambayo yamezagaa karibu kila mahali mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuwaomba Waheshimiwa Wabunge ni kwamba madawa ni sumu, madawa yanaua, kwa hiyo, lazima yasimamiwe na kanuni za kitaalum. Naomba Waheshimiwa Wabunge, wajue kwamba hizi dawa siyo biashara tu, ni zaidi ya biashara. Hizi ni huduma kwa maisha ya watu, kwa uhai wa watu, lazima zisimamiwe kitalaam ili kulinda afya za wananchi kulinda afya za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi baada hayo.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Augustino L. Mrema kama nilivyokwishesema utafuatiwa na Mheshimiwa Kabwe Zubeir.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Muswada huu. Kwanza nafahamu wewe na Spika aliyejita ni mionganoni mwa Wajumbe kutoka Chama cha Mapinduzi ambao mmepitishwa kugombea Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama chenu. Nilikuwa naomba watu wote wa CCM ambao tunaheshimiana wawape kura ili muweze kuingia kwenye kikao muhimu hicho cha chama chenu. (*Makofi*)

Lakini pili, nimpongeze sana Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa kusoma maoni ya Kambi kwa ufasaha kabisa. Naamini kabisa kwamba tunao Mawaziri Vivuli ambao wataweza kuisimamia Serikali ya CCM vizuri kabisa na kuweza kutoa huduma kwa wananchi. (*Makofi*)

Tatu, niwapongeze Serikali kwa kuja na huu Muswada, nafahamu kwamba ni Muswada ambao umechelewa muda mrefu sana, ilikuwa tuupitishe toka Bunge la Tisa, haikuwezekana na sasa umefanikiwa kupita kwenye hatua za Kamati na kuja kwenye Bunge hili la Kumi.

Lakini vile vile katika kazi yetu kama Bunge, kazi ya kutunga Sheria, Muswada huu umeingia kwenye rekodi kuwa ndio Muswada wa kwanza wa Bunge la Kumi kuweza kujadiliwa kwenye Bunge. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hiyo rekodi iweze kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina tatizo moja kubwa sana katika huu Muswada. Kwanza unapopata Muswada unaangalia madhumuni na sababu, Waziri Kivuli ameeleza hili vizuri sana. Ukitosha ukurasa wa 34 wa Muswada *Objects and Reasons, the proposed law is intended to regulate the pharmacy profession in different levels*. Ukienda kusoma kwa Kiswahili pamoja na kuongezeka kwa maneno na kuwa mapana zaidi, lakini pia bado ni kusimamia taaluma na maadili ya wafamasia katika utoaji wa huduma zinazohusu taaluma hiyo.

Sasa tunafahamu kwamba kuna *market entry regulations*, ni usimamizi unaohusiana na kuingia kwenye soko, ndio usimamizi wa *profession*. Lakini kuna *market conduct regulation* ambao ni usimamizi wa biashara. Sasa *market conduct regulation* imekuwa ikifanya TFDA siku zote za nyuma. Muswada huu unataka kuunganisha kwa pamoja kwamba Baraza la Wafamasia lishughulikie *market entry regulation* iwe *regulator* kwa wafamasia wanaoingia kwenye ufamasia wakishatoka kwenye vyuo kuwasimamia taaluma yao.

Wakati huo huo, wasimamie *Market Conduct Regulation*. Baraza hilo hilo sidhani kama *principle* inakwenda vizuri hapa. Nadhani ni vizuri, na tuna mifano. Nyuma huko na Waziri Kivuli amezungumza *contractor Legislation Board, Engineers Legislation Boards, Nurses and Midwives Regulation Act* ya mwaka 1997 zote zimetofautisha. Nadhani ni vizuri Mamlaka ya *Council* ya Wafamasia ikabakia kwenye kusimamia taaluma ya ufamasia. Isiingie kwenye kusimamia biashara ya ufamasia. Hii itasaidia sana nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ni kwamba sasa hivi Tanzania tuna Wafamasia 700 tu kila mfamasia mmoja anahudumia wananchi 50,000 wenzetu kwa nchi za kiafrika kama Ghana mfamasia mmoja anahudumia watu 10,000, wenzetu Kenya wako juu kidogo wao wana wafamasia wengi kidogo, lakini hatupishani sana ndani ya eneo la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa la wale *ma-technician* wa ufamasia tunao 300 tu. Bahati mbaya sana katikati ya miaka ya 1990 Taifa letu haliwfundishi tena *pharmacist technicians* hatuna. Hizi ni taarifa za Serikali, Taarifa ya Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha ilifanya tathmini ambao ilikuwa *funded* na WHO na European Union mwaka jana Septemba, walitoa hiyo taarifa na kuonyesha tatizo kubwa tulilonalo katika taaluma hii ya ufamasia. Kwa maana hiyo, ni kwamba tuna haja zaidi ya kuimarishe taaluma kuliko kwenda kusimamia biashara. Kwa hiyo, Muswada huu ungebakia kusimamia taaluma ya ufamasia na kuimarishe na kuweza kutatua tatizo kubwa sana la *human resources* katika taaluma hii ya ufamasia. Kwa hiyo, hili ndilo ambalo nilikuwa naomba liweze kuangaliwa. Muswada ubakie na madhumuni ya ku-regulate taaluma usiende kwenye ku-regulate biashara. (*Makofi*)

Lakini hata kama Bunge likikubali kwamba tukapisha Muswada kama jinsi ambavyo Serikali imeuleta kwa ajili ku-regulate pamoja na biashara ya ufamasia, bado tutakuwa tuna tatizo kwa sababu ukiangalia Muswada ule, Sheria ya Madawa ya Kenya ambayo inaanishi Bodi ya Madawa na Sumu ya Kenya ambapo kwa kiasi kikubwa sheria yetu imeiga kutoka huko, wao hiyo *regulation* pamoja na kwamba wamechanganya kila kitu wameanzia kwenye utengenezaji kwa maana ya *manufacturing* wakaenda kwenye ufamasia na wakaenda kwenye *trading* ya madawa.

Kwa hiyo, wamechukua yote kwa *comprehensive*. Sisi tume - *shell- pick* kwamba utengenezaji, basi tuwaachie TFDA lakini biashara wachukue Baraza. Nadhani hapa kuna tatizo. Ni ama unachukua sekta nzima kuanzia utengenezaji *licensing* mpaka biashara au unafanya kazi ya taaluma tu ya ufamasia na kuiachia biashara ifanywe na TFDA. Tayari tumeshajenga uwezo wa TFDA imeshapata uwezo wa muda mrefu na uzoefu kutoka mwaka 2003 hakuna sababu sasa hivi kuanzia kuichukua na kuipunguza na kuipeleka kwenye kitu kipyä ambacho kinaanza na itakuwa ni *risk*, yaani *actually* tunafanya kitu *opportunistic venture* sasa hivi. Kwa hiyo, maeleo ya Waziri amesema kwamba tutafanya marekebisho baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, hakuna sababu ya kwenda kufanya marekebisho baadaye. Kifungu chote cha nne cha Muswada kiondolewe ambacho kinahusiana na biashara ya ufamasia, Muswada ubakie na kusimamia taaluma ya ufamasia. Hivyo ndivyo ambavyo tutaweza kulitendea wema Taifa letu. Vinginevyo tutaingia kwenye matatizo makubwa sana. Tutakwenda kuanzisha kitu kipyä bila sababu yoyote ya msingi.

Unapotunga sheria, kuna jambo ambalo unataka kulijibu ambalo labda Serikali haijatueleza, labda itufahamishe ili Bunge liweze kufahamu. Kwa sababu unaitunga sheria ili kurekebisha kasoro ambazo zipo hivi sasa. Sasa Serikali ituambie, Wizara ya Afya kuna kasoro zipi ambazo mmeziona kwa TFDA kusimamia biashara ya madawa,

tukielezwa hili na likawa kwa ufanuzi mzuri na Wabunge wakaelewa, basi ndio hapo tunaweza tukaruhusu Muswada huu uweze kwenda. Lakini vinginevyo, kwa namna ambavyo Muswada huu ulivyo sidhani kama tutakuwa tunatendea haki Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo makubwa sana kwenye taaluma hii yarekebishwe, tunaambiwa na Taarifa za Serikali, taarifa ya Wizara ya Fedha kwamba asilimia 51 ya vijana wanaohitimu kwenye ufamasia wanaacha taaluma ya ufamasia wanakwenda benki, wanakwenda wapi asilimia 51.

Sasa ni vyema Baraza likahakikisha kwamba wana-*retain* kwanza tuongeze watu, lijenge uwezo hapo baadaye kama itakuja kuonekana kuna haja ya baadhi ya shughuli ama ni *retail* au *wholesale* au hata *manufacturing* kama zitahitajika ziingie kwenye Baraza tuwe tumeshafanya tathimini ya kutosha, lakini tumeppata wafamasia wa kutosha. Yaani kwa mazingira ya sasa, naungana kabisa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwamba ama kipengele Na. 4 yaani kifungu cha Nne cha Muswada chote kiondolewa au Muswada urudi kwenye Kamati ukafanyiwe kazi upya, kusema kwamba haiwezekani tutakuja kufanya marekebisho baadaye hapa kwa Muswada huu unaondoa kazi yote ya TFDA katika kusimamia biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 31 wa Muswada, ukurasa wa 32 wa Muswada kifungu 24, 26, 27, 47, 48 na 74 vifungu hivi vyote ndio ambavyo vilikuwa vinaipa TFDA ile mamlaka ya kufanya kazi ya kuweza kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nadhani Serikali iangalie upya suala hili, ama iletu *schedule of amendment, section (4)* yote ya Muswada iondolewe kabisa katika Muswada na wafanye *consequential amendment* zote za maeneo ya Muswada tubakie na taaluma au Muswada urudi kwenye Kamati ukafanyiwe kazi upya uletwe hapa kwa ajili ya kushughulikia taaluma kama jinsi ambavyo madhumuni na sababu za Muswada zilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sina hakika kama Dr. Kebwe yumo humu ndani, kama yupo namkaribisha atoe mchango wake.

MHE. DR. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kwa ajili ya kuchangia hoja ya Muswada. Kwanza na-*declare interest* kwa sababu mimi ni Mjumbe katika Kamati. Kwa sababu ya majukumu mengine, kuna sehemu sikushiriki kikamilifu. Naona ni vema tusaidieni katika kushauriana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kidogo ya *profile* ya masuala mazima ya *nature* hata ya kuleta Muswada huu hapa Bungeni. Mwaka 1978 Sheria Na. 9 ambayo ilikuwa ni chini ya *Pharmacy Board* ilivyokuja kuanzisha mamlaka pamoja na Baraza la Famasi kwa ile sheria namba moja ya mwaka 2003 kuanzisha TFDA na sheria Na.7 ya mwaka 2002 kuanzisha *Pharmacy Council*.

Katika masuala mazima ya sura 311 katika sheria ya sasa ya *pharmacy* ni dhahiri kwamba kuna umuhimu wa kutenganisha vyombo hivi viwili ili kusudi sheria ambazo zilitumika kuanzisha vyombo hivi zifanye kazi vizuri, ziwe na *meno* na *harmony* katika utekelezaji. Kwa sababu kikubwa ambacho kinaonekana sasa hivi ni masuala ya kuingiliana majukumu kati ya *TFDA* na *Pharmacy Council*.

Tukijaribu kuangalia, kwa mfano katika suala zima la utekelezaji, unaweza kukuta mfamasia kutoka *TFDA*, anakwenda kufanya usimamizi wa kazi katika eneo fulani. Lakini wakati huo huo *Pharmacy Council* ina takwimu na *database* kuhusu wataalam wake, yaani wafamasia. Utashangaa kuona kwamba sehemu nyingine kuna mfamasia, lakini kwa sababu ya kutafuta hali ya maisha alishaondoka nchini, yuko labda Marekani au yuko sehemu nyingine. Lakini *TFDA* kwa sababu hawana takwimu za undani kuhusu watalaam hawa, akienda kukagua duka, yeze ataonyeshwa cheti kwamba mfamasia anayesimamia famasi hii yuko wapi, aliyekutwa dukani pale atafanya kuonyesha cheti hiki hapa. Lakini mfamasia huyo una hakika kweli yuko nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho hapa kinasikitisha ni pale ambapo bahati mbaya Mfamasia amefariki, lakini cheti bado kiko ukutani cha kuonyesha kwamba huyu ndiye anayesimamia duka hili. Lakini masuala haya yalikuwa chini ya jukumu la *Phamarcy Council* ambao wanafuatilia, wana takwimu zao, hawa Wafamasia Wataalam inakuwa ni rahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la msingi ambalo nalionna ni masuala ya *ADO*. Hapa kidogo tumeachwa njia panda kwa sababu gani tunaambiwa *ADO* kutekelezwaa nchi nzima bado imeachwa kwa *TFDA*. Lakini tukijaribu kuangalia Muswada sehemu ile ya 37 kipengele cha *Kwanza* (a) ni pamoja na uuzaajii wa dawa rejareja (*retail*). Hapa kuna giza, ndiyo sababu Kamati imesisitiza kabisa suala zima la kutazama upya kuanzia Sheria ya *TFDA*, Sheria Na. 1 ya 2003 ili kusudi kupunguza hili giza. Kwa sababu leo hii Muswada huu kwa nia njema kabisa nina hakika utapita lakini kule katika uwanja wa utekelezaji itakuwa tabu. Kwa sababu *TFDA* kwa Sheria iliyopo sasa hivi itamruhusu kukagua maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Muswada huu ukipita na kuwa Sheria na Kanuni zake zikishatoka, utakuta kwamba wanayo majukumu tayari ya kuangalia masuala mazima ya dawa na usimamizi. Hapo tayari kutakuwa na mgongano. Kwa hiyo, ninachokiomba, suala hili la usimamizi lifanyike vizuri mapema iwezekanavyo ili kusudu uundwaji wa Sheria hii ambayo leo imeletwa kama Muswada iweze kupita mapema kuondoa giza hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukijaribu kuangalia kuna suala zima la mafunzo na taaluma ambalo liko katika Muswada na kwamba wataalam hawa wanaouza dawa basi waweze kuwa chini ya Baraza. Lakini kama *TFDA* bado iko na *ADO* na wale wauzaji, wanasomeshwa kwa muda wa wiki nne. Hawa hawako katika *Council*. Hawajapokea, lakini *ADO* na kifungu cha 37(1)(a) ambayo ni uuzaaji wa rejareja iko katika eneo hili. Kwa hiyo, bado ni changamoto ambayo naiona Muswada huu katika

kufanya marekebisho sehemu hiyo ili iendane na kufanya kazi kwa pamoja na kwa suluhu na *TFDA* ifanye marekebisho mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukijaribu kuangalia suala zima la biashara pamoja na taaluma, huwezi ukalitenganisha. Kwa sababu huyu muuzaji yuko katika eneo labda ni *pharmacy* au ni duka la rejareja. Huyu *conduct* yake na uwezo wake hata kitaaluma bila kuwa chini ya Baraza ambalo linahusika, Baraza la *Pharmacy*, *TFDA* kwa utaratibu hawana meno. Wao watafika watamwona kweli yuko pale, ni mtaalam, lakini kama ana-*misconduct* yoyote ile hawa hawana meno mpaka ipelekwe taarifa kule *Pharmacy Council* kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha amegusia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba hili lifanye kazi mapema ili kusudi liweze kuendana na nchi zingine, wenzetu wa Marekani, Afrika Kusini, Ghana wanakwenda kwa utaratibu huo na *experience* imetuonyesha wanakwenda vizuri. Hizi *consequential amendments* ni vizuri ziendane pamoja na suala zima la kuangalia uzoefu ambao tunao nchini, uzoefu baada ya Sheria hizi mbili kuunda vyombo hivi viwili, Baraza pamoja na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi utusaidie kurekebisha haya ambayo yameletwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nashukuru sana. (*Makofi*)

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Muswada wa Sheria wa *Pharmacy* wa Mwaka 2010 au *The Pharmacy Act, 2010*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza wafanyakazi wote katika Sekta ya Afya kwa uvumilivu wao mkubwa wa kufanya kazi katika mazingira magumu na wakati mwingine ni hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwapongeza hasa wafanyakazi wa Sekta hii ya Afya walioko Jimboni kwangu Kwimba, Jimbo ninaloishi pamoja na wale wanaotoka Mikoa ya Mwanza na Geita na Tanzania nzima. Naomba niende moja kwa moja katika kifungu cha 10(v) kinachozungumzia utekelezaji wa majukumu. Endapo majukumu hayo yatatekelezwa kwa kufutilia uwajibikaji na uadilifu hakika Muswada huu utatunufaisha Watanzania wote nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende katika kifungu cha 10(1) kinachozungumzia uteuzi wa Wajumbe wa Sekretarieti ya Baraza. Ni matumaini yangu kwamba uteuzi wa Wajumbe hawa utazingatia uwiano wa kijinsia ukizingatia kwamba zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania ni wanawake na ni matarajio yangu kwamba Baraza hili litakuwa na Wajumbe wanawake wengi kuliko wanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, endapo marekebisho yote yaliyotajwa na wasemaji wa awali na kasoro zote zitarekebishiwa ndani ya Muswada huu. Ni matumaini yangu kwamba Muswada huu utakuwa na manufaa na mimi nitakuwa tayari kuuunga mkono. Naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Leticia Nyerere. Kabla sijamwita Dokta Seif Rashid, niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna *Schedule of Amendment*, kwa hiyo ni vizuri kwa watakaochangia baadaye kuipitia, nayo ni nzito, ina kurasa 11. Daktari Seif Rashidi, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyambari Nyangwine.

MHE. DKT. SEIF S. RASHIDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani za dhati kunipa nafasi. Lakini pili, nichukue nafasi hii vile vile kwa sababu nazungumza kwa mara ya kwanza kuwashukuru Wanajimbo wa Rufiji kwa kunipa nafasi ya kuwa Mbunge wao na mwakilishi wao kwenye chombo hiki muhimu.

Lakini nichukue nafasi hii kueleza kwamba mimi ni mionganoni mwa wanakamati na kwa namna fulani sitarudia kuyazungumza yale ambayo tayari tulishayazungumza kwenye Kamati. Lakini napenda kwa tahadhari zaidi niweze kuyazungumzia kwa maoni yangu kwa ujumla ili tuweze kufanya maamuzi yaliyokuwa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nizungumzie juu ya nafasi mbili za Baraza na kazi za *TFDA*. Ni matumaini yangu kwamba *TFDA* itakuwa na nafasi kubwa zaidi ya kuweza kuangalia ubora, usalama na kuhakikisha kwamba mlaji hatakuwa na matatizo ya kutumia kile kilichokwuwa kimepitishwa na *TFDA* na kwa namna hiyo tunazungumzia uzalishaji na usambazaji wake yaani katika matumizi tunategemea kabisa kwamba Baraza litakuwa na nafasi kubwa zaidi kwa sababu ndiyo chombo cha kitaalam kinachowenza kuzingatia matumizi sahihi lakini vile vile utunzaji na uhakikishaji kwamba utoaji wake unakwenda sambamba na viwango vilivyokuwa salama kwa mtumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hiyo nafasi ya Baraza la Famasia litakuwa na mchango mkubwa zaidi kuhakikisha kwamba siyo tu katika utendaji wake wa kazi wa kutoa dawa au *prescription* lakini vile vile kusimamia biashara yenewe ya dawa. Nije katika tafsiri ya kwamba tuna changamoto kubwa, tunaweza tukasema nini kianze na nini kifuate. Kwa sababu sasa hivi tuna sheria ambayo itakuwa inadhibiti taaluma ya famasia na hivyo hivyo kuhakikisha kwamba wale wanaofanya kazi zinazohusiana na taaluma hii wanapata ridhaa ya Baraza hili.

Lakini mse maji aliyetangulia ameonyesha moja katika changamoto ni idadi ya watalam tuliokwuwa nao. Naamini Wizara ya Afya, Serikali itakuwa na wajibu mkubwa zaidi wa kuweza kufanya kila jitihada zinazowezekana kuhakikisha kwamba idadi ya wanataaluma hii inaongezeka. Lakini katika kuongeza idadi ya wanataaluma nirudie kupendekeza kwa Serikali kwamba kuzuia vile vitu ambavyo tayari vilikwishafanyika kwenye miaka ya 60 na miaka ya 70, kutayarisha taaluma zinazokwenda kwa kuharakisha kwa mafundisho ya muda mfupi na kutoa vyeti na kutoa kada ambazo zenewe baada ya muda fulani vinakuwa na ukuta wa maendeleo. Kwa hakika huyu mtu ambaye anaingia kwenye taaluma hiyo katika kada hiyo ambayo inafundishwa kwa muda mfupi kwa anayoitwa *technician* au anayoitwa *assistant*.

Lakini baada ya huyu mtu kufundishwa na kuingia katika nafasi ya kutoa mchango wake kusaidia Watanzania wenzake anakuwa hana tena mpango wa

kuendelezwa kufika katika fani, katika kada na katika ngazi zinazotakiwa kufuatwa kule juu. Nasema hii ni changamoto na ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba tunapompata Mtanzania ambaye anajitolea kuingia katika mafundisho hayo mafupi basi lazima pawepo na mkakati wa kutosha wa kumwendeleza ili na yeye aweze kunufaika na kazi ambazo atakuwa ametoa kwa kuwasaidia Watanzania wenzake kwa kufanya kazi ambayo inahitaji taaluma ya juu zaidi lakini ametumia muda mfupi kujifunza na akaifanya kazi hiyo. Ni wajibu wake yeye kupata nafasi ya kuendelezwa kufikia katika kada na ngazi ambayo anastahili kuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi katika kuzungumzia juu ya idadi ya wafanyakazi ambao wapo katika vituo vyetu vya tiba, maeneo yote nchini, bado Wizara ya Afya ina changamoto kubwa kwamba zaidi ya asilimia sitini ya mahitaji ya wafanyakazi hayapo. Tunafanyaje hili, sambamba na kwamba idadi ya Watanzania inaongezeka kila mwaka na kwa namna hiyo uzalishaji wetu unahitaji kwenda katika sura mbili. Ya kwanza kuziba pengo la asilimia 60 lakini vile vile kuangalia namna ambavyo inaweza ikaziba pengo la ongezeko la watu kila mwaka. Kwa mfumo wa idadi ya wafamasia 700, *assistant au technicians* wale wasiozidi 500. Hii ni changamoto kweli. Kwa tafsiri nyingine tunasema hivi leo kwenye zahanati zetu vituo vyetu vya Afya na hata baadhi ya mahospitali bado hayana Wafamasia, vituo vyetu vya Afya bado vinatolewa dawa siyo tu na *Nurse* na inawezekana kabisa akawa hajapata hicho cheti cha kuwa *Nurse*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kwenye zahanati na vituo vyetu vya afya kuwa na wataalam wachache sana na hasa kwenye zahanati, unakuta kina mtaalam mmoja tu ambapo yeye akiondoka akienda likizo au ameitwa kwa sababu kuna semina sehemu fulani, basi hiyo sehemu wanavijiji hapo wasiugue siku hiyo. Kweli changamoto ni nzito na jukumu ni zito kwa Wizara yetu ya Afya. Niwaombe tu kwamba juhudi hizi za vyuo usimamiaji wake, udahili na kuhakikisha kwamba wale wanaotoka wanapata nafasi ya kurudi na kufanya kazi Serikalini uongezewe mikakati ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kwamba sasa tuna Asasi zisizokuwa za Kiserikali, ni nyingi ambazo zinajihusisha na shughuli nyingi sana za kiafya. Kwa namna fulani ndiyo sehemu ambayo wale wanaomaliza vyuo wakiwa kama matabibu, wakiwa kama ma-*Nurse*, wengine Madaktari wanamezwu huko na kwa namna fulani kile ambacho tunakitegemea kwenye Serikali kwamba baada ya kuingiza wanafunzi kadhaa kwenye vyuo, mategemeo ni kuziba mapengo katika vyombo vyetu katika vituo vyetu vya kutolea huduma za Kiserikali unakumbana na changamoto hiyo kwamba wengi tunaowategemea waje wanakuwa hawaji kwa sababu wanamezwu na taasisi hizo zisizokuwa za kiserikali.

Mheshimwia Naibu Spika, lakini tunasema tunakwenda sambamba na *public private partnership*, ni mchango mzuri ambao taasisi hizi zinafanya, pengine ni kuziba mapengo ambayo Serikali ingewajibika kuyafanya. Lakini tuone kwamba sasa tuna changamoto na kuhakikisha kwamba pamoja na juhudi na kazi nzuri zinazofanywa na hizo Asasi hizo zisizokuwa za Kiserikali, ni wajibu wetu sasa kuona wanaoingia kwenye vyuo wanakuwa na mkakati wa kutosha ili waweze kufanya kazi katika vituo vyetu vya

Serikali na kuongeza ubora wa kazi na ubora wa makusudio wa malengo ya huduma ya afya nchini kwa kusudio zima la kupunguza vifo hasa vile vinavyoweza kuzuilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hoja na kushauri wenzangu kwamba tofauti zilizopo kati ya Baraza au *Council* ni kwamba, inasimamia taaluma lakini taaluma hiyo inakwenda sambamba na biashara na kwa namna hiyo ni vyema ikapata nafasi hiyo, lakini vile vile *TDFA* ikasimamia kwa makini zaidi ubora na usalama wa mlaji wa zao linalotolewa na vyombo vinavyozalisha madawa na vyakula. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi binafsi kabla ya kuendelea kuchangia naomba ku-*declare interest* kwamba ni Mjumbe katika Kamati hii na nilishiriki kuujadili Muswada huu tangu mwanzo mpaka mwisho, lakini leo hii napenda tena kutoa maoni kuhusiana na huu Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote nitumie nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali ambayo iliona tatizo hili na kuleta kwetu. Sisi Wajumbe tulijadiliana kwa kina sana na kuishauri Serikali juu ya masuala mbalimbali ambayo yanahusiana na huu Muswada. Lakini vile vile niliona kabisa kwamba Serikali iliupitia na mengi yamefanyiwa marekebisho. Kwa hiyo naamini kabisa kwamba kwa mchango wetu sisi Wabunge pamoja na wadau wengine, Serikali kama itafuata kile ambacho tulichangia, Muswada huu utakuwa bora na vile vile utasaidia kudumisha au kuimarisha afya katika sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo langu kwa kweli lilikuwa katika kipengele namba 37 ambacho niliona kabisa kwamba mamlaka ya hili Baraza yatakuwa makubwa mno, kwamba Baraza litengeneze dawa au kuna baadhi ya watu ambaeo ni Wajumbe katika Baraza hilo wafamasia, wanamiliki Viwanda vya Kutengeneza Madawa, wanamiliki maduka makubwa ya madawa hapo hapo wanamiliki maduka ya rejareja. Naomba kwa wamiliki wa maduka ya rejareja hasa vijijini wangebanwa sana kwa sababu Baraza lisema kwamba litakuwa linatoa adhabu, faini ya miaka miwili, jela au milioni 10. Ikaonekana kabisa kwamba kutakuwepo na *interest* kwa baadhi ya watu binafsi. Lakini kwa kuwa Serikali iliitikia na kukifanyia marekebisho kipengele hiki, naamini kabisa kwamba huu Muswada utasaidia sana kuboresha afya katika Majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho ningependa kukichangia kwa kweli Sekta ya Afya katika jamii yetu ya Tanzania bado ni duni sana hususan maeneo ya vijijini. Hasa hasa katika Jimbo langu la Tarime ambapo nilitembelea hospitali ya Wilaya nikakuta kwamba hamna Madaktari, Wafamasia hata Manesi, sasa tatizo kama hili, naombeni katika sheria hii Serikali ifanye haraka iwezekanavyo kuhakikisha kabisa kwamba Wafamasia wanapata *training* ya muda mfupi kama tuloutumia kuwaandaa walimu ili waweze kutusaidia katika hospitali zetu za vijijini. Baraza liwe na jukumu la kutunga mitaala kama tulivyopendekeza lakini ile mitaala iweze kuwasaidia wale watu ambaeo tunawaandaa ili kuweza kuimarisha afya za wanavijiji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo lakini natoa changamoto kwa Serikali, kwamba tunaanzisha sheria, hii sheria tumeifanyia utafiti wa kutosha mpaka vijijini? Watu wa vijijini watanufaikaje na hii sheria au wataumiaje? Hii ni changamoto ambayo pamoja na kuiunga mkono hoja hii, lakini naiachia Serikali itafiti kwa makini sana kwamba hii sheria tunayoitunga mtu wa kijijini inamnufaisha vipi? Au mtu wa kijijini anaathirika vipi? Lakini kwa sababu tutadhamiria kwamba tutaongeza wataalam mpaka vijijini naamini kabisa kwamba wataalam wakipatikana mpaka ngazi ya Kata na hata *dispensary* za vijiji, haya yote yatawezekana. Lakini hii ni changamoto ambayo kwa kweli mimi binafsi naiachia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulichangia ni kwamba tuangalie sasa hivi tunakoelekea katika dunia ya ushindani. Kuna umuhimu sana Baraza kama Baraza kusimamia biashara hasa wale wafanyabiashara ambao wataanzisha maduka wapitie au wasimamiwe na Baraza. Maana ukienda huko vijijini utakuta dawa zimeshatumika muda mwangi sana na zimeshapitwa na wakati, lakini watu wanabandua ile lebo inayoonesha *expired date*, wanaweka nyingine lakini hakuna mtu ambaye anaweza kuwafuatilia. Sasa kitu kama hiki tukisema kwamba tuwaacie Mamlaka ya Chakula wasimamie mambo kama haya ambayo sio ya kitaalam, naamini kabisa kwamba tutakuwa tunawaangamiza wanavijiji wetu au watu wengine katika sekta hii ya afya. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa kwamba Mamlaka ya Chakula na Dawa isimamie uingizaji na uuzaji, lakini masuala ya kiutaalam tuwaacie Baraza la Famasia lifanye kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali yetu kwa kuleta Muswada mzuri ambao una lengo la kusimamia maadili ya Wafamasia katika nchi yetu. Nina maeneo machache sana ambayo ningependa kuchangia na kupata ufanuzi baadaye kutoka kwa Waziri wetu wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua kwamba Mwenyekiti wa Baraza hili atatoka *Private Sector* au atatoka katika Sekta za Umma? Waagizaji wa dawa na watengenezaji wa dawa nchini karibu wengi ni watu binafsi na ukisema Baraza liwe na Mwenyekiti ambaye anatoka katika sekta binafsi nashindwa kuelewa kwamba yeze ni Mwenyekiti, yeze ni Mwingizaji wa dawa, yeze ni Mkaguzi, yeze ni mambo yote katika Baraza; sioni kama watatenda haki katika upande wa ukaguzi wa dawa, nadhani wao wabaki katika suala zima la kusimamia Wafamasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wengine walivyosema, katika kifungu cha 37 (1) na ile (b) yake, Baraza litasimamia wauzaji ambao ni *wholesalers*, yaani waingizaji wa dawa ndani ya nchi na dawa zinazotengenezwa ndani ya nchi. Kazi hii ni ya Mamlaka ya Usimamizi wa Dawa, *TFDA*. Nadhani kazi hii ibaki huko iliko kwa sababu wanaoingiza dawa na wanaosimamia dawa mpaka sasa nchini ni hawa *TFDA*, sioni sababu ya kutoa kazi hii kwa *TFDA* kama ilivyoolezwa katika sheria na wazalishaji waliopo nchini wanasmamiwa na *TFDA*, ndio maana ya Mamlaka na

Udhibiti wa Usalama wa Dawa na Chakula Nchini. Tuache kazi hii ifanywe na Mamlaka ambayo imeanzishwa kwa madhumuni husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie kifungu cha 14(1) ambacho kinasema kwamba Wataalam hawa Wanafamasia watakomaliza kazi, watakapotaka kujisajili katika Baraza itabidi wafanyiwe tena mitihani ya kitaaluma. Naona hapa ni *double work*, watafanya kazi mara mbili wakati hawa watakuwa wameshafuzu katika vyuo vyao na vyuo vinavyotambulika kisheria na vyuo vilivyoanzishwa kisheria. Wakishafuzu mitihani yao nadhani pasiwepo tena na sababu wanapotaka kujisajili wakafanyishwe mitihani mingine. Hapa naona kama Baraza litakuwa linawaonea hawa watu na wengine wanawenza wakapangiwa kazi katika maeneo ya vijiji ambapo hakuna namna ya kupata mawasiliano na Baraza na kuweza kusajiliwa. Nadhani wakishafanya mitihani na wakafaulu mitihani yao, basi waweze kusajiliwa kama ilivyo katika Mamlaka nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimeona kwamba Mamlaka itahusika sana na mambo ya kutoa elimu kwa Wafamasia, sio kazi mbaya na sio wazo baya, lakini sikuona kwamba pesa au gharama za kuwaelimisha hawa watu watazitoa wapi? Tuelezwe vyanzo vya mapato ambavyo watavitumia katika kuwaendeleza au kuwasomesha watu ambao watakuwa katika sekta hii ya Ufamasia. Nadhani kazi hii ni ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii au ni Wizara ya Elimu katika vyuo vyetu mbalimbali, kwa hiyo kazi hii iachwe katika sekta inayohusika ambayo ni sekta ya elimu ya juu na Wizara ya Afya yenye we ishughulike na hawa Wanafamasia ambao watataka kujiendeleza au ambao watataka kuongeza elimu yao kutokana na ujuzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwa na mengi ya kuchangia lakini bado nasisitiza kwamba ukaguzi wa dawa zinazoingia nchini na dawa zinazozalishwa nchini iachwe mikononi mwa *TFDA*. Kwa sababu sheria iliyounda Mamlaka hii inatamka hivyo, kwa hiyo, waachiwe kazi yao ambayo wametungiwa sheria na ambayo wanaitumia sheria iliyotungwa. Pia nizidi kusisitiza kwamba Mwenyekiti asitokane na sekta binafsi isipokuwa Mwenyekiti ateuliwe na Waziri anayehusika ili aweze kusimamia utendaji mzuri wa Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia Muswada huu ambao ni Muswada wa kwanza katika Bunge hili la Kumi lakini pia ni Muswada wa kwanza kwa mimi kama Mbunge mpya, kuweza kushiriki mchakato ambao ni sehemu ya majukumu ya Bunge ya kutunga sheria. Muswada huu ningependa kuuchangia katika eneo moja tu ambalo ni sehemu ya IV. Kama alivyozungumza Muwasilishaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu eneo la Biashara na Taaluma; ningependa kulisihi Bunge lako Tukufu, tukubaliane kwamba tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba tunachunguza misingi ambayo imesababisha udhaifu katika usimamizi mpaka tukaleta Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TFDA* imeshindwa ku-*perform*. Tumeleta Muswada kwa ajili ya kuboresha sheria ili kusudi iweze ku-*perform* lakini ni bahati mbaya sana

kwamba Muswada wenyewe bado misingi yake haitofautiani sana na ile sheria ya mwaka 2002 ambayo kimsingi ilipaswa kuboreshwa kwa Muswada huu wa Sheria ya sasa. Kwa hiyo, napenda kuchangia eneo hilo moja tu kwamba, Taifa letu lina tatizo la taaluma katika *pharmacy*, kwamba tuna tatizo la wanataaluma na tuna tatizo la kudhibiti taaluma katika utendaji wa sekta nzima ya *pharmacy*. Kwa ushauri wangu ni kwamba, sheria hii au Muswada huu unapaswa kuzingatia eneo kubwa ambalo ni la msingi la kutenganisha majukumu ya Baraza na majukumu ya *TFDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuhakikishe kwamba kwa kuwa *TFDA* pengine ilishindwa ku-*perform* kwa sababu ya kuchanganya biashara na taaluma, sasa tupate sheria mbili; tuwe na sheria ya watu ambao watahusika na biashara na tuwe na sheria ya watu ambao watahusika na kusimamia taaluma kama ambavyo Bodi nyingine zinafanya. Hapa kuna watu wana mashaka, kwamba pengine *TFDA* ikipewa jukumu la kusimamia biashara wakati Baraza ndilo ambalo linasimamia taaluma itakuwa tatizo. Sioni tatizo kwa sababu hata kwenye Bodi ya Uhasibu inakupa cheti kwamba wewe ni Mhasibu lakini haikupi leseni ya biashara na bado ufanisi unakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kushauri Bunge lako Tukufu kwamba tukubaliane Bodi, kwa maana ya Baraza, ibaki na usimamizi wa taaluma. Ihakikishe kwamba tuna uwezo wa ku-*manage* idadi ya wanataaluma katika eneo hili. Badala ya wanataaluma kutokomea nje kwa sababu ya maslahi duni, Bodi iangalie ni kwa namna gani ambavyo inaweza ikaboresha eneo hilo. Badala ya watu wengi kuikimbia taaluma hii kwa sababu pengine inashindwa kulipa vizuri, tuangalie ni kwa namna gani tunaboresha eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya uchache pengine wa wanataaluma kutokana na watu ambao wanahitimu elimu ya fani hii, Baraza hili liangalie ni kwa namna gani ambavyo tunaongeza kiasi cha kutosha katika eneo hilo. Kwa hiyo, Baraza hili lihusike na kuangalia ni kwa namna gani tunaongeza wanataaluma na ni kwa namna gani tunaongeza nidhamu ya wanataaluma ili kusudi kuongeza ufanisi katika taaluma. Lakini sasa Baraza hili lisimamie taaluma, wakati huo huo lisimamie biashara, ile *check and balance* itakosekana na matokeo yake ni rahisi sana kuvuruga mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni uzoefu wa kawaida tu, mpaka leo tunazungumza kutenganisha siasa na biashara, ni mambo ya kawaida tu kwa sababu ukiyachanganya mambo hayawezi kwenda kwa sababu yatakuwa yanaingiliana. Lakini ukitenganisha taaluma ya *pharmacy* na biashara ya *pharmacy* ni wazi kwamba kazi itakwenda kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuwashauri ndugu zangu Wabunge na Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu lengo lake kimsingi kabisa ilipaswa iwe ni kuboresha taaluma ya *pharmacy* katika nchi yetu. Katika madhumuni yao wameeleza lakini kwa bahati mbaya sana katika *content* wamechanganya kwamba badala ya kusimamia dhumuni hili ambalo wameleleza la kusimamia taaluma na kuboresha taaluma katika eneo la *pharmacy* sasa wanachanganya na sehemu ya nne ambayo inaingiza biashara katika eneo la taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuwasihii, Wajumbe wa Kamati wamezungumza hapa kwamba tuondoe eneo la *wholesale* kufanywa na Baraza, lakini nashangaa ni kwa nini muone kwamba eneo la *wholesale* ndio ambalo linapaswa kuondolewa kwenye Baraza, lakini wakati huo huo michakato mingine ya kibashara kwa maana ya *level* ya *retail* ibakie kwenye Baraza, *this is a contradiction*. Ndio maana nafikiri tukubaliane na ushauri ambaa umetolewa na Kambi ya Upinzani, kwamba Muswada huu uwe ni maalum kwa ajili ya kutenganisha taaluma na biashara. Kitendo cha Kamati kupendekeza kwamba eneo la *wholesale* peke yake ndicho ambacho kiondolewe, ni bahati mbaya kwamba sababu yake haikutajwa bayana, kwamba ni kwa nini tunadhani tunaondoa eneo la *wholesale* peke yake kwenye kifungu cha 37 na tusiondoe eneo lote la biashara kwenye kifungu kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningependa tu kuwashauri wenzangu na Bunge lako Tukufu kwamba uzoefu unaonesha hivyo. Kuna nchi kama Ujerumanii wanatenganisha, ni vitu tofauti. Kuna Bodi ambayo inahusika na biashara ya *pharmacy* tu, tena wao wanakwenda mbali zaidi kwamba mtu hapaswi kuwa na duka zaidi ya moja. Kwamba mtu mmoja katika nchi ya Ujerumanii haruhusiwi kuwa na maduka mawili ya dawa. Sasa wao pengine ni kwa sababu ya kiwango cha maendeleo ambacho wameshakifikia, sisi pengine kwa sababu ya umaskini bado hatujafika huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokizungumza hapa ni kwamba, tunazungumzia kiwango cha udhibiti wa kutenganisha hawa watu, kiwango cha udhibiti wa namna gani ya kutenganisha biashara na hii taaluma. Tuongeze kipengele kwenye hii *schedule of amendment* ambacho kitaondoa sehemu yote ya IV ili kusudi kwa pamoja tuupitishe Muswada huu ambaa ni muhimu sana kwa sasa hasa kwa kipindi ambacho tuna tatizo kubwa la nidhamu, ufanisi na maadili katika taaluma hii ya Ufamasia, kuliko katika maeneo mengine na hasa ukizingatia kwamba mnapokosa maadili katika eneo la Ufamasia tafsiri yake ni kwamba mnacheza na maisha ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba....

(*Hapa sauti ilikatika*)

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niseme kwamba mimi ni mmoja katika Wanakamati. Lakini vile vile naomba *declare interest* kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Baraza la Famasia ambaye ninamaliza muda wangu hivi karibuni, lakini vile vile mimi ni Mfamasia. Kwa hiyo, nimeomba kuchangia ili kusudi niweze kusaidia kidogo katika kuelezea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Sheria ya *Pharmacy* inakuja ili kusudi kuwezesha wanataaluma kuweza kusimamiwa katika kufanya kazi yao na kuwanusuru wananchi waweze kupata dawa kufuatana na maadili. Wengi mtakubaliana nami kwamba sasa hivi kumekuwa na matatizo makubwa sana kwenye sehemu nyingi sana ambako ndiko wanakofanya kazi. Kumekuwa na utoaji wa huduma isiyoridhisha, kumekuwa na uuzwaji wa dawa, kukiuka sheria, sasa hii sheria ilikuwa inatarajiwa imsaidie

mwananchi, ambaye mara nyingi sana ni mgonjwa, ili aweze kupata huduma inayostahili. Ni wapi anapata huduma hiyo? Huduma hii ni kwamba ni lazima umdhibiti huyu mwanataaluma ili kusudi asicheze na maisha ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, unamdhiliti wapi? Unamdhiliti katika maduka ya dawa, unamdhiliti katika *wholesale*, unamdhiliti katika utengenezaji, unamdhiliti katika ufundishaji, unamdhiliti katika usambazaji. Ni lazima umdhibiti katika nyanja zote, hakuna ya kuchagua, huwezi kusema kwamba nitakwenda kumdhiliti katika hiki ukamuacha katika hiki, ni lazima umdhibiti sehemu zote. Sasa hiki ndio kitu inachokisema hii sheria. Nakubaliana na wenzangu wengi kwamba kumekuwa na mapungufu na maneno ya kubadilisha, kama ilivyo katika *schedule of ammendments* ambayo imesambazwa. Ni sahihi kabisa, ndio tuliyokaa tukajadili, tukitilia maanani na matakwa au maoni ya wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaposema kwamba huyu Mfamasia usimdhiliti mahali fulani, maana yake ni kwamba ile *area* unayoiacha unaiacha bila kuangaliwa na mtu yejote. Jamani, hawa wateja wa hawa Wafamasia ni wagonjwa ambao hapa hawapo kujitetea, ni sisi ndio tunaowatetea. Kwa hiyo, kama hujamdhiliti huyu huwezi kumtetea huyu mgonjwa na huwezi kumdhiliti huyu Mfamasia barabarani, ni lazima umdhibiti katika sehemu yake ya kazi. Hivi huyu mtu ambaye hana kibali cha kuuza dawa anapata wapi zile dawa kama hakuuziwa na huyu Mfamasia ambaye yuko pale sheria, sasa hivi haimpi mamlaka yule kwenda kuangalia utendaji wake wa kazi anapofanya kazi anatakiwa kuna vitabu ambavyo lazima ajaze na vikae pale kwa muda wa miaka kadhaa, ili Mkaguzi akienda acheki kwamba kweli alichotoa ndio sahihi? Sasa huyu unamdhiliti wapi? Lakini sisi sote tunajua kuna madawa yanauzwa ambayo ni feki, kuna dawa ambazo watu hawaruhusiwi kuziweka, wameziweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu ni msingi mzito sana huwezi kusema unafundisha watu kwa muda wa mwezi mmoja au miwili halafu waende wakachezee maisha ya mtu wanachezeaje maisha ya mtu kwa kumfundisha miezi miwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile naomba tuelewe kwamba huyu Mfamasia ana *deal* na madawa, madawa kila siku yanatengenezwa na yanazaliwa upya. Nyuma kama nikitoa mifano, tulikuwa tunatumia *cloroquine*, tukatoka kwenye *cloroquine*, tukaenda kwenye *metakelfine*, tukatoka *metakelfine*, sasa hivi kwenye *Alu*, *combination* ya dawa mbili. Hivi huyu Mfamasia ambaye haendi shule kwenda kujifunza upya akajua, kwa sababu Wazungu wanasesma hii fani sio *static*, ni *dynamic* inaendelea kukua siku zote, kwa hiyo ni lazima uno kichwa cha Mfamasia kila siku aendane na maendeleo yanayotokea katika ulimwengu, aendane na masuala yote ambayo yanahu maendeleo ya dawa za ulimwengu. Kwa hiyo, huwezi kusema kwamba huyu Mfamasia akitoka shulenii basi, kuna watu ambao tunawaita *professional students*, ambaye yeye ni mwanafunzi lakini ukimpeleka kwenye *practice* ni *zero* kwa sababu gani? Huyu ni lazima aende akafanyiwe *test* kwamba je, ameshinda kile kiwango anachotakiwa? Kama hajashinda anapewa *chance* nyingine ya kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa kwenye Kamati lakini naomba nisisitize na niwaombe ndugu zangu Wabunge, Wizara imechambua kwa kina sana na imeona na sisi tuliona kweli tulikubaliana tulitoa hoja na inaonyesha kwamba Wizara imefanya kazi hoja kama ilivyokuwa kwenye *schedule of amendments*. Kwa hiyo, naomba niwashawishi ndugu zangu, ili kusudi kunusuru maisha ya Watanzania kuhakikisha Watanzania wanapata huduma iliyokuwa sahihi, kuhakikisha Watanzania hawatapeliwi kupewa dawa ambazo hazistahili kupewa wao, hatufanyi kazi kwa ajili ya kumnufaisha mtu binafsi, hatufanyi kazi kwa ajili ya kunufaisha familia ya mtu binafsi, tupidishe Muswada huu ili wananchi wetu wa Tanzania waweze kupata huduma bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga hoja Muswada huu kama ambavyo imeletwa na Mheshimiwa Waziri pamoja na *schedule of amendment* ambayo naiona kabisa inakidhi mambo mengi ambayo yamesemwa. Naomba kurudia kusema tena mimi ni Mfamasia, kwa hiyo nina *interest* lakini sio ya hela na mimi ni Mwenyekiti wa Baraza ambaye sio mwajiriwa, sipati mshahara wala sina *interest* ya hela humo ndani kama kanuni zetu zinavyotuambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kuunga mkono Muswada. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zarina Madabida na umefanya vizuri kabisa ku-*declare position* yako na unatudhihirishia kwamba wako Wabunge amba ni wasomi wanaoelewa haya mambo, hongera sana. (*Makofi*)

Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani kabla, naomba sasa achukue nafasi hii kuwa mchangiaji wetu wa mwisho mchana wa leo na jioni tutaendelea ni Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani.

MHE. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nami ili kuweza kuchangia katika Muswada huu ulioko mbele yetu. Kwanza niseme tu kwamba, ile Kamati iliyokuwa imeujadili huu Muswada imekuja kuainisha maeneo mengi ambayo walikuwa wanatofautiana, lakini hatimaye wakasema wanaunga mkono Muswada, sasa nilifikiri wangeupinga kabisa. Lakini bahati nzuri kuna hii *schedule* imeletwa imejaribu kupunguza baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa na utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina kitu kimoja ambacho nilifikiri ni vizuri wakati tunaujadili huu Muswada tukazingatia jinsi Serikali ilivyowekeza kwa gharama kubwa kujenga Maabara ambazo zinaangalia ubora wa madawa kulq *TFDA*. Lakini nazingatia vilevile ni muhimu sana taaluma ya Wafamasia kufuatiliwa kwa karibu jinsi wanavyotenda kazi zao na jinsi wanavyozingatia matumizi bora ya madawa. Lakini vilevile tusiharibu juhudhi kubwa ambayo tumeshafanya mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lingine nililokuwa napata tabu ni huu muundo wa Baraza hili, nimeona kwenye *schedule of amendment* wameeleza kwamba Mwenyekiti atatoka *private*. Madawa yote ni *potentially* lakini madawa yanawenza kutumika kama silaha, vilevile vyakula vya kuharibu nchi yasipotumika vizuri, *is a National Security*. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kumpa mamlaka mtu wa *private* naona kama Serikali inaachia hili jukumu muhimu kwa mtu tu, anaweza kweli akawa mtu muadilifu kama mama yetu hapa aliyemaliza kuzungumza lakini kama ikitokea akawa *corrupt*, Serikali inachukuaje wajibu huu. Nafikiri ni muhimu sana wakaangalia huu muundo.

Lakini vilevile katika muundo wao wanazungumza hii habari ya Kamati na uwezo wa kuteua Wakaguzi wa Madawa, wanasema, wanaweza wakateua ye yeyote, sasa utateuaje ye yeyote asiye na sifa. Nafikiri ni vizuri wakaliangalia hili wakabainisha kabisa wazi kwamba watakaoteuliwa wawe na sifa fulani. Lakini katika muundo vilevile nimeona Baraza hili ambalo linakuwa na majukumu ya madawa ya aina zote, uwakilishi wa *veterinary profession* hauonekani japo madawa ni madawa lakini yanatofautiana sana matumizi kwa wanyama na binadamu. Kama hili Baraza linadhamiria kuwapa mamlaka hayo yote, basi lazima kwenye uwakilishi *veterinary professional* ione kane hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimeona katika vifungu vya 42 na 43 vinaleta mkanganyiko kidogo katika taaluma hizi hizi tena za Wafamasia lakini vilevile jinsi ya watu wengine ambao wanaweza kutoa madawa. Wa-*veterinary* wamefundishwa kwa ukamilifu kutoa madawa na tuna tatizo la Wafamasia kuwa ni wachache katika nchi. Sasa kwenye *clinics* za mifugo hakuna Wafamasia lakini hawatajwi dhahiri kwamba hawa watu wanaruhusiwa na sheria yao ipo, iko *Veterinary Act*, iko Sheria ya Baraza la *Veterinary* ambalo liko huru kabisa imetungwa na Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri sana wakabainisha wazi kwamba kuna watu wengine ambao watakuwa na mamlaka ya kuendelea kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile na tatizo la huu uchache wa wataalam Wafamasia kwenye maeneo ya vijijini ambako unaweza ukakuta Wilaya ina wafamasia walio-*qualified* labda wawili, sasa huko kwenye maduka ya vijijini huko kwenye zahanati za vijijini huko wanasmamiae hawa. Sasa tunachoona mara nyingi kule ni kwamba, wanatoa vyeti na vyeti tu ndiyo vinafanyiwa biashara kwamba anasimamia lakini sio kweli wanasmamia. Sasa nafikiri hapa kuna haja ya kuangalia namna ya kurahisisha hii huduma ya utoaji wa madawa kwa maeneo mengine. Wenzangu wameshazungumza kuna Manesi, kuna Waganga wasaidizi wako kule vijijini wanafanya, sasa labda tuangalie namna gani ili kazi ile ifanyike kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ambalo nilipata utata ni kwenye kifungu cha 52 *indemnity of liability of the members*, hawa wanataka kulindwa, hawa kwamba wakifanya kitendo chochote au maamuzi yoyote wasiguswe. Jamani katika dunia ya sasa kuna mtu anataka asiguswe kwa nini, sasa hivi watu wanazungumzia hata mamlaka ya Rais wanahoji yaangaliwe, sasa hawa wao wanataka walindwe kwa nini? Kama watafanya kitu ambacho hakiko sawa ni lazima waulizwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kinga naona inaweza ikatupeleka kwenye mazingira ambayo watu wakiwa *corrupt*, wakifanya kundi la watu wanaotaka kufanya hujuma ina maana wasiguswe na sheria, hapana. Nafikiri hiki kipengele hakistahili kwa

dunia ya sasa na vilevile kinaweza kikawapa mamlaka kwa washindani wengine wa kibashara kama wajumbe wa Baraza hili wanaweza kuwa na *interest* katika biashara. Sasa inaweza kuwa rungu la kuhujumu au la kudhulumu watu wengine, nafikiri ni vizuri sana hii kinga kubwa wanayotaka kijiwekea iondolewe, haihitajiki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, nafikiri kwamba marekebisho haya yakikaa vizuri Muswada huu ni wa msingi, tunahitaji sana sana kusimamia afya za watu wetu, lakini Serikali lazima iwe na mkono wa dhati katika usalama wa madawa. Ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu muda wetu hauturuhusu kwa mchangiaji mwingine inabidi twende kwenye mapumziko ya mchanana. Naomba niseme tu bado tunao wachangiaji karibu 13, tutajitahidi kuwachukua kadri iwezekanavyo kwa jioni ya leo, niwataje watakaoanza ili kuwahi kuingia humu ndani, nao ni pamoja na Mheshimiwa Said Suleiman Said, Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba na wengine watafuata.

Basi baada ya maelezo hayo niwaombe sana Kamati pamoja na Mheshimiwa Waziri na wale wanaohusika maana kwa kweli wametuchanganya, Kamati wamekuja na ya kwao na Mheshimiwa Waziri na yeye ana msimamo fulani. Basi ni vizuri jioni tukapata maelezo mazuri ili *at least* kutusaidia katika kutuweka sawa ili tutakapofika kwenye vifungu kwa vifungu tusipate tabu sana.

Waheshimiwa Wabunge baada ya maelezo hayo, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(*Saa 6.59 mchanana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Famasi wa mwaka 2010, yanaendelea. Naomba nimwite mchangiaji wetu wa kwanza kama yupo humu ndani Mheshimiwa Said Suleiman Said, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah.

MHE. SAID SULEIMAN SAID: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kuchukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu wa Famasi ambao uko mbele yetu.

Vilevile, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kuweza kuuleta Muswada huu wa Famasi kwa wakati katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kuchangia labda nielezee tu kidogo madhumuni ya hii *Pharmacy Bill*. Madhumuni yake ni kuwa chombo ambacho kitasimamia taaluma ya famasi pamoja na maadili katika utendaji wa kazi zao.

Vilevile, naomba niungane na wachangiaji waliotangulia kuzungumza, lakini naomba nitofautiane kidogo na wachangiaji wengine kutokana na maelezo ambayo wameyatoa. Naomba nielezee kuhusu mambo mawili kabla ya kuendelea na Muswada. Moja ni kuhusu Taasisi ya *TFDA* na uhusiano wake na huu Muswada wa Famasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni Taasisi mbili za Serikali, *TFDA* ni chombo ambacho kimeundwa kusimamia usalama na ubora wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaatiba. Halikadhalika, *Pharmacy Council*, ni chombo ambacho kitasimamia taaluma ya *pharmacy* pamoja na maadili yake na utendaji kazi. Sasa ni vyombo viwili vya Serikali ambavyo vinafanya kazi kwa pamoja na kwa kushirikiana isipokuwa vina majukumu tofauti. Hapo mwanzo vilikuwa ni vyombo vilivyofanya kazi pamoja lakini sasa *TFDA* baada ya Muswada huu kuitishwa kuwa Sheria itabakia kuwa inashughulikia *product* ya dawa yaani usalama wake na ubora wake. Vilevile wao watakuwa wanawajibika kwa watu wote ambao wanaagiza madawa kutoka nje ya nchi na kuyaingiza nchini yaani *importers* na wale *manufactures* wetu *locally* walioko ndani kwa sababu kutokana na utaratibu wa Sheria wanatakiwa mtu yejote kabla ya kutengeneza dawa au kabla ya kuingiza dawa ni lazima wapitie *TFDA* na Mamlaka hayo bado yako mikononi mwao, hawajanyang'anywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa moja kwa moja niende kwenye Muswada huu lakini kwanza niende kwenye *Part One, page five* ambapo kuna *interpretation* yaani tafsiri ya maneno. Ukiangalia hapa utakuta kuna tafsiri nyingi zimewekwa lakini kuna baadhi ya maneno ambayo yametumika kwenye Sheria hii lakini hayatolewa maana. Maneno hayo ni “*officer*” ambalo linapatikana Kifungu cha 5(e) na “*organisation*” ambalo linapatikana katika Kifungu hicho hicho. Neno lingine ni “*proper person*” ambalo linapatikana Kifungu cha 37(4) na lingine ni “*any other person*” ambalo linapatikana Kifungu cha 39(3). Ni vizuri tukapewa tafsiri halisi ya maneno haya ili yasije yakatumika vibaya wakati Sheria itakapopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili naomba niupeleke kwenye kazi za *Council* au Baraza. Hapa zimetajwa kazi nyingi, kuanzia moja mpaka ishirini. Lakini moja ya kazi ya chombo cha kitaalamu ni kufanya utafiti, sasa Baraza hili halikupewa uwezo au haikutajwa hapa miongoni mwa kazi zake kama itafanya utafiti. Ni vizuri kama Baraza lipewe uwezo huu wa kufanya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niende kwenye ukurasa wa tisa, Kifungu cha 5 ambapo madaraka ya Baraza yameelezwa na kuna kukasimu madaraka. Kuna watu wametajwa ambao wanatakiwa wakasimiwe madaraka, kuna neno *officer or inspector or any organization*. Neno *inspector* liko katika tafsiri lakini haya maneno mawili na yale ambayo nimeyataja mwanzo hayakutolewa ufanuzi. Naomba ili kuondoa *misuse of power* mara Sheria hii itakapopita, ni vizuri tukapata ufanuzi wake, ni nini kilichokusudiwa hasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika hiyo *delegation of power*, ni vizuri kukawa na *limit of delegation* hasa kwa yule mtu ambaye si sehemu ya *Council*, kuwe na *limit* ya kupewa madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Kifungu kingine, *page nine, section 6(2) na page 10* Kifungu cha 7(2) ambapo kuna *Pharmacy Committee na Disciplinary Committee na its composition*. Sasa hapa imeelezwa tu kwamba Wenyevit wa hizi *Committee* watakuwa ni *Council members* lakini wale *members* wa hizi *Committee*, wanasema watateuliwa. Sasa naomba maelezo ya vigezo vyao na mchakato wa kuteuliwa utakuwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, *section* nyingine ni *section 9(2)* ambayo iko *page 10* kuhusu mikutano ya *Committees*. Humu imeelezwa kuwa *Council* inaweza ikamuagiza Mwenyekiti wa hizi Kamati kuitisha mikutano wakati wowote lakini ni vizuri tukajiwekea utaratibu wa kukutana kama kila baada ya miezi mitatu au sita na hiyo ya wakati wowote wanapotakiwa kufanya mikutano, bado ikabaki kuwa palepale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye *page 16, section 24(1)(b)* ambapo kuna usajili wa Fundi Dawa Sanifu, pamoja na sifa ambazo anatakiwa kuwa nazo lakini kuna neno pale katika *paragraph* ile “*additional requirement*” ni vizuri hizi *additional requirement* zikawekwa bayana ili kuondoa hii *bias*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye *page 21, section 37(4)* katika *type of permit, revocations, suspension and cancellation of permit*. Mtu anapotaka kuomba kibali cha dawa anatakiwa apeleka maombi yake katika *Council*, lakini *Council* vilevile imepewa uwezo wa kukubali au kukataa ombi lile kutokana na misingi aliyoombea lakini kuna maneno ambayo yameandikwa, naomba ninukuu:-

“*Where the Council consideres that the applicant is not fit and proper person to be issued with a permit to carry on any business specified under this section it shall refuse to issue the permit, as the case may be.*”

Sasa hapa neno “*proper person*” halikuwa *defined* vizuri kwa sababu mtu anaweza kunyimwa haki yake akaambiwa wewe siyo *proper person*, ni vizuri nalo hili likawekewa ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo naomba nitolee ufanuzi ni *page 21, section 38* kwenye maadili ya famasi yaani *Pharmacy practice* ambapo inasema wale wote ambao wamekuwa *registered* yaani *Pharmacist, Pharmaceutical Technician, Pharmaceutical Assistants* watapangiwa majukumu na maeneo ya kazi. Ni vizuri haya yakawekwa bayana ndani ya Muswada huu.

Tukitoka hapo naomba twende *page 22, section 39(3)* ambapo kuna matumizi bora ya dawa yaani *rational use of medicine*. Pale kuna maneno yameandikwa

“appropriate practitioner” na imetolewa maana yake na wametajwa kwamba mmoja ni *Medical Practitioner, Dentist* na mwagine ni *Veterinary*. Lakini Mheshimiwa Waziri kapewa uwezo wa kumteua “any other person”, sasa hapa ndijo naomba nipaye ufanuzi huyu “any other person” ni mtu wa aina gani yaani sifa zake na kwa misingi ipi au ni kwa wakati upi Waziri anatakiwa amteue huyu “any other person”?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya michango hiyo ambayo ipo ndani ya Muswada, naomba niende kwenye michango ya jumla ambayo ni changamoto Sheria hii itakabiliana nayo mara baada ya kupitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ambalo lipo mbele yetu hivi sasa ni upungufu wa rasilimali watu, fedha na vitendea kazi na ukiangalia hasa *report* ambayo tumeipata kutoka Wizara ya Afya, mpaka sasa hivi tuna Wafamasia 850, Mafundi Dawa Sanifu 550 na Wasaidizi ni 378 na wale wageni ambao wamesajiliwa ni 25 ambao wanaleta hesabu ya 1,803. Ukienda na *ratio* ya *population* yetu ya *40 millions* ya Watanzania wote, utakuta mhudumu mmoja anahudumia watu karibu 220. Sasa hili ni eneo ambalo Wizara ilione na ilifanyie kazi. Naomba nitoe mapendeleko kuwa tujaribu kuhamasisha sekta binafsi iweze kuwekeza katika kujenga vyuo ili kuweza kuondoa hili tatizo la rasilimali watu. Lakini kuhusu fedha na vifaa, nitamwomba Mheshimiwa Waziri wa Afya na Waheshimiwa Wabunge itakapokuja bajeti ya Wizara ya Afya, tuwaongezee bajeti yao ili tuweze kuondoa hili tatizo la kwanza. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo au changamoto nydingine ya pili, ni dawa kutolewa kiholela na watu wasiokuwa na taaluma, hili kwa kweli limedhirika. Lakini kutokana na maelezo mazuri ambayo yapo au utaratibu ambao unaandaliwa na Wizara ya Afya, kuna utaratibu wa kuyahamisha Maduka ya Dawa Baridi na kuingia katika maduka ya Madawa Muhimu (*ADO*), ni vizuri hawa wakakaguliwa na kupewa ule ukaguzi elekezi ili huduma wanazotoa ziwe bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo naomba niende kwenye udhibiti wa madawa feki na yasiyo na kiwango na yale ambayo yamepigwa marufuku kuingizwa nchini yaani yale ambayo yanabadili maumbile ya binadamu. Tatizo la dawa feki limeenea katika nchi yetu lakini pia katika nchi zote za Kanda ya Afrika, hili limekuwa ni tatizo sugu. Mambo mawili makubwa ambayo yanachangia hapa ni kuwa na mipaka mingi isiyokuwa rasmi ambayo iko nchini mwetu. Hawa wanaoingiza madawa wanatumia mipaka hii kuingiza dawa feki na ambazo zimepigwa marufuku. Lakini vilevile kuna wafanyabiashara wachache wakorofii ambao wanatumia njia hizi kuingiza dawa nchini wakikwepa ushuru na kulikosesha Taifa letu mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo linasababisha kuwa na madawa feki, ni mfumo tofauti wa udhibiti wa madawa mionganii mwa nchi wanachama wa Afrika Mashariki na nchi za *SADC*, kila nchi inakuwa na mfumo wake. Sasa ni vizuri mifumo ya dawa ikaweza kuwiana yaani ikakubaliana ili sote kwa pamoja tupige vita tatizo hili la dawa feki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la mwisho nalopenda kuchangia, ni elimu ndogo kwa jamii kuhusu utumiaji wa dawa bora na sahihi kwa matumizi halisi. Hili tunaliona kwani watu wengi hivi sasa wamejenga tabia wanapoumwa badala ya kwenda hospitali au kumwona Daktari moja kwa moja wanakwenda katika maduka ya dawa na kutafuta dawa, hali hii inahatarisha maisha yao. Aidha, wale ambao wanatumia zile dawa za kubadilisha maumbile laiti wangekuwa wamepata elimu hii, nafikiri wengi wao wasingeweza kutumia dawa hizi. Sasa ni vizuri chombo hiki ambacho tunakiunda kisimamie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana.
(*Makofi*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami pia nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Muswada huu uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Wataalamu wote wa afya, kwa kuandaa Muswada huu ambao ni muhimu sana na kutuletea hapa Bungeni ili tuweze kuujadili na kuweka *inputs* zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu sana kwa sababu moja kwa moja unahusu afya ya Mtanzania, yaani unahusu wananchi na afya zao. Nia ya Muswada huu ni kuunda Baraza la Famasi linaloshughulika na taaluma na maadili ya wanataluma pamoja na kusimamia viwango na ubora wa huduma za famasi katika Taasisi za Umma na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Tanzania tunalo tatizo kubwa sana kwenye suala la famasi ndogondogo zilizopo kwenye vijiji vyetu. Tunajua na Serikali inafahamu kwamba famasi zilizopo kule vijijini na maeneo mengi zinatumika kama ndizo hospitali kwa sababu unakuta sehemu nyingine mwananchi analazimika kutembea zaidi ya kilomita 20 au 25 na hata 30 akifuata hospitali kwa sababu ya upungufu wa Vituo vya Afya, hizi famasi ndogondogo zimekuwa ndiyo hospitali, wananchi wanapata huduma zao kule. Mtoto akiumwa anachukuliwa, anapelekwa famasi ndiyo anapata dawa kwa hiyo biashara imeisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuwepo kwa ubora wa dawa zote zinazotolewa kwenye zile famasi ni muhimu sana na kwa bahati sana hizi famasi za vijijini zimekuwa hazina viwango, tukianzia na yale maeneo yenyewe yaani ile famasi ilipo, kile kibanda ni kidogo, ndani ukiangalia zile dawa kwenye *prescription* au *leaflet* inasema dawa ziwekwe chini ya *temperature ya two degree centigrade*, lakini unakuta kibanda ni kidogo wala hakina *ceiling board*, ni bati, kuna joto la ajabu, dawa ambazo zinatakiwa kuwekwa kwenye friji haziko kwenye friji. Kwa hiyo, ukiangalia utaona dawa inayotolewa kwenye yale mazingira siyo bora na ndiyo maana unakuta wakati mwingine mtu anatumia dawa ambayo wala haiwezi kumsaidia lakini wananchi wafanyaje kwa sababu ndiyo mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia pia wale wanaotoa huduma kwenye hizo famasi za vijijini unakuta pamoja na mazingira halisi kwamba kile kibanda hakifai kuwepo kwa famasi lakini pia mtu anayetoa ile huduma hana ujuzi wala uelewa wowote kuhusu madawa. Unachukua dawa, unamuuliza dawa itumike mara ngapi? Anakwambia tumia mara mbili. Kama wewe ni muelewa, ukichukua *leaflet* ukisoma unamuuliza kwa nini mbona ninaona hapa ni mara tatu, anakwambia basi tumia utakavyoona. Kwa hiyo, *standard seven* ndio wanaotoa huduma kwenye zile famasi za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona hili Baraza ni muhimu sana, litasimamia kikamilifu kuhakikisha kwamba famasi zetu zinakuwa na viwango. Kwa kweli hatutaki zisiwepo kwa sababu maeneo ya vijijini na hali halisi ambapo Serikali hajjaweza kusambaza huduma za vituo vya afya, maeneo yote bado zinahitajika. Tunataka ziboreshweli ili wanaotoa huduma wawe ni watu ambao wana fani za famasia, vile vibanda viwe ni vibanda vinavyofaa na wafuate utaratibu unaotakiwa na kuwepo na *inspection* ya mara kwa mara. Unakuta vile vibanda vinavyouza dawa, dawa zina- *expire* wala anayeuzza hana habari, wewe unayekwenda kununua kama ni mwelewa ndiyo uangalie, unamwambia kwamba mbona dawa *ime-expire* anakwambia na mimi mwenyewe sikujua. Kwa hiyo, kwa kweli tunahatarisha maisha ya wananchi wetu kwa kuruhusu wapate dawa katika mazingira ambayo siyo mazuri na kuruhusu kupewa dawa na watu ambao hawana ujuzi wowote wa kutoa dawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kusisitiza ni kwamba Baraza la Famasi *wa-deal* na taaluma ya Famasia, tuache *TFDA* wafanye kazi yao ya kuangalia ubora, uzalishaji na usambazaji kwa maana kwamba Serikali bado ibebe jukumu la kuhakikisha ubora wa dawa zinazotolewa. Tukichanganya mambo haya mawili, tutakumbana na matatizo yaleyale ambayo *TFDA* kwa muda wote wameshindwa kusimamia. *TFDA* wapo lakini biashara zimekuwa zikifunguliwa kiholela, mimi nashindwa kuelewa ni kwamba hawana meno au wameamua kuwa *idle*? Kwa kweli, ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuwapunguzie majukumu sasa ili wabaki na jukumu la viwango yaani wahakikishe *production* ya dawa inatoka vizuri, ina viwango vya kutosha, usambazaji umekwenda vizuri, wananchi wanapata dawa kwa muda na kwa njia hiyo basi Serikali iwawezeshe *TFDA* kwa kuwapatia vitendea kazi kama ni magari au kufungua ofisi sehemu mbalimbali ili kuhakikisha kwamba wanafanya kazi kwa viwango lakini jukumu lake linaendelea kubaki palepale la kuhakikisha ubora wa madawa unakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ni tatizo tulilonalo Tanzania sasa hivi, ni suala la uingizaji wa madawa kiholela nchini. Kwa kweli nimekuwa nashangaa muda wote hivi kwa nini Serikali inaweka rehani maisha ya Watanzania wake? Ukienda unakuta madawa yanayotumika kwenye tumbo la binadamu yanauzwa kwenye mabasi kama njugu au karanga, unakuta barabarani dawa zinauzwa kama njugu, vijana wengine hata hawakwenda shule lakini wanatembeza dawa na wananchi kwa uelewa mdogo wanenanua na wanazitumia. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana, ni tatizo kwa sababu

hata wale wanaotembeza zile dawa hawana lolote, ni wafanyabiashara tu, kwa nini Serikali isiweke viwango?

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kwamba tukiiwezesha *TFDA*, wataweza kufanya kazi yao kikamilifu na kuhakikisha kwamba kabla dawa haijaingia nchini iwe imefanyiwa utafiti wa kutosha, tusikubali kuweka rehani maisha ya Watanzania wetu kwa kuruhusu kila dawa itumike, hapana! Sitaki kusema kwamba tusiruhusu dawa zisiingie kama tunavyosema kwamba Wachina wasilet dawa zao kwa sababu ndiyo zimejaa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kulikuwepo na swal hapa Bungeni, Mbunge aliuliza kwamba, sasa hivi matatizo ya meno yameongezeka Tanzania na wataalamu ni wachache. Tujiulize, sasa hivi kuna dawa za meno hazina idadi huko zinakouzwa na kila mmoja ananunua pengine ndizo zinazotuleta matatizo, hatujui ubora wake tunatumia tu, hakuna *limitation* wala *regulations*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na ongezeko la magonjwa kama vile kansa, kila leo yanaongezeka kila mahali hatujui chanzo ni nini. Mara ni mafuta tunayokula, naweza kusema pia hata utumiaji wa dawa usiokuwa na utaratibu, unaweza kuchangia matatizo na magonjwa mengine ambayo yanajitokeza kila siku. Tunaomba sana Serikali inapoandaa hili Baraza kwanza ihakikishe inaliwezesha vyta kutosha, wafanye kazi yao vizuri na pia ihakikishe *TFDA* inafanya kazi yao kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda Sehemu ya Pili, kile Kifungu cha 4(a), nakubaliana na wachangiaji waliopita kwamba suala la kutoa mafunzo, suala la elimu, suala la kuendeleza taaluma za Wafamasia liendelee kubaki kuwa ni jukumu la Serikali. Serikali ndiyo inaweza ikajua kabisa kwamba hapa tuna *gap* fulani tuweke hivi na sasa hivi inatambua kwamba hatuna Wafamasia, ni wachache, wenzangu wameshazungumzia. Nafahamu na nina *data* za kutosha, Serikali ihakikishe inawapeleka shule mapema iwezekanavyo na wale waliopo kwa sababu mambo yanabadilika kila siku, magonjwa yanabadilika, madawa yanakuja mengine, taaluma zao ziweze kuboreshwa ili waweze kwenda kwa wakati na kwa muda uliopo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni lile lililoko katika Sehemu ya Tatu, kwenye Kifungu kinachohusiana na *registration* ya hawa Wafamasia. Kwa hapo kwa kweli napenda Baraza lipewe meno ya kuhakikisha kwamba linachunguza kwa ndani vile vyeti vyta wale Wafamasia hata kule vinakotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye Kifungu cha 28(2)(a) wanazungumzia usajili wa hawa *Pharmaceutical Assistants* ambao watakuwa na *certificates*. Siku hizi kuna *certificates* feki nyingi, kuna vyuo vinavyotoa taaluma mbalimbali katika kila kona mitaani. Naomba sana kuwepo na *regulation* ya kuhakikisha kwamba kile cheti, Baraza lipewe *mandate* na mamlaka ya kufuatilia mpaka kule cheti kilikotoka vinginevyo wanawenza wakasajiliwa watu hapa kwenye hili Baraza ambao hawana *qualifications* kwa kuangalia tu cheti, wakawasajili, matokeo yake wakaja kutoa huduma kwa Watanzania

ambayo haistahili na mbaya zaidi kwa sababu inahusiana na afya inaathiri maisha ya Watanzania wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba sana Baraza hili litakapoundwa, Kanuni zianishe wazi ni kwa kiasi gani kutakuwa na utaratibu wa kuweza kupitia zile *pharmacy* mara kwa mara (*routine check up*). Wawe wanapitia mara kwa mara, siyo kwamba *pharmacy* iko kule Kaliua, kule mwishoni katika kijiji cha Panda Mleka basi hakuna anayeangalia wala kufuatilia kwamba kila ilipo *pharmacy* kwa sababu watakuwa na *list* na watakuwa na wataalamu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Aah, kengele ya pili!

WABUNGE FULANI: Ndiyo!

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nitumie fursa hii leo kwa sababu nachangia kwa mara yangu ya kwanza, niwashukuru wapiga kura na wananchi wote wa Jimbo la Buchosa bila kuisahau familia yangu, marafiki zangu na wote walionisaidia katika mchakato wa uchaguzi kuanzia katika kura za maoni hadi Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikishukuru pia Chama changu cha Mapinduzi na kuwapongeza sana kwa ushindi mnono walioupata, Mungu akibariki na awabariki sana wanachama wote. Ahsanteri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ulioletwa leo, kwa maoni yangu umechelewa. Taaluma hii ya Wafamasia ipo miaka mingi sana, nadhani ipo hata kabla ya taaluma ya Udaktari lakini kwa miaka mingi wameishi na ku-*practice* bila *regulation* wakiwa chini ya mamlaka zingine ambazo hazikuwa za kwao moja kwa moja. Kwa hivyo, niseme tu kwamba Muswada usicheleweshwe tena kama ilivyotokea huko nyuma bali tufanye utaratibu wa haraka upitishwe ili waanze kufanya kazi katika masharti na namna ambayo inakubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 4, maoni yangu, unajau Wafamasia wanahudumia binadamu moja kwa moja na huduma yao ni ya kutoa dawa tofauti sana na Mhandisi au mtu mwagine ambaye anamhudumia binadamu lakini siyo kwa kitu ambacho kinakwenda kwake moja kwa moja. Kwa hiyo, ushauri wangu wa kwanza ambao ningependa sana Muswada huu uliweke vizuri ili baadaye huko tusije tukapata *confusion* kama ambayo inatokea sasa hivi, suala la usajili wa maduka ya dawa lifanywe na Wafamasia wenyewe. Sasa hivi kilichopo, kila mtu mwenye fedha anawenza kwenda Bodi akapata usajili kwa *pre-test* kwamba ataajiri Mfamasia. Sasa Mfamasia anakuwepo

pale dukani kama muajiriwa na ile siyo mali yake kwa hivyo hata *chances za misconduct* zinakuwa kubwa zaidi kuliko kama duka lile lingekuwa limesajiliwa kwa jina lake mwenyewe na kwa maana kwamba yuko *responsible* nalo *one hundred percent*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano, ukitaka kusajili kampuni ya ujenzi kwa daraja fulani ni lazima mmoja wa *Directors* awe Mhandisi aliyesajiliwa na huyo anatajwa kabisa anakuwa *Technical Director* kwa maana kwamba atakuwa *responsible* na mambo yote ya kifundi ya kampuni yako. Sasa haya maduka yanjasajiliwa kwa *condition* tu kwamba mwenye mtaji atamuajiri Mfamasia. Mimi naomba hili jambo libadilishwe kabisa, iwekwe ndani ya sheria kwamba anayesajiliwa kufanya biashara ya dawa awe ni Mfamasia, sasa mwenye mtaji amtafute Mfamasia waungane wafanye hiyo biashara lakini Bodi au mamlaka nyingine yoyote iwe inamtambua yule *Pharmacists* kwamba ndiye *responsible* na duka na ni la kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, nani anawajua Wafamasia vizuri? Kwa mujibu wa Muswada huu, atakuwa ni Baraza la Wafamasia na kama Baraza la Wafamasia ndiyo litakuwa linawafahamu vizuri Wafamasia liachiwe hiyo kazi ya kuwapa hizo leseni za kufanya biashara ya dawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina ugomvi na *TFDA*, *TFDA* watabakiza *functions* za kuangalia huo ubora wa hizo dawa lakini *licencing* ya biashara ya dawa iachwe kwa *Council* kwa sababu ndiyo itakuwa inajua ubora wa hao Wafamasia na ndiyo itakayokuwa inasimamia *Code of Conduct* ya Wafamasia wenyewe. Ni vibaya sana kuwa-subject *Pharmacists* katika *dual loyalty*, wanajishauri wamtii zaidi nani, *TFDA* au *Pharmacy Council*? Tuwaache wawe *loyal* kwa *organization* moja ya Serikali. Napata tabu kuona kwamba *Council* siyo mkono wa Serikali, *Council* ni mkono wa Serikali, inakuwa *established* kwa *Act of Parliament* kama hivi tunavyotaka kufanya. Kwa hivyo, ufanyabiashara wa dawa uachwe kwa Wafamasia wenyewe na mtoaji wa hizo leseni awe yule anaye wa-register na anayejua *competency* yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ni suala hili la idadi ya Wafamasia, *Technicians* na hao *Auxiliaries* wao. Kwa muda mrefu sana walikuwa wako Muhimbili pale *Paramedical*, sina hakika kilichotokea ni nini, lakini *training* ikasimama na leo tunapata takwimu kwamba katika nchi yenye *Pharmacist Technicians* 700, *registered* wako 300. Hiki ni kinyume kweli kweli, tungetegemea kila *pharmacist* mmoja anakuwa assisted na *technicians* kama 10 au 15. Sasa kinatokea kinyume kwamba *Pharmacists* ni wengi kuliko *Technicians* wao, kwa hivyo *Pharmacists* wanawa-assist *Technicians*. Niombi sana Wizara ivifufue hivi vyuo vilivyokuwa vinafundisha *technicians* katika fani hii ya *Pharmacy*. Wako Muhimbili, Bugando lakini upo uwezekano pia wa kuwa-train katika vyuo vingine vinavyofundisha mambo haya ya *medicine*. Kwa kweli tukiacha hivi, hilo alilokuwa akilisema Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ndiyo linapata nafasi zaidi kwa sababu tunakuwa na maduka ya dawa huko vijijini, jambo ambalo hatuwezi ku-avoid ni lazima yawepo, hizo *ADO* mwendo wake ni mrefu hazitakamilika katika vijiji vyetu ndani ya miaka miwili au mitatu labda itachukua hata miaka mitano na nani watafanyakazi huko kama hawa watu wa kada hiyo ya kati hawapati mafunzo na wakawa manufactured wa kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana tuweke mkakati kama utawekwa na *Pharmacy Council* au na Wizara ya Afya yenyewe wa *ku-train more Pharmaceutical Technicians* wengi zaidi kuliko idadi ya *Pharmacists* ambayo inazalishwa sasa hivi. Namna hiyo ndiyo hata usimamizi wa dawa utakuwa *effective* kwa sababu wao wana taaluma siyo kubwa sana kwa *level* ya *degree* lakini angalau *ABC* za dawa wanazifahamu. Sijawahi kuona *Engineer* mjenzi ana-exist bila *Civil Technician* lakini *it is very sad* kwamba *Pharmacists* wana-exist bila *Technicians* wao. Niombe sana Wizara ilichukulie kwa namna ya pekee suala hili ili hata hii sheria inapotungwa basi iweze kutekelezeka vinginevyo tutakuwa tunatunga sheria ambayo utekelezaji wake utakuwa hauwezekani ndiyo maana *TFDA* wamekwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia Muswada huu wa Famasia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nichukue fursa hii kupongeza wale wote waliowasilisha hoja zao kwa upande wa Serikali, Kambi ya Upinzani na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii. Kabla ya kuchangia, napenda vilevile niwakumbuke wananchi wangu wa Manyovu na kuwaambia kwamba Obama yuko kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda *ku-declare interest* kwamba nilikuwepo kwenye Kamati hii ambayo imewasilisha Muswada huu, ni mmoja wa Wajumbe. Kwa kweli Muswada huu nasi tumeupitia kwa kina, nasi ulitusumbua kama unavyosumbua wajumbe wengine. Tumejaribu kuita watu wa vikundi mbalimbali ili nasi waweze kutupa ufahamu zaidi, tumeendelea vilevile kuwaita hata hawa *TFDA* ambao tunawasema, tumekaa nao zaidi ya mara mbili, mara tatu ili nao waweze kutupa wanavyoathiriwa na huu Muswada. Kwa ujumla wao Waheshimiwa Wabunge, naweza kuwaambia kwamba *TFDA* wako *comfortable* na *Bill* hii, hawana shida kabisa. Mimi mwenyewe nilikuwa na wasiwasi kwenye Kamati pale nilikuwa nawasumbua kweli kweli lakini wakanihakikishia kwamba wako *comfortable* na wamejadili katika *level* ya Wizara mambo yako vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwamba kwa kweli imeweza kuona kilio cha Watanzania. Kwa sisi ambao tuko Mikoa ya pembezoni kutoka Kigoma mpaka Dar es Salaam ni kilomita 1620 na wataalam wako Dar es Salaam ina maana Kigoma tunapewa dawa ambazo huenda ni feki. Sasa napenda niamini kuwa kwa kuwa na hii Baraza hili na sisi kule wataweza kufika sasa ili wananchi wetu waweze kupata dawa ambazo zina ubora ambapo na wao wakinywa mara moja kulingana na ile dozi basi waweze kupona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuundwa kwa Baraza hili kunatoa fursa na napenda niseme kwamba ninaunga mkono lakini pia niseme kwamba kama tulivyoanisha kwenye majadiliano, ubora wa dawa na chakula unabakia chini ya *TFDA* kwamba *importation* zote zinapoingia nchini ni kazi ya *TFDA* *ku-check* na kuona kwamba hizi dawa ni bora na

zinafaa zitumike nchini. Kama kuna viwanda *local ambavyo* vinazalisha madawa vilevile TFDA atahakikisha kwamba ubora ni ule unaotakiwa. Sasa *Pharmacy* wanaingia kutoa *permit* kwa wale amba wanataka kusambaza na kuuza dawa. Pale wanataka kujua kwamba hizi dawa ndiyo zenyewe lakini pia *premises* au yale maduka wanayofanya biashara yana ubora unaofaa. Kama mwenzetu mmoja alivyochangia, tunayo maduka ya dawa ambayo yanakuwa na joto sana. Kwa hiyo, Wafamasia watakapopita pale wataweza kuona kama hili duka linafaa kuwa kituo cha kutolea dawa au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza litaendelea kuwa na changamoto. Watumishi wa kutoa hizi dawa hawako wa kutosha kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema. Ni changamoto na kama wameamua kuichukua basi wachukue changamoto kwamba sasa hatutaki maduka ya dawa yapungue na hasa katika *level* zetu za vijiji. Vijiji vyetu viko mbali na maduka ya dawa angalau yawepo karibu na hili Baraza liweze kupeleka wataalamu na kama limeamua kuchukua hili jukumu basi lihakikishe kwamba linapeleka watu amba ni *qualified*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye Muswada huu, kuna sehemu yametajwa mambo ya *penalty* kwamba utaadhibiwa miaka miwili kama umefanya nini na nini. Nashauri Baraza litoe leseni za muda mrefu na muda mfupi kwa wale amba wamewa-*train* kama wale wa kwenye maduka ya *ADO* nayo itasaidia sana kuweza kuponyesha watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Muswada imeonesha kwamba *Chairman* wa Baraza atakuwa ni *private*. Sisi tuliuliza lakini wakatuhakikishia kwamba ni lazima kwa sababu Mabaraza mengi ambayo ni ya Serikali, *Chairman* wake ni vizuri awe mtu binafsi na hapo tukaridhika na mchana huu tumeendelea kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba ndivyo ilivyo na ye ye akatuhakikishia kwamba inapendeza ikiwa hivyo na ni sera ya *partnership*, kwa hiyo bado ni sera nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taaluma, tunao Wabunge wengine amba wamekuwa na wasiwasi kwamba *it-deal* na taaluma. Nasi tuliuliza hilo lakini taaluma waliyoisema ni taaluma ya Famasia kwa maana ya kuhakikisha kwamba ye yote yule anaye-*practice* ana ile *qualification* ya Famasia, hata kama ni kushauri, hizi elimu za juu wanawenza wakashauri kulingana na mitaala na taaluma yoyote ambayo inaweza ikabadilika kulingana na mazingira. Ni kama vile Bodi ya Uhasibu inavyotoa cheti kwa Wahasibu wake kwamba nenda ukapate ajira, kwa hiyo hata hii nayo kwenye taaluma zao ni vizuri waweze kucheki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama mmoja wa wajumbe wa Kamati, kile kipengele cha 4 ambacho watu wanasema kwamba famasia isijihusise na biashara, ukiiangalia haraka haraka, kwa kweli ilitakiwa isifanye ile kazi, lakini sasa Famasia vimebebana sana na biashara na hali halisi ya nchi yetu Mfamasia huyo huyo ndiye anatoa dawa, sasa ni vizuri adhibiti dawa. Tumetolea mfano ma-*Engineers* lakini *functions* zake haziko *attached* sana kama Famasia. Kwa hiyo, naomba nishawishi Wabunge wenzangu kwamba kwa kweli baada ya kuwa tumeupitia, inatushawishi kwamba hii *Pharmacy Council* na kama ilivyordhiwa vilevile na Baraza la Mawaziri na

Wajumbe wa Kamati hii, kwa kweli tuipe baraka, tuipe meno, ifanye kazi yake vizuri na ifanye kazi yake kama itakavyokuwa imedhamiria. Waziri amesema ataleta *amendments* za *TFDA* zile *functions* zote ambazo zinatoka *TFDA* basi ni vizuri nazo waweze kuzifanyia kazi haraka tuweze kuzifanyia *amendment*, ili ule mgongano kwenye soko usiweze kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba ni-*declare* kwamba naunga mkono hoja, nawashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Albert Obama. Waheshimiwa Wabunge, huyu ni Obama, Mbunge wa Manyovu. Nilisema atafuatia Mheshimiwa John Mnyika halafu atafuatia Mheshimiwa Anastazia Wambura.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mjadala wa Muswada huu muhimu ambao unagusa maslahi ya Watanzania wote kwa ujumla wake wakiwemo wa Jimbo ninalotoka, watumiaji wa dawa, wafanyabiashara wa sekta hii pamoja na wafanyakazi, wanataluma, Wafamasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia maeneo kadhaa kwenye Muswada huu. Eneo la kwanza, ni eneo linalohusu mamlaka ya uteuzi ya Waziri. Kwa mujibu wa Muswada huu, Waziri amepewa mamlaka ya kuteua Wajumbe wa Baraza, amepewa mamlaka ya kuteua Mwenyekiti wa Baraza, amepewa mamlaka ya kuteua Msajili, Naibu Msajili na nafasi nyingine mbalimbali ambazo zimetajwa kwenye sheria hii. Naona mamlaka haya aliyopewa Waziri ni makubwa sana. Ni muhimu kwa Waziri kupewa mamlaka ya kuteua Mwenyekiti, ni muhimu kwa Waziri kupewa mamlaka ya kuteua Wajumbe wa Baraza kwa ushirikiano na yale makundi mbalimbali lakini sioni ulazima kwa Waziri kupewa mamlaka ya kuteua Watendaji ambao kimsingi walipaswa kuteuliwa na chombo ambacho Waziri anakiunda ili kuweka mgawanyo wa kimamlaka na kiuwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza marekebisho yafanyike kwenye eneo hili ili kutenganisha majukumu yale ya kiusimamizi kwa maana ya *oversight* ambayo yanafanya na Baraza, Mwenyekiti na timu yake na majukumu ya kiutendaji kwa maana ya yale yanayofanya na Msajili, Naibu Msajili na Watendaji wengine. Nasema hivi kwa sababu kwa mujibu wa Muswada wenyewe, Kifungu cha 10 na 12, Waziri amepewa mamlaka ya kuliwajibisha Baraza hilo kwa sababu ukiangalia muundo mzima ni wa kwake yeche mwenyewe kwa maana ni wateule wa Waziri halafu yeche huyo huyo ndiye ana mamlaka ya kuwajibisha, naona hapa kuna mwengiliano sana wa kimamlaka ambao unaweza kusababisha ufanisi wa hili Baraza kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nimepitia nyongeza ya Muswada huu pamoja na marekebisho yake yaliyoletwa kwenye *schedule of amendment*, Wajumbe waliopendekezwa kwenye Sheria kuingia kwenye hili Baraza, nimeona kwamba kuna wadau wa msingi ambao binafsi naona ni muhimu sana wakawakilishwa. Kwa kufanya kazi ya kusimamia sekta ya ufamasia, Baraza hili litagusa vilevile wafanyakazi wa sekta ya umma, waajiriwa wa Serikali, watumishi wa Serikali ambao wanafanya kazi za

Ufamasia. Sasa katika mazingira kama haya, wafanyakazi nao wana haki zao na wana maslahi yao, wakiwemo wafanyakazi walionitura kutoka Jimbo la Ubungo ninalowakilisha, wangependa vilevile maslahi yao kulindwa katika kazi za hili Baraza. Kwa hiyo, naomba kupendekeza kwamba mionganoni mwa wale Wajumbe waliotajwa kwenye nyongeza ya huu Muswada pamoja na marekebisho yake aingizwe mwakilishi wa Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Afya ili basi Wafanyakazi nao katika kazi za hili Baraza maslahi yao yawewe kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba kuchangia kuhusiana na Kifungu cha 19 na 46 cha huu Muswada ambao uko mbele yetu. Hivi vifungu vyote viwili vinahusu masuala yanahusiana na utoaji wa adhabu, lakini ukisoma mathalani Kifungu 19(4) kinasema kwamba, “*The decision of the Council shall be final*” kwamba maamuzi ya hili Baraza yakishafanyika ndio maamuzi ya mwisho kabisa na maamuzi haya ni ya mwisho lakini yanaanza kwenye Baraza, mashtaka yake yanaanza kwenye Baraza ama malalamiko yake yaanza kwenye Baraza. Kitendo cha Baraza kuwa chenyewe ndio ambacho kinapelekewa mashtaka na kikiamua kwa mujibu wa sheria maamuzi yake yanakuwa ni ya mwisho, ni kinyume kabisa na Katiba ya Nchi na tukipitisha Kifungu hiki kama kilivyo kitakuwa kinakinzana na Katiba ambayo inatoa uhuru hata kwa mkosaji kuweza kukata rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kupendekeza kwamba kuwe na mfumo ambao utaruhusu uwepo wa fursa ya mtu ambaye amehukumiwa aweze kupata haki yake ya msingi ya kuweza kukata rufaa kama hakubaliani na hukumu ambayo imetolewa na Baraza. Kwa jinsi ilivyotajwa hapa maana yake ni kwamba inaingilia hata uhuru wa vyombo vingine. Mimi kwa tafsiri yangu naweza kusema kama unasema uamuzi huu ni wa mwisho maana yake hata Mahakama nayo ambayo ndiyo chombo cha juu katika Taifa letu cha kutoa haki inaweza ikapokonywa ama ikaminywa sehemu ya wajibu wake. Kwa sababu hiyo, napendekeza Kifungu hiki kirekebishwe ili kuruhusu uwepo wa mazingira ya kukata rufaa pale mtu anapohukumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia tena eneo linguine, nakubaliana na wajibu uliotajwa kwenye Sheria na Muswada huu wa kusimamia taaluma na viwango vilivyowekwa. Nakubaliana vilevile na tahadhari mbili ambazo zimetolewa na wachangiaji wengine na naomba niongezee kidogo tu. Tahadhari ya kwanza, umuhimu wa kutenganisha kati ya usimamizi wa biashara na usimamizi wa taaluma. Tahadhari hii ni ya msingi na naungana na wote ambao wameainisha vifungu ambavyo vinapelekea mwilingiano wa moja kwa moja kati ya kazi za Baraza za kusimamia taaluma ya famasia na kazi za Baraza za kusimamia biashara ya maduka na uuzaji wa madawa na mambo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, viwango vilivyowekwa hapa ni pamoja na viwango vinavyobeba sura ya kielimu. Tuna kada moja muhimu sana ambayo nashauri Baraza litakapofanya kazi yake lizingatie sana. Pamoja na kada ya *technicians* ambayo imetajwa, kwa kweli lazima tuendeleze kada ya *technicians* katika Taifa kama letu ambalo wasomi wa kada ya juu zaidi ni wachache katika masuala haya ya *dispensing* ya madawa lakini kuna kada ya Wauguzi Wasaidizi (*Assistant Medical Officers*) ambao

kimsingi ni wengi, lakini ukiangalia namna wanavyotambuliwa, wanawekwa pembezoni kidogo wakati ambapo hawa ni watu walio wengi sana katika mifumo yetu ya huduma za afya. Nashauri Baraza liangalie namna ya kuendeleza kada ya Wauguzi Wasaidizi (*Assistant Medical Officers*). Leo Tabibu Msaidizi pamoja na kuwa amesoma mwingine miaka mitano amesoma *Diploma*, amesoma *Advance Diploma* lakini akitaka kuijendeleza kufikia Udaktari kamili kwa maana ya *Medical Doctor* anarudi chuoni anasoma tena miaka mitano ya Udaktari kama mtu ambaye amemaliza Kidato cha Sita wakati huyu amesoma *Diploma*, amesoma *Advance Diploma*, ni lazima kuwe na mfumo mzuri zaidi wa kuitambua kada ya *Assistant Medical Officers* na ikasaidia kuziba hili pengo ambalo linaweza kujitokeza kama masharti haya ya viwango vya juu vya namna hii yakiwa ndio msingi wa utendaji kazi wa sekta nzima ya Ufamasia katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba kuchangia Kifungu kingine cha kwenye Muswada huu wa Sheria ulio mbele yetu, Kifungu cha 18 ambacho kinahusu utoaji wa usajili wa muda (*provisional registration*). Kifungu hiki kimetaja tu kwa ujumla kwamba kutatolewa huu usajili wa muda, lakini hakijaweka mipaka ya muda. Mtu akipewa usajili wa muda (*provisional registration*), usajili huu ni wa muda gani? Kwa hiyo, nashauri Kifungu hiki kiambatane na marekebisho ambayo yataweka mipaka ya usajili huo wa muda uwe walau miezi sita ili baada ya hapo taratibu zingine ziweze kufuatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kutoa rai, utungaji wa hii sheria ni jambo moja na ni jambo zuri kwa sababu inakwenda kuweka mifumo ya kusimamia sekta hii lakini usimamizi wa sheria na utawala wa sheria ni jambo lingine tofauti sana. Kwa hiyo, nitoe rai kwamba sheria hii iambatane na dhamira ya vitendo kweli ya kusimamia sheria hii ikiwemo kuhakikisha kwamba kanuni za sheria hii zinatungwa mapema kwa sababu zipo sheria zingine ambazo zimetungwa na Bunge hili Tukufu zikigusa sekta hii hii ya afya ambazo utekelezaji wake haujaanza ama haujafanyika kwa ukamilifu wake kwa sababu tu kanuni ambazo zinaambatana na sheria husika hazikuweza kutungwa kwa wakati. Kwa hiyo, nitoe rai kwa umuhimu wa sheria hii na kwa kuzingatia mazingira ya Taifa letu yalivyo hivi sasa ikiwemo na Jimbo ninalotoka la Ubungo kwa sekta hii ya ufamasia, maduka ya dawa, ni muhimu jambo hili likaharakishwa sana ili tija stahiki iweze kupatikana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimalizie kwa ile rai ya kwamba kuna umuhimu sana pamoja na kutunga sheria hii, Bunge hili Tukufu lisipokonye sana mamlaka ya Taasisi ya Chakula na Madawa kuhusiana na usimamizi wa kibashara na kuelekeza kwenye chombo hiki ambacho kinafanya usimamizi wa kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nakushukuru kwa mchango wako, kwa kuwa umeleta *schedule of amendment*, wakati utakapokaribia, kama kutakuwa na eneo ambalo ndilo unalisemea katika kipengele chochote, ukumbuke kusimama wakati huo vinginevyo hii peke yake haitoshi, lazima wakati huo pawe na hatua kama hiyo. Mheshimiwa Wambura atafuatiwa na Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuwa mmoja wa wachangiaji jioni hii ili niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu wa Sheria ya Famasi. Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote kuwepo mahali hapa siku ya leo, lakini vilevile nimshukuru kwa kuniwezesha kusimama na kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kwa dhati kabisa kwa sababu ni mara yangu ya kwanza katika Bunge hili kwa awamu ya pili kusimama na kuchangia hapa Bungeni, niwashukuru kwa dhati kabisa wapigakura wangu wa Mtwara pamoja na wananchi wote ambao wamekuwa wakiniunga mkono katika shughuli mbalimbali, lakini kwa namna ya pekee katika Uchaguzi Mkuu uliopita, wameniunga mkono vizuri sana na matokeo yake yamekuwa mazuri, nimeweza tena kurejea Bungeni kwa awamu ya pili. Nasema ahsante na Mwenyezi Mungu awabariki sana na kuwapa mafanikio katika maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda tena nichukue nafasi hii kuishukuru familia yangu, ndugu, jamaa na marafiki pamoja na watu wote wenye matashi mema, kwa kuniombea mara kwa mara, lakini pia na kuliombea Bunge. Wapo watu ambao huwa wanaliombea Bunge na wanaiombea nchi yetu amani nikiamini kwamba bila ya sala mambo hayawezi kwenda vizuri. Nawashukuru wote, napenda pia nitoe mwito waendelee kuomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina suala moja kabla sijachangia kwa sababu najua sina mengi sana nitakayozungumza, nitoe tu ufanuzi kuhusiana na majina matatu ambayo huwa yanawachanganya Waheshimiwa Wabunge wengi humu ndani, wanawachanganya pia wananchi kwa sababu huwa napata pongezi nyingi tu kutokana na michango ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa haya majina ni mimi mwenyewe Anastazia Wambura ambaye nimesimama hapa, mimi ni Wambura, yupo Felister Bura, huwa anakaa nyuma, kushoto, yule ni mwingine sio mimi, akichangia huwa napata pongezi. Akichangia pia Martha Umbulla, huwa napongezwa mimi na wananchi na Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, naomba tu ieleweke kwamba huwa yupo Anastazia Wambura, Felister Bura na huwa yupo Martha Umbulla, mmoja ni wa Dodoma, Martha Umbulla ni wa Manyara. Kwa hiyo, naomba kwa leo kama kuna pongezi basi nipewe mimi asipewe Martha lakini pia hata kama kuna marekebisho fulani fulani basi niambiwe mimi mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuyasema haya, sasa nianze kuchangia lakini kabla sijachangia, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza kwanza Waziri wa Afya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Timu yake nzima ya Wizara ya Afya, kwa kuweza kuleta Muswada huu ambao ni muhimu sana katika afya ya wanadamu, nadhani tutapiga hatua, tuko mbele lakini tutapiga hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze mchango wangu na nina mambo manne ambayo ningependa kuchangia na moja niliwahi kulizungumza, nilililetu mwaka 2006.

Niliuliza kwamba hivi ni kwa nini unakuta dawa inatibu ugonjwa mmoja labda ni aina moja, lakini utakuta dawa hiyo hiyo inauzwa kwa bei tofauti ni kwa nini? Nikajibowi kwamba ni kutokana na kwamba hizi dawa zinatoka nchi tofauti tofauti. Sasa nikijiuliza kwamba zinatoka nchi tofauti tofauti, wakati mwingine ukienda hospitali Daktari anakwambia kanunue *metakefin* ya Italy, anakuuliza wakati ule ultumia ya wapi, ya Kenya? Ndio, nilitumia ya Kenya, lakini safari hii katumie ya Italy, sasa napata wasiwasi kama kweli hizi dawa zinakuwa na ubora ule unaotakiwa, kwa sababu ni muda mfupi sana umetumia dawa hiyo hiyo halafu baada ya muda mfupi tena unarudi ukiwa hujapona. Sasa hili napenda sana sheria hii iliangular iweze kuli-*incorporate* pengine hata kwenye kanuni sababu ni suala la muhimu na la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna zile dawa za *typhoid (cipro)*, unakuta wakati mwingine Daktari anakwambia kanunue za UK, sasa kwa nini ununue za UK na si za mahali pengine? Kama hizo za nchi nyingine hazikidhi matakwa ya matibabu yale basi ni bora zikapigwa marufuku tukaelewa moja kwa moja. Hata *diclofanac* zimekuwa zikilalamikiwa sana, unakuta ziko ambazo zinazuwa kwa bei rahisi na nyingine za bei ya juu, ukiuliza kwa nini, wanakwambia hizi sijui za India, hizi za UK, ni kitu ambacho si kizuri sana, ni hatari. Nadhani hili ni suala ambalo inabidi tuliangular sana. Ndani ya hilo hilo utakuta kuna wengine sasa wanachukua hiyo hiyo ya bei rahisi wanai-*pack* upya wanaiuza kwa bei ya juu wanasema kwamba ni ya UK. Hilo nalo ningeomba lizingatiwe pengine kwenye kanuni au kwa namna yoyote ile Wizara ya Afya ilizingatie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Sehemu ya Pili, Kifungu cha 3(4) ambacho nimekisoma, utaona kwamba kinahusiana na *schedule* ambayo iko mwishoni mwishoni huko, kinasema kwamba “*the Minister may upon advice of the Council and by order published in the Gazette, amend, vary or replace all or any of the provisions of the Schedule to this Act*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kifungu hakina matatizo lakini kwa sababu *schedule* yenye iko huku nyuma na inaonyesha jinsi gani hii *council* itateuliwa na mambo mengine mengine. Nilikuwa nashauri labda, kihamie huku mwisho kiwe pengine kifungu cha 12, naona kinaweza kikaeleweka kwa urahisi. Mtu anaposoma ile *schedule* anakisoma na hiki kifungu moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine uelewa wangu ni mdogo, nilikuwa napenda tu nipaye ufanuzi katika Kifungu cha 4 hiyo hiyo *Part II*, Kifungu cha 4(d) kuna (ii) na (iii) vinanichanganya. Naona kama ni vitu *similar*, sasa sielewi tofauti yake ni nini. Kwa hiyo, wakati akifanya majumuisho Mheshimiwa Waziri, naomba nipaye ufanuzi kwa hayo masuala mawili. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapo hapo kuna suala lingine la tatu ambalo ningependa nichangie kulingana na hizi *functions* za hili Baraza ambazo ni kifungu cha 4. Kuna moja ambalo nasikia limezungumziwa sana na lipo hapa kwamba inabidi hawa Watalaam wa Famasi waelimishwe. Lakini kuna kitu kimoja ambacho naona tunakisahau; elimu kwa watumiaji wa dawa. Ni jambo moja la msingi kwa sababu nimekuwa nikishuhudia vifo vingi tu kutokana na *overdose* ya dawa mbalimbali. Kuna

tatizo kubwa la *overdose* na hata mimi mwenyewe nilishawahi kuponea chupuchupu miaka 24 iliyoipita. Niliandikiwa vibaya *Metacalphine*, kwa hiyo nilinusurika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wapo watu mpaka sasa wanapoteza maisha. Wakati mwengine anakunyuwa dawa fulani kwa ugonjwa ule ule, anakunyuwa tena dawa nyungine kwa ugonjwa ule ule. Wanaopoteza maisha ni wengi, lakini pia kuna tatizo la *under dose*. Sasa nilikuwa nashauri kwamba hapa kwenye wajibu huu wa hili Baraza, uwepo wajibu wa kuwaelimisha watumiaji wa dawa. Mara nyngi tunaona elimu hii kwa wananchi ya usalama barabarani, tunaona *first aid* wananchi wanaelimishwa, sasa Baraza hili lingepewa pia wajibu wa kutoa elimu ya matumizi ya dawa, pengine madhara yake na mambo kama hayo. Ni tatizo kubwa ambalo nadhani tukilichunguza vizuri tutaona lina athari kubwa sana, wakati mwengine linazaa na maradhi mengi tu; kuna watu wanapata mpaka na kansa ya maini kutokana na matumizi mabovu. Kuna Waheshimiwa wameshatangulia kusema lakini nadhani ni vizuri tukaliweka katika hiki Kifungu cha 4 kama wajibu wa *council*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nimalizie mchango wangu kwa kuiomba labda ni Wizara sijui au Baraza, lakini wakati wa uteuzi wa wajumbe wa *council*, uteuzi pia wa wajumbe wa kamati mbalimbali; *gender* naona kama haikuzungumziwa, kwa hiyo, wakumbuke *gender*. Wapo watalaam wazuri sana wa Famasi amba ni wanawake, kwa hiyo wakati wanafanya uteuzi waangalie pia na wanawake ili Kamati, *council* isije ikawa na wanaume watupu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi. Nasema asante kwa kunisikiliza. Asanteni sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Anastazia Wambura. Nilikuwa nimemwahidi Mchungaji Luckson Mwanjale, lakini nimwombe radhi kwa sababu ya mgawanyo wa muda na Muswada wenyewe jinsi mlivyochangia hapa, tutakavyoenda kwenye vifungu unaweza ukatuchukulia muda kidogo.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hiyo ya Muswada wa Famasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, si jambo la kupuuza kabisa kuacha kuwasimamia watoa huduma za dawa na vifaa viendavyo navyo. Hivi sasa baadhi yao wanajifanya madaktari amba wanao uwezo wa kumpa mtu dawa au kujinunulia bila ya kupimwa na kujulikana maradhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, fani ya *Pharmacy* ni muhimu sana, kwani bila ya kuisomea na kuijua vyema, watendaji wanaweza kuua mara moja. Zipo dawa zinazouwa *over the counter* kwa mfano, *asprin* lakini akipewa mwenye ugonjwa fulani anaweza kufariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya dawa huwezi kuzichanganya na kuliwa kwa pamoja, hivyo iwapo daktari kaandika kwa makosa na *pharmacist* yupo basi anaweza kuepusha balaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya kusimamia vyema dawa ya mifugo hivyo bodi inayohusika na uagizaji, usambazaji wa dawa hizo lazima wawe karibu na baraza hili la famasia na kusaidiana mawazo na *coordination*.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa dawa za kienyeji zinazotengenezwa *locally* na zile zinazoagizwa nchini zenye lengo la kuboresha urembo hayana budi sasa kufanyiwa utafiti na kujua ubora wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya kuweka bayana kazi za *TFDA* na hizi za Baraza la Famasia ili kuondoa mwingiliano wa majukumu. Baraza hili ni vyema wakaongezewa madaktari katika wajumbe wake kwani wao ndio wanao-*prescribe* hizo dawa.

Mheshimiwa Naibu spika, *composition of the council*, kupita kwa baraza hili isiwe ndio chanzo cha kupokea rushwa kwa wauza dawa za reja reja na ukiukwaji wa *ethics* za profession hii. Naamini *regulation* nzuri zitatungwa kwa haraka ili kusimamia utekelezaji mzuri wa shughuli za dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja na kuwa na baraza la kumlinda mlaji ili watumiaji wapate *forum* ya kupeleka malalamiko yao na mawazo pia. Naelewa upungufu mkubwa uliopo wa mafamasia na kada hizo ziendazo nazo, hivyo Wizara ianze sasa kuweka mikakati na kutekeleza kwa haraka ya kuongeza *intake* ya wanafunzi wa fani hiyo katika shule husika. Umuhimu wa kutoa elimu kwa umma ya kuwaeleza majukumu ya *Pharmacy Council*, *TFDA* na *TBS* ili wananchi waelewe wapi pa kupeleka kero zao.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa maduka ya dawa, pamekuwepo na uhaba mkubwa wa wafamasia nchini lakini tatizo hili linaweza kupungua kwa kiasi fulani kama Serikali ikikubali mfamasia mmoja kusimamia duka zaidi ya moja la dawa. Kwa mfano unakuta kuna mtaa wenyewe zaidi ya maduka matano na kila duka lina mfamasia na msaidizi. Je, ni kwa nini wasaidizi wasitumike na *pharmacist* wawili wakasimamia maduka yake? Hii ni kupoteza rasilimali watu ambayo inahitajika sana mahali pengine nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri wataalam wasimamie kazi yao na *TFDA* isimamie biashara na kufanya ukaguzi wa dawa kama vile dawa zisizokidhi viwango, kuna dawa nyingi na hata vipodozi vinaharibu kabisa sura za wanawake wengi na kuapelekea kupata magonjwa ya saratani (*cancer*) ya ngozi. Hivyo ni muhimu kazi hii ifanywe na *TFDA* kwa sababu kuna wataalam waliobobea katika kazi na walismeshwa

kwa ajili ya kazi hii. Nasisitiza kazi ya kudhibiti na kusimamia biashara ifanywe na *TFDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne inayohusiana na usajili wa maduka au sehemu za biashara na utoaji wa vibali kwa biashara ya dawa, je, hawa wataalam watafanyaje shughuli hii? Huu ni muingiliano wabaki na utaalam na *TFDA* wafanye kazi hii na wafamasia waendelee kudhibiti maadili ya taaluma za ufamasia na si vinginevyo.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Aidha, naomba kushauri kuwa Ukaguzi wa Maduka ya Famasi uwe unafanyika mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa shughuli hii inafanyika *in a professional way*.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada katika *objects and reasons* una lengo la “*to regulate the pharmacy profession at different levels*”. Hata hivyo, kwenye madhumuni na sababu (Swahili version) sheria inakusudia kuweka masharti ya kudhibiti na kusimamia taaluma na maadili ya Wafamasia katika utoaji wa huduma zinazohusu taaluma hiyo. Sababu za Muswada katika Kiswahili ni “*more elaborative*” kuliko Kiingereza lakini zote zinasisitiza “kudhibiti” na “kusimamia” taaluma. Hii maana yake ni kwamba sheria inakusudia “*market entry regulation*” na wala sio “*market conduct regulation*”. Inashangaza kwa nini Sheria ya *Food, Drugs and Cosmetics Act No. 1 of 2003* inafanyiwa marekebisho kwa kufuta kutoka kwayo Vifungu 26,27,47,48 and 74 ambavyo havihusiki na taaluma bali biashara (*market conduct*). Ni vema sheria inayotungwa isimamie taaluma tu na isihusike kusimamia soko kwani *TFDA* inatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Wafamasia likiusika katika kusimamia soko italeta matatizo makubwa sana kwani sheria hii itakayotungwa haitoi na haipaswi kutoa mamlaka ya leseni za dawa kwa Baraza (*mandate for drug licensing*). Vilevile halitasimamia viwanda vya madawa, soko la madawa (*pharmaceutical market*) linaanzia *manufacturing and trading*. Sheria inataka kudhibiti *trading* na kuacha *manufacturing* kwa *TFDA*.

Hii ni *opportunistic venture* ambayo *Pharmacy and Poisons Board Act, Cap 244 of laws of Kenya*, Bodi yao inaanzia usimamizi katika utengenezaji (*manufacturing*). Pamoja na kwamba Bodi ya Kenya inasimamia pia taaluma lakini sio sawa “ku-pick” maeneo. Kama tunataka *Kenyan way* ni vema tuchukue sekta nzima *pharmacy, manufacturing and trading otherwise* sheria yetu ibakie na kudhibiti na kusimamia taaluma tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *part IV* ya Sheria ya *TFDA* isifutwe na badala yake Muswada uondoe vipengele vyote vinavyohusu kusimamia biashara ya *pharmacy (business of pharmacy)*. Baraza la Wafamasia libakie na kazi ya kuendeleza, kudhibiti na kusimamia taaluma kwani changamoto za taaluma ni nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Ghana ina *Pharmacists* 2162 na hivyo kila *Pharmacist* mmoja kuhudumia watu 10,000 hapa Tanzania tuna *Pharmacists* 700 na kila Mfamasia anahudumia watu 50,000, Kenya ina Wafamasia 1342 na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina Wafamasia Wasaidizi 250 tu na *Technicians* 300 tu (taaluma ambayo inapotea toka nchi iache kusomesha raia kwenye taaluma hiyo). Zaidi ya yote 51% ya wanataluma wafamasia wanakimbia taaluma na kukimbilia sekta nyingine hali inayoathiri Taifa sana. Iwapo Baraza likijikita kwenye biashara pia, nguvu ya kusimamia taaluma itapotea na kujikuta biashara inapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho ni kutenganisha shughuli za biashara na taaluma kwa Baraza, lengo la Taifa liwe ni kuimarisha taaluma na biashara ibaki *TFDA* ambao wameshajenga uwezo wa kutosha na usoefu. Changamoto ya nchi hii sasa ni *Human Resources* katika taaluma na sio biashara.

MHE. AMINA A. CLEMENT: Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Famasia kwa Muswada huu ina madhumuni ya kulinda na kuendeleza taaluma ya Mfamasia hilo ni jambo la msingi sana. Lakini kazi ya kutoa vibali kama ilivyo katika Sura ya nne (4) kifungu cha 37 hususan 37(1)b nahisi sio sahihi kazi hii ifanywe na *TFDA* inayodhibiti ubora na usalama wa dawa, vifaa na vifaa tiba hasa ukizingatia mazingira yetu ambayo bado baadhi ya dawa ziko katika viwango vya chini zinazozalishwa hapa nchini pia zinazoingizwa nchini. Kifungu hiki naomba kiangaliwe upya na kifanyiwe marekebisho.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja ya kupitishwa Muswada wa Sheria ya Famasi ya Mwaka 2010 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu kama utafanyiwa kazi vizuri baada ya kupitishwa utatusaidia sana na hasa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, madawa yanauzwa mikononi Mkoani Dar es Salaam kama karanga. Dawa hizi hazijulikani zinakotoka na sijui kama mamlaka husika wanafahamu kama kuna madawa mengi yanauzwa mikononi katika mabaa, mahotel, mashuleneni na katika vituo vya mabasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madawa yanatibu lakini pia madawa yanaua kwa kuwa ni sumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa madawa yanaua basi wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam maisha yetu yako hatarini. Baada ya muda kuna hatari ya kutokea vifo vingi vinavyotokana na sumu ya madawa yasiyo na viwango yanayouzwa hovyo mitaani. Pamoja na kuuzwa hovyo mikononi kwa madawa pia kuna utitiri wa makampuni yanayotoa madawa yanayosema ni lishe, hazina sumu, zinatokana na miti na mimea ya asili. Kama ni kweli je, kuna mamlaka ambazo zimechunguza makampuni hayo na kuhakikisha madawa hayo ni salama?

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Kwanza, jukumu la kuhakiki na ukaguzi wa madawa ni kubwa, ningeomba jukumu la ukaguzi liachiwe *TFDA* lakini kiongezwe Kitengo Maalum cha Ukaguzi wa Madawa na Utaalam.

Pili, leseni za uuzaaji wa madawa ziangaliwe vizuri na hasa katika uuzaaji wa jumla, maduka ya madawa ya jumla yamekuwa mengi Kariakoo, sidhani kama wana wataalam wenye sifa.

Tatu, naipongeza *TFDA* na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya kwa kazi ngumu lakini wanajitahidi sana wanahitaji tuwaongezee nguvu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja Muswada upitishwe lakini uangalie ukubwa wa majukumu katika kitengo kimoja na kingine tusije tukapeleka mzigoto mkubwa pale pasipostahili.

MHE. ZARINA SHAMTE MADABIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja (Muswada) kwa sababu ni muhimu sana Serikali iweze kudhibiti taaluma ambayo ni muhimu sana ili kulinda afya ya wanadamu ambao mara zote ni wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona ni busara kabisa kufanya marekebisho yaliyofanywa ili kutotenganisha taaluma na huduma. Hivyo kwa maoni yangu binafsi, naunga mkono Muswada kama ulivyowasilishwa na Wizara.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Mswada huu “*The Pharmacy Act, 2010*” una matumaini makubwa sana kwa wananchi kwani unaondosha Mamlaka kutoka *Tanzania Food Drug Authority (TFDA)* na Mamlaka hayo kwenda kwa Baraza la Famasia (*Pharmacy Council*).

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji huu wa *Pharmacy Council* na Mamlaka yaliyoainishwa kwenye Muswada huu itakuwa ni kama vile Baraza hilo limepewamo ambayo yatasaidia sana, kutokana na majukumu mazito yaliyopewa Baraza hili endapo yatapita na kutekelezeka mambo yafuatayo yatapungua kwa kiasi kikubwa:-

Kwanza, Baraza kwa kuzingatia *procedures* zote za *application permit* itasaidia sana kuondoa maduka ya dawa baridi za binadamu ambayo yapo mengi na hayakidhi viwango. Hii ni hatari sana kwa wananchi kwani dawa ni sumu kama hazihifadhiwi inavyotakiwa na kutumika kwa usahihi.

Pili, kwa kuwa Muswada huu unaanzisha na umeboresha zaidi nguvu ya Baraza, endapo utapita na kuanza kutumika, itapunguza sana ama kuondoa kabisa wafamasia wasiofaa ili kuokoa afya za wananchi.

Tatu, ili kuweka majukumu vizuri zaidi kwa *TFDA* na Baraza la Famasi, yale ambayo yamependekezwa na Kambi ya Upinzani ni muhimu sana, nami nayaunga mkono yafanyiwe kazi kabla ya Muswada huu kuwa Sheria kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu, kinachoonekana ni kuwepo kwa vyombo vingi. Kifungu cha 7(1) kinasema, kuna Bodi ya Famasia, Kamati ya Famasia, Kamati ya Adhabu na pia kuna Sekretarieti ambayo ipo katika kifungu cha (13).

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha (8) kinaeleza kwamba, bado Bodi ya Famasia ina uwezo wa kuunda Kamati nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa vyombo vingi katika Muswada huu na hatimaye kuwa Sheria, vitasababisha mwingiliano wa kazi baina ya Kamati mbalimbali. Kamati hizo hazikuwekewa muda wa kukutana. Hali hiyo itasababisha utendaji uwe kwa matakwa ya Watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni kubwa na Msajili (*Registrar*) ni mmoja. Sijaona kama kutakuwa na Msajili kutoka kwenye kila Kanda; ukosefu huo unaweza kusababisha utendaji usioridhisha na hatimaye kuweka mazingira ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani ipo haja ya kuwa na Wasajili Wasaidizi kwa Kanda angalau nne ili usajili ufanyike kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la maduka ya madawa kufanya matibabu badala ya kuuza dawa kwa mujibu wa maelekezo ya daktari, matokeo yake kwa sababu maduka hayo lengo lao ni kuuza dawa, siyo ajabu mtu anapokwenda kutaka dawa bila ya maelekezo ya daktari, mgongwa huyo hupewa dawa nyingi. Kuwepo na Mkakati Maalum wa kuwataka wafamasia wasitoe tiba bali wauze dawa. Ahsante. Kwa heshima na taadhima nawasilisha na kwa dhati naunga mkono hoja hii.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu umekuwepo mtindo wa wenyе baa na migahawa nchini kutumia sabuni ya unga (*detergent*) kunawisha wateja kabla na baada ya kula. Ingawa sijafanya utafiti wa kisayansi, uchunguzi niliofanya kwa kuzungumza na wataalam, unaonyesha kuwa matumizi ya sabuni hiyo ambayo ni vigumu kuimaliza kwenye ngozi kwa kuosha kwa maji kwa haraka, huweza kuwa na madhara ya magonjwa ya ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa naishi Ungereza, tulishauriwa kutotumia sabuni ya unga kufua kwa mikono sababu kubwa ni hiyo kuwa sabuni hiyo ilitengenezwa mahsusit itumike kufulia kwa kutumia mashine na kuwa mikono haina uwezo wa kuimaliza kwenye nguo. Mabaki ya sabuni hiyo kwenye nguo huyeyuka mvaaji anapotokwa jasho na kushambulia ngozi. Kwa mantiki ya maelezo hayo, nashauri kuwa

Serikali ipige marufuku matumizi ya sabuni za unga kunawisha wateja kwenye baa na migahawa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea kujibu hoja za Wabunge, ningependa tu nitoe ufanuzi mfupi tu kidogo kwamba *The Pharmacy Council* (Baraza la Wafamasia) maana yake ni nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Wafamasia wajibu wao mkubwa katika Muswada huu ni kuhakikisha kwamba wanalinda na kusimamia *professional* (taaluma) ya Kifamasia pamoja na utendaji (*Pharmacy Practice*). Sasa inapokuja kwenye kile kifungu ambacho anaona kimeleta utata mkubwa ndiyo sababu nimeona kwamba nizungumzie kwa sababu muda ni mfupi, ni kwamba kazi ya *Pharmacy Council* pale ni kupata makarasi ya maombi, kwenye karatasi ya maombi ya mtu anayetaka kufanya biashara ya Famasia, ya kuuza dawa, tunataka tuone kwamba anakuwa ni mtu mwenye utalaam ili tuweze kudhibiti uingizaji wa dawa ambazo hazina kiwango, dawa *fake* na dawa zingine ambazo zinaharibu afya za watoto wetu na dawa za kulevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kwa sasa hivi unakuta kwamba mtu yejote anaamka anataka kufanya biashara ya kuuza dawa, na wamejitokeza wengi, anakwenda kutafuta cheti mahali, anakiweka, halafu anapata kibali cha kuanza kuagiza dawa. Hakuna *Professional Pharmacist* ambaye amefanya Mtihani wa *Forensic* wa kuhakikisha kwamba anajua tofauti ya dawa na tahadhari za dawa ili aweze kuhakikisha kwamba yule anayeagiza dawa haagizi dawa ambazo hazikubaliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hapa basi, kutoa kibali maana yake ni kwamba Baraza hili liangalie kwamba kuna watalaan ambao wana kiwango, ambao wamekidhi kiwango ambacho kimetolewa na Baraza la Wafamasia, ambao watasaidia *ku-check list* ya dawa kabla haijaagizwa. Wakiridhika, watampa kibali. Akipata kibali huyu mtu kwa sababu anataka kufanya biashara, atakwenda kwenye Halmashauri husika akaombe leseni ya biashara, atapata leseni ya biashara. Lakini kabla ya yote hayo atakuwa ameji-*register* na *BRELA* ili aweze kujulikana kwamba hiyo kampuni yake inaitwaje.

Kwa hiyo, kuna mamlaka kama tatu hapo. Lakini, mamlaka inayoangalia kwamba huyu mtu kweli ana uwezo na anajua kwamba dawa ni kitu gani atakayehakikisha ni *Pharmacy Council*. Sasa *TFDA* inaingiaje hapa; *TFDA* inaingia pale ambapo sasa huyu bwana anaagiza dawa, anapoagiza zile dawa ataomba kibali *TFDA*, atapeleka *list* ya dawa ambayo imetayarishwa na Mfamasia wake ambaye amethibitishwa na Baraza la Wafamasia na atasema zile dawa zinaingilia wapi, zitakapokuja, *TFDA* watakwenda kuchukua *sample*, watakwenda kuipima. Baada ya pale, ni jukumu la *TFDA* pia hizi dawa zinapokwenda sokoni wafuatilie kwamba kweli zile dawa ambazo wamezipima kwenye *warehouse*, kwenye *point of entry* ndizo ambazo zinasambazwa kwa walaji, ubora wake upo. Kwa hiyo, watakuwa wanatumia maabara na utalaam wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti ndiyo hiyo kwamba mmoja ataangalia taaluma, atoe *permit*, mwagine ata-*check product* inayoingia na inayosambazwa kwa walaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba sasa nijibu hoja za Kambi ya Upinzani. Ndugu zetu wa Upinzani nashukuru kwamba wamechangia, wamezungumza, mimi naamini yale waliyozungumza mengine ni kwa nia ya kuboresha. Wanataka kujua ni nani Mfamasia. Kwa Muswada huu, Mfamasia ni mtalaam ambaye amesoma akamaliza *degree* inayotambulikana na *TCU*. Lakini pia akafanya na *internship* ya mwaka mmoja na akaja akafanya mtihani wa *forensic*. Mtihani wa *forensic* tunajaribu kumwangalia kwamba ujuzi alionao, ana ufahamu wa kutambua kwamba ni dawa ipi ambayo ni sumu, ni dawa ipi ambayo haitumiki hapa, haitumiki pale, ndiyo sasa anakuwa-*registered* na *council* ya Wafamasia. Huyo ndiye Mfamasia au kwa Kiingereza tunasema *Pharmacist*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema kwamba Sera ya Dawa ilihimiza kuwepo kwa maduka ya dawa ili kusogeza huduma na kurahisisha upatikanaji wa dawa. Kwa nini chombo kiwe pia chombo cha kusimamia biashara? Nimezungumzia hapo kwamba hawasimamii biashara, hawatoi leseni za biashara, wanatoa kibali cha wewe kuruhusiwa kupewa leseni ya kwenda kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wametoa angalizo katika Sheria ya *Nurses and Midwives Registration, 1997* kuhusu mitihani ya wanataluma ya Uugazi. Mimi ningependa kusema kwamba hii Sheria ya *Nurses* ya mwaka 1997 inafanyiwa marekebisho, lakini pia haina mahusiano na sisi kuzungumzia Wafamasia. Lakini naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba hii sheria inafanyiwa marekebisho sasa hivi ili kukidhi muundo mpya wa Mpango wa Afya ya Msingi wa kuwa na wanataluma wa kutosha kwenye Taaluma ya *U-Nurse*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wameuliza pia, kwa nini Baraza lisimamie viwango vya mafunzo? Naomba kusema kwamba huwezi kusimamia taaluma kama hutasi mamia namna au kiwango cha wale ambao wanakuja kuwa ndiyo wanataluma. Mchango wao ni kwamba mtu anayetaka kuanzisha Chuo cha Ufamasia anaomba kwanza kupata kibali kupitia kwenye Baraza la Famasia, wanaangalia kwamba ana watalaan wangapi, *premises* ambazo zinahitajika, ana maabara, ana *technicians* wa kutosha, ana watalaan wa kutosha. Wakishakubali kwamba anakidhi hivyo vyote, ndipo wanampa kibali sasa, anakwenda kupata usajili *NACTE* na *NACTE* ndiyo ambayo inamruhusu aweze kutoa mitihani na baada ya huo mtihani wao ambao wanafanya, lakini wanaangalia na *curriculum*, wanaangalia na vitabu kama viro na ikiwezekana wanakwenda kuangalia pia kama kuna *library* ambayo ina vitabu ambavyo vitawasaidia wale wanafunzi wapate elimu ya kitaaluma ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wameuliza pia ukomo wa madaraka ya Kamati. Bahati mbaya hawakusema ni kamati ipi, ila ni kwamba kamati zote, madaraka ya kamati ni kweli yanatakiwa kuwa na ukomo. Madaraka haya yataainishwa kwenye kanuni pamoja na sifa zao. Mimi naomba kusema kwamba kamati zote ambazo zimeingia kwenye huu Muswada, tutaainisha uhai wao kutoptana na kanuni za utekelezaji wa hii sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ameuliza kwamba hivi Baraza hili la Watalaan watakuwa wamebobea kwenye masuala ya fedha? Ni kwamba mahali popote ambako kutakuwa na masuala ya fedha ni lazima watalaan wa fedha wataajiriwa kuweza kufanya kazi katika hiyo *council*. Wao hawana utalaam, ila wataajiri, ndiyo sababu hata wanataaluma wengine wanaajiri pia watalaan wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, anauliza je, katika Sekretarieti hiyo, jinsia itazingatiwa? Naomba kusema kwamba ninawashukuru, huo ushauri nimeuchukua na jinsia itazingatiwa katika *composition*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kuna haja ya kujandikisha mara ya pili kwa kutoa ada za mtihani? Naomba kusema kwamba, *Professional Boards* zote ulimwenguni ni kwamba wewe ukimaliza kusoma, unakwenda kufanyiwa tena mtihani wa kuhakikisha kwamba yale maadili ya kazi yako unayaelewa, ndiyo sababu nimesema kwamba zaidi hapa kwenye Baraza la Wafamasia watakupa mtihani unaoitwa *Forensic Examinations* kuangalia kwamba wewe unafahamu maadili yako, unafahamu mipaka ya kazi yako na unafahamu namna ambavyo utawajibika katika utendaji wako wa kazi kama utakosea. Kwa sababu mtu asiye na ufahamu wa namna hiyo, hawezi kuwa anafanya kazi kufuatana na maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, anauliza *internship* ni muda gani? Nafikiri, tutakapofanya mareklebishi kwenye jedwali, ni kwamba *internship* itafanyika kwa muda wa miaka miwili ili kuhakikisha kwamba wanapitia vitengo vyote ambavyo Mfamasia anatakiwa kuvijua katika hospitali, katika *manufacturing* na katika kuangalia kwenye maduka ya *wholesale*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichangie kidogo kuhusu wale ambao wamechangia kwa kuzungumza. Amechangia Mheshimiwa Augustino Mrema, ambaye amekubali kwamba sheria itaboresha utendaji wa huduma za dawa ili kuondokana na watalaan Wafamasia bandia. Aidha, sheria itawezesha kupatikana watalaan wenye sifa na ujuzi unaokidhi viwango na baada ya hapo, akaunga mkono hoja. (*Makofi*)

Naomba nishukuru kwamba ushauri wake tutazingatia na nina hakika kwamba hii sheria kweli itakwenda kuboresha kiwango cha utendaji katika kutoa dawa kwa wagonjwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa David Kafulila pamoja na Mheshimiwa Dkt. Kebwe Kebwe, wamezungumzia majukumu ya *TFDA* na Baraza. Naomba niseme kwamba majukumu ya Baraza na *TFDA* tutayaanisha kwenye kuandika kanuni za utekelezaji wa hii sheria, tutaweka mipaka ya Baraza, tutaweka na mipaka ya *TFDA*. Lakini naomba niseme Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba huwezi ukawatenganisha kabisa hawa watu wawili, kwa sababu pale ambapo Mfamasia anagundua kwamba kuna tatizo mahali, ni lazima amwambie *TFDA* nenda kachukue tena *sample* mara ya pili pale. Pale ambapo *TFDA* itagundua kwamba kuna tatizo, atakwenda kumpa taarifa Mfamasia, tunaomba uchukue hatua ya kumnyang'anya yule leseni, kwa sababu amekiuka maadili yake ya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Leticia Nyerere, amezungumzia uteuzi wa Wajumbe wa Baraza na akasisitiza kwamba jinsia izingatiwe. Naomba kusema kwamba ushauri tumeuchukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid Seif, alishauri kwamba *TFDA* isimamie ubora na usalama wa dawa, uzalishaji na usambazaji wa dawa, Baraza lisimamie matumizi na utunzaji na utoaji wa dawa.

Mimi naomba kusema kwamba kwa hili la *TFDA*, Wizara imepokea ushauri na itauzingatia wakati wa kuandaa kanuni ili kutenganisha majukumu ya *TFDA* pamoja na majukumu ya Baraza. Lakini la muhimu ni kusema kwamba wote hawa *TFDA* na *council* ni vyombo au ni mamlaka ambazo ziko chini ya Wizara na Wizara ndiyo itakuwa inawaratibu. Lakini, naamini kwamba wote wapo kwa ajili ya kulinda usalama wa Watanzania, lakini ushirikiano utakuwepo na mipaka yao ya kazi itakuwepo na pale ambapo tunaona kwamba kunaleta matatizo, tutakuwa tayari kudurusu hii sheria ili tuweze kufikia kile kiwango cha kutoa huduma ya dawa kwa Watanzania, tupunguze uwepo wa dawa *fake* na dawa zingine ambazo ni hatari kwa matumizi ya binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe masahihisho kidogo, ni kwamba Sheria ya *Nurses* imefutwa na Sheria Mpya ya mwaka 2010 ya Uugazi na Ukunga ambayo inaangalia taaluma ya Uugazi na Ukunga kwa ujumla ikiwemo na sehemu wanayofanyia kazi (*maternity homes*) inatengenezwa. Waheshimiwa Wabunge, hii Sheria ya *Nurses and Midwives* itakapomalizwa kufanyiwa *review*, nafikiri na ninyi mtapata taarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba tatizo lililokuwepo mwanzoni ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa wamepata *signal* kwamba Baraza litakuwa linanunua dawa na linafanya biashara. Hapana! Baraza litakuwepo tu kuangalia ubora na kuangalia *professionalism* pamoja na *practice*, ndiyo sababu wao watatakiwa kukagua cv na vyeti kwa ajili ya watu ambao wanataka kufanya biashara ya famasi. Baada ya kukagua wakaridhika, watawapa *permit*, wakishawapa *permit* watakwendwa kupata leseni. Ukagazi wa *premises* zao pamoja na *product* watakayokuwa nayo itakuwa inafanyiwa kazi na *TFDA* ndiyo sababu Waheshimiwa Wabunge, naomba mtupe fursa ya kuweza kwenda kukaa chini na hawa watalaan wote kwa sababu wote ni watoto wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tuandike kanuni, tuwekeane mipaka. Kama kutakuwepo na *conflict* ya utekelezaji kwenye *operation*, sisi tutakuwa wa kwanza kurudi katika Bunge hili tukufu kuja kufanya marekebisho (*Miscellaneous Amendment*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naamini kwamba hatutakuwa na sababu ya kurudi kwa sababu kanuni zetu zitahakikisha kwamba kila mmoja anajua wajibu wake, hakuna mwingilio. Pale ambapo kutahitajika na ushirikiano ambao naamini kwamba ni lazima uwepo kwa sababu kutoka kwenye *council* na kutoka kwenye *TFDA* kwenye

ngazi ya Taifa kwenda kwenye Mikoa na kwenye Wilaya tutatumia Wafamasia ambao watakuwa wamekuwa ni *registered* na Baraza la Wafamasia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tena kwamba hawa wote wawili ni watoto Sheria hii inalenga kuboresha ubora wa dawa na kupunguza usambazi wa dawa feki pamoja na kupunguza usambazaji wa dawa ambayo hayakubaliki kama yale ambayo mmezungumzia yanayoharibu maumbo ya binadamu. Haya yote yanaingia kwa sababu wengine wanafanya biashara wanaingiza kwa sababu wanataka pesa sio kwa sababu wanataka kuhudumia afya. Kwa hiyo, Baraza litacheki haya na hii ndiyo tunasema kwamba ni *check and balance*. Nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Mwanzoni nilisema dakika ishirini lakini hazitakutosha jitahidi angalau nusu saa. Tunakuongeza kidogo. (*Makofi*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja yangu. Umenipa muda wa kutosha lakini napenda nikiri mengi ambayo nilipanga kuzungumza ameyaelezea Naibu Waziri kwa hiyo, nafikiri haitakuwa busara kurudia haya. Kwa hiyo, nitasisitiza yale mambo muhimu katika hoja yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu na Wabunge waliochangia kwa maandishi wote nawashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge 19 walichangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge kama ifuatavyo; Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Mbunge na Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge na Makamu Mwenyekiti wa Kamati wa Huduma za Jamii, Mheshimiwa Pauline Gekul, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Dkt. Kebwe Kebwe, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Dkt. Seif Suleiman Rashid, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Said Suleiman Said, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa Albert Obama, Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Anastazia Wambura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile waliochangia kwa kutoa maandishi ni Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Amina Clement, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Dkt. Abdulla Juma Saadalla, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye na Mheshimiwa Aliko Kibona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao ambayo wameitoa michango hiyo iliyotolewa nitatolea ufanuzi ,

lakini naomba nianze kutoa ufanuzi wa hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii ambao walitoa hoja uboreshaji wa Kifungu cha 37(1)(b) ili jukumu la utoaji wa leseni za uagizaji wa jumla na utengenezaji wa dawa libaki kuwa jukumu la *TFDA*.

Maoni yote ya Kamati yamefanyiwa kazi katika hati ya marekebisho yaani *Schedule of Amendments*. Kwa mujibu wa hati ya marekebisho Serikali imeshazifanyia kazi maoni ya Kamati kwa kuwaagiza na watengenezaji kubaki kusimamiwa na *TFDA*. Baraza litasimamia wale wanaonunua dawa kwa jumla kutoka kwa waagizaji na kuziwa kwenye maduka ya rejareja. Hii ni kutokana na wateja wa dawa katika maeneo ya katika maeneo haya ni wagonjwa na hivyo kutoa nafasi kwa Baraza kusimamia maadili ya kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo haya napenda kutoa ufanuzi katika maeneo yafuatayo; suala la uagizaji na utengenezaji wa dawa na vifaa vyta tiba unaendelea kusimamiwa na *TFDA* kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi sura namba 219. Naibu Waziri alilagusia na mimi naomba nirudie tena hili ndilo linawachanganya Watanzania kwamba suala la uagizaji na utengenezaji hii ndiyo *entry point* ya dawa. Kwa hiyo, suala hili litaendelea kusimamiwa na *TFDA* kwa mujibu wa Sheria za Chakula. Hapa tunataka kuangalia ubora na usalama wa zile dawa. Serikali itaendelea kusimamia uwezo wa *TFDA* kutekeleza majukumu yake kulingana na mahitaji na wakati utakaposibu. (*Makofii*)

Kuhusu kuongeza idadi ya Wajumbe wa Baraza Serikali haini athari kuendelea na Wajumbe waliopendekezwa katika Muswada huu. Aidha, idadi hii ya Wajumbe itapunguza gharama za uendeshaji, vigezo vyta kuwateua na kuwapata Wajumbe wa Baraza vitaainishwa katika Kanuni. Baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walizungumzia hoja hii na mamlaka aliyopewa Waziri ni vigezo gani vitatumika na kuteua na kuwapata hawa Wajumbe wa Baraza. Hili tutalitolea maelezo ya kutosha na itaainishwa katika Kanuni ambazo tunesema mara tu baada ya kupitisha Bunge lako hili tukufu Muswada huu basi tutakwenda kutengeneza Kanuni ambazo zitawezesha namna gani ya kutekeleza hii Sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa ubora wa dawa kwa jumla na rejareja kwa dawa za mifugo utaendelea kuwa chini ya *TFDA* ukishirikiana na Baraza la *Veterinary* kama ilivyokuwa hivi sasa. Naomba nisisitiza kwamba Sheria hii haitafuta majukumu ya *TFDA* katika kudhibiti ubora na usalama wa dawa. Badala yake Muswada huu unataka zaidi na kuangalia zaidi namna gani tunaweza tukasimamia na tukadhibiti wale wanataluma ndiyo wanaotoa hizo huduma za dawa. Katika kuweka utaratibu madhubuti wa kudumu wa kukagua maduka ya dawa muhimu (*ADO*) Baraza litawatumia Wakaguzi wa Dawa ambao kwa sasa wanatumika na *TFDA* katika ngazi za Mikoa na Halmashauri. *TFDA* wao katika ngazi za Halmashauri na Mikoa wanatumia wale Wafamasia walioajiriwa na Halmashauri. Hivyo basi katika kuanzisha hawa nao wataendelea kutumika wakiwa ndani ya huu Muswada ambao leo tumewawakilisha mbele yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa *ADO* mpaka sasa ni wa Kitaifa na mpaka sasa upo katika hatua za mwisho na upo kama mradi. Lakini ifikapo mwisho wa mwaka huu mpango wa maduka ya dawa baridi ni kwamba tumeboresha kama baadhi ya Wabunge walivyotoa malalamiko na hoja kwamba huko vijijini hasa maduka yenye we hayakidhi, hata jengo lenyewe na ndiyo huu mpango wa *ADO* umetengenezwa ama umeanzishwa kuboresha haya maduka ambayo Waheshimiwa Wabunge wameeleza kwamba hayakidhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mpango huu upo kwenye hatua za mwisho na tutakapofika mwisho wa mwaka huu tutakuwa tumemaliza nchi nzima na tutakuwa tumeuingiza katika mfumo wa Kitaifa. Tofauti na maduka haya baridi, maduka ya *ADO* yanaorodha ya namna gani yataendesha zile shughuli na namna gani wataweka sehemu za kuhifadhi dawa na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie kwa ujumla tu hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kuchangia Muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge, wamezungumzia suala la mafunzo ya hii taaluma, Naibu Waziri alilieleza mimi minachositisiza kwamba haitakuwa tofauti kama ilivyo taaluma zingine kama za Wahasibu, Manesi na Madaktari. Ni lazima tuwahakiki kama kweli baada ya kumaliza vyuo hawa watu wanauwezo, maana wengine mnaona vyuoni wengine wanachakachua kwa kupata digrri zao na vyeti vyao. Sasa huyu unamweka, unampeleka kutoa huduma za kuokoa uhai wa Mtanzania, jamani hili si jambo la zihaka, tutashirikiana na vyuo husika ambavyo vinatoa mafunzo ya taaluma hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza litaunda Kanuni za utoaji wa mafunzo za wataalam hawa wa fani za famasia ngazi mbalimbali pamoja na zile kozi za muda mfupi kwa kushirikiana na vyuo mbalimbali katika kuandaa mitaala ya wataalam wafamasia. Kwa hiyo, kazi ya Baraza ni kuwasimamia hawa wafamasia ambao wamefunzwa na wamekidhi kufanya hizi kazi za taaluma je, wanakwenda sambamba na maadili? Ndiyo maana tumeweka Sheria za kuweza kuwadhibiti na kuwapatia adhabu pale ambapo panastahiki. Sasa Sheria iliyopo ina mapungufu, hatuwezi kuwadhibiti hawa.

Vilevile limezungumziwa suala la Muundo wa Baraza. Wajumbe wa Baraza watareuliwa kutoka katika sekta ya umma na sekta binafsi, na ikumbukwe kwamba Baraza hili lipo ndani ya Wizara na tuliona kwamba Mwenyekiti na *Registrar* walikuwa wanateuliwa na Rais. Lakini tumeteremsha sasa Waziri anayesimamia majukumu haya ya afya na hii taaluma ya famasia ndiye atakuwa na jukumu la kuwateua hawa na vigezo vitawekwa wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Baraza atateuliwa kutoka kwenye sekta binafsi ili kuwezesha Baraza kuwa huru katika kutoa maamuzi yake kwa manufaa ya umma. Mkumbuke kwamba watendaji wengine wa haya mambo ya dawa ni wa Serikali, sasa pale wanapokiuka au kukosea itabidi washtakiwe. Sasa kama unamweka huyu Mwenyekiti ndiyo mtumishi toka sekta ya umma atakuwa na kigugumizi kuiadhibu Serikali. Kwa misingi hiyo Mwenyekiti kutoka sekta binafsi, Baraza tutaliwezesha kuwa

huru katika kutoa maamuzi yake bila kuingiliwa na mtu yeote na kuna sehemu ndani ya Muswada huu imeelezwa uhuru wa kutokuingiliwa na Baraza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge wamechangia hasa Ibara ya 19(4), hii imechangiwa na Mheshimiwa John Mnyika ambayo inasema “*the decision of the council shall be final*” hoja yake yafutwe na yabadilishwe na “*the person may appear to the Minister*” ndiyo iwe badala yake. Ibaa hii ya 19(4) pendekezo la kufutwa maneno haya linakubalika na kuongeza “*the person may appear to the Minister whose decision shall be the final.*”

Vilevile Wabunge wamezungumzia kuhusu kuongezwa kwa wawakilishi katika Baraza hili na wamependekeza wawakilishi wawepo pia wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi. Naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba hii ni *profession* Baraza la Taaluma. Sasa taaluma zingine hakuna uwakilishi wa vyama. Sasa sijui kwa nini watu bado wanasisitiza basi Baraza hili nalo kama *profession* nalo kuwe na wawakilishi toka vyama vya wafanyakazi. Kiutaratibu hili Baraza litakuwa ndani ya Wizara. Hivyo basi *TUGHE* watakuwa wanawakilisha moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge vilevile wamezungumzia na kuhoji sana kwamba Muswada huu utahodhi kazi za *TFDA*. Mheshimiwa Naibu Waziri amelizungumzia na mimi naomba nilifanue.

Mheshimiwa Naibu Spika, umezungumza ndani ya ile sheria tumeelekeza Muswada na katika utangulizi wangu wa kuwasilisha hoja, nilizungumzia kwamba sheria ya *TFDA* Namba 219 itafanyiwa marekebisho kwa sababu vile vifungu ambavyo tutarekebisha vifungu vya 26, 27, 47 na 74 vinahusu moja kwa moja masuala ya huduma ya Famasi katika maduka ya dawa, haihusiani na majukumu makubwa ambayo *TFDA* ndiyo wanatakiwa wafanye ya kudhibiti ubora na usalama wa dawa.

Ukiangalia vile vifungu havimnyimi wala havitamdhooftsha huyu *TFDA* katika wajibu wake. Vifungu hivi vinazungumzia zaidi mambo ya kupewa vibali, kunyang’anywa vibali vya kuendesha taaluma hii ya Famasia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi na udhibiti wa taaluma ni pamoja na usimamizi wa maadili na utendaji kazi *ethics and conduct* kwa wanataluma, mahali, kazi na ndiyo maana tumeona vipengele hivi viondolewe kule *TFDA* la sivyo ndiyo tatarudi pale pale tulipotoka ile Sheria ya Famasi ya mwaka 2002 ambayo imekuwa vigumu kutekelezeka. Wakati mwagine kulikuwa na mwingiliano wa hizi taasisi mbili ambao wote wawili ni watoto ndani ya mzazi mmoja yaani Wizara ya Afya na Wizara ya Maendeleo ya Jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya dawa ni huduma inayotakiwa kutolewa kwa mazingira kwa kuzingatia hasa taaluma, ujuzi na kwa maadili ya kifamasia na siyo kama biashara nyingine, ndiyo maana tumekuwa makini sana kunyofoa vile vipengele ili kuondoa utata huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile baadhi ya Wabunge waliochangia walirudia ile hoja ya Kamati kifungu cha 37(1)(b) kinachotoa mamlaka ya Baraza kutoa kibali cha biashara ya jumla kifanyiwe marekebisho na kuangalia upya kazi hii ifanywe na **TFDA**.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri huu umezingatiwa katika jedwali la marekebisho katika Ibara ya 37 ambayo inaainisha mipaka na majukumu ya Baraza la Famasi na **TFDA**, aidha, Baraza la Famasi litasimamia taaluma ya famasi katika maeneo ya usambazaji wa dawa na utoaji wa huduma za dawa (*distributors and drugs outlets*) na **TFDA** itaendelea kudhibiti ubora na usalama wa dawa kwa wazalishaji na waagizaji wanje wa dawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile baadhi ya Wabunge wamegusia kwamba kwa nini Wafamasia wasiruhusiwe kusimamia maduka ya dawa zaidi ya matano kwa kuwa katika dawa nyingi wapo wasaidizi ili kukabiliana na uhaba tuliokuwa nao wa huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, watalaaam hawa wanatofautiana katika ngazi za taaluma kuhusu dawa, kazi kubwa ya Wafamasia ni kuhakikisha mgonjwa anapata huduma bora na sahihi kulingana na hali au matatizo aliyokuwa nayo. Pia kuhakikisha kuwa mgonjwa analindwa dhidi ya madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya dawa kwa hali hiyo kuruhusu Mfamasia mmoja kusimamia duka zaidi ya mmoja kutamnyima mgonjwa au mteja kupata huduma bora anayostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo niliyoyaeleza na yale aliyotangulia kuyaeleza Naibu Waziri, tumegusia karibuni masuala yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia na mimi naomba nirudie tena kuwakumbusha kwamba huu mjadala ulianza tangu mwaka 2006 baada ya kuona kwamba kuna mapungufu katika ile sheria ambayo inatuongoza upatikanaji wa dawa, ndipo mwaka 2009 Baraza la Mawaziri waliona kuna haja ya kuanzisha sheria mpya itakayoweza kuondoa utata huu na kuboresha huduma hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, namshukuru sana Mbunge mmoja yeye amekumbusha kwamba kwanza tumechelewa sana, tukumbuke wanaoteseka hasa ni wananchi wetu sisi wengine tulimo humu wengi wetu tuna hakika ya kupata huduma hizi kwenye Famasi ambazo ubora wake kidogo ni mzuri na nyingi zimejazana sehemu za mijini. Huko wanakokaa Watanzania wengi bado tatizo ni kubwa, upatikanaji wa dawa hizi, dawa zingine zinaisha wakati, wanataluma wanaotoa huduma hizo hawakidhi na hawatoi huduma kama inavyotakiwa, hivyo basi, tumeona tuiangalie tena upya sheria ambayo inaoanisha huduma hizi za Famasia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimalizie tena kwa kuwashukuru wote waliochangia kwa kuongea hapa Bungeni na wale waliochangia kwa maandishi, ila jambo la mwisho naomba mtafakari kwa makini zaidi ili muweze kuridhia hoja hii ipite na sheria iundwe ili tuweze kurekebisha upatikanaji wa dawa bora na upatikanaji wa huduma bora za Famasia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Famasi (*The Pharmacy Bill, 2010*)

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 77(1) (2). Hivi sasa Bunge lako linakaa kama Kamati.

MWENYEKITI: Naomba uisome

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 77. Akidi kwa kila kikao cha Bunge wakati wa kufanya maamuzi itakuwa ni nusu ya Wabunge wote kama ilivyofafanuliwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 94, isipokuwa kwamba idadi hiyo haitaruhusu hoja kuhusu uamuzi wa kubadilisha masharti yoyote ya Katiba kwa mujibu wa Ibara ya 94. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 94 nusu ya Wabunge wa Bunge hili ni 176, Wabunge waliopo hapa hawatimii hivi sasa hiyo 176 au vinginevyo wahesabiwe ili kuweze kufanya maamuzi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, bahati nzuri hoja yako haikuungwa mkono, tunaendelea. (*Makofi*)

Kifungu cha 1

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 2

Kifungu cha 3

Kifungu cha 4

Kifungu cha 5

Kifungu cha 6

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 7

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 8

Kifungu cha 9

Kifungu cha 10

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 11

Kifungu cha 12

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 13

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 14

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 15

Kifungu cha 16

Kifungu cha 17

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 18

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Ibara hiyo kwa kuongezea maneno ambayo yataweka kikomo cha muda kwa hizo leseni au usajili wa muda mfupi (*provisional*

registration) kuwekewa mipaka kwamba usajili huo uwe ni kipindi cha miezi sita kama ambavyo isomeke kwenye jedwali la marekebisho nililoliwasilisha. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika nakuomba urudie tena kwa kukumbuka jambo moja, unachoruhusiwa kukizungumza hapa ni kile ulichoki-*move* kama *amendment* peke yake, huwezi tena kuchomekea hapo ndani yake. Kwa hiyo, naomba sasa useme mabadiliko yako ni yapi ukikumbuka kwamba yale uliyoyaandika Waziri alishayakubali. (Makofi)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili siyo ambalo limekuwa *admitted*, ni suala lingine labda niseme tu kwamba *in the clause 18 inserting the words for a period of six month, between the words registered and under* ili kuweza kuweka kikomo cha muda.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mnyika Mbunge wangu mwengine wa Ubungo kwa marekebisho aliyoyapendekeza, mantiki ya marekebisho haya ni kwamba hizi *provisional licence* ziwe na muda wa miezi sita, lakini kwa sababu kazi zenyewe hizi zinategemeana kutoka sehemu moja kwenda nyingine tunadhani kwamba ni vizuri huo muda uachiwe ile *council* yenyewe ndiyo itakayofahamu ulazima wa hiyo *duration*, ule muda wa leseni lakini *otherwise* katika hali nyingine tungeweka hicho kikomo. Kwa hili nafikiri kwamba ilivyo sasa inafaa. (Makofi)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa hiyo mantiki lakini sheria ikiacha wigo, wigo huo unaweza ukatumika kutoa leseni za muda kwa muda mrefu sana sawa na leseni zingine kwa sababu hiyo hoja ya kuweka kikomo cha muda bado ni ya msingi sana. Kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaona siyo lazima muda utajwe kwenye sheria basi hiyo *provision* ibadilike isomeke kama itakavyotajwa kwenye Kanuni, ili kwenye Kanuni kuwe na utaratibu wa hizi leseni za muda ili hayo mamlaka yasiwe *abused*, ama kutoa muda mfupi sana au kutoa muda mrefu sana. (Makofi)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge sasa isomeke kwamba *with additional requirements, be entitled to provisional registered as may be provided under the rules or regulations made under this act.* (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili Makatibu waipate vizuri utusomee *provision* yote sasa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, fasili ya (1), *A person who is not entitled to be registered by reason only of the fact that he has not complied with the additional requirements referred to in section 16(2)(b) shall, if, upon application in prescribed manner, he satisfies the Council, that he has secured an offer for employment or training in an institution or facility approved by the Council for the purposes of complying with the additional requirements, be entitled to be*

*provisionary registered for a duration provided under the rules made under this act.
Badala ya rules tuweke regulations kwa sababu regulation zinatengenezwa. (Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 19

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kifungu husika kifanyiwe marekebisho kwa kufuta maneno, *the decision of the council shall be final* na badala yake kuongeza maneno *the person may appeal to the Minister whose decision shall be final.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (Makofi)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeshamfahamisha Mheshimiwa Mnyika na nilimpa mapendeleko mbadala kwamba Kifungu hicho kiishie tu pale kwenye *council* na yale maneno *the decision of the council shall be final* yafutwe, na tuongeze kifungu kingine cha tano kinachosomeka kama ifuatavyo; *not notwithstanding sub-section four, a person agreed by the decision of the council may appeal to the Minister.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyika aliniletea karatasi hapa akikubaliana na haya. (Makofi)

MWENYEKITI: Asante sana. Naona Mheshimiwa Mnyika amekubaliana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 21

Kifungu cha 22

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 23

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 24

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 25

Kifungu cha 26

Kifungu cha 27

Kifungu cha 28

Kifungu cha 29

Kifungu cha 30

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 31

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 32

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 33

Kifungu cha 34

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 35

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 36
Kifungu cha 37

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 38

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 42

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 46
Kifungu cha 47

(*Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 48

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mabadiliko kwenye hicho kifungu cha kuongeza kipengele kinachosomeka kama

ifuatavyo; “A person aggrieved by the decision of the council under subsection 1 may appeal to the ministry within a period of seven days.” Naomba kuwasilisha.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna tatizo na hilo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 49

Kifungu cha 50

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 51

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 52

Kifungu cha 53

Kifungu cha 54

Kifungu cha 55

Kifungu cha 56

Kifungu cha 57

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 58

Kifungu cha 59

Kifungu cha 60

(*Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima
bila mabadiliko yoyote*)

Jedwali

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kupendekeza marekebisho kwenye jedwali (*schedule*) iongezwa kifungu (g) kisomeka “A representative from Tanzania Union of Government Health Workers’ na kwa sababu ya kuongezwa kipengele hicho basi mtiririko wa namba ubadilike *item* (g) na (h) mtiririko wake wa namba ubadilike. Pamoja na kuwasilisha haya pengine naomba kwa mujibu wa Kanuni 88(5) na (6) niweze kupewa wasaa wa kutoa sababu za kwa nini mapendekezo haya ni muhimu kuzingatiwa katika marekebisho maana katika ufanuzi wa Waziri alionyesha hayakuwa na ulazima. Kwa hiyo, naomba nipewe kwa mujibu wa Kanuni kueleza sababu za mapendekezo haya. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Sawa endelea.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa mujibu wa Muswada wa Sheria tunayopitisha Kifungu cha 4 kinachoeleza majukumu ya hili Baraza na Kifungu cha 5 kinachoeleza mamlaka ya hili Baraza kifungu (c) kinasema mamlaka haya ni pamoja kumfuta mtu kwenye orodha ya wafamasia waliosajiliwa na Kifungu (g) kinasema mamlaka ya hili Baraza ni pamoja kumshtaki na kumhukumu kwa makosa mbalimbali yaliyotajwa humu.

Sasa tukumbuke kwamba kwa wafamasia hawa kwa mujibu wa sheria yenye ni watu ambao wengine ni wafanyakazi wa sekta binafsi, wengine ni wafanyakazi wa sekta ya umma. Kwa mujibu wa Mikataba ya *ILO* ambayo nchi yetu imeridhia masuala ya vyombo vyote vinavyohusu mwisho wa siku kumhukumu mfanyakazi ni muhimu sana wafanyakazi wakawa na wawakilishi wao. Kwa sababu hiyo basi, hata kama kuliwahi kutungwa sheria nyininge ambazo hazikuzingatia uwakilishi wa wafanyakazi kwenye vyombo vyenye mamlaka kama haya ya kuhukumu wafanyakazi. Kwa kuwa sasa tunatunga sheria hii ya sasa ni muhimu tukazingatia hali hiyo na mikataba ambayo nchi yetu imeridhia tukakubali baraza hili likawa na mwakilishi wa wafanyakazi kwa kuwa mamlaka na wajibu wa hili baraza ni pamoja na kuwashukumu wafanyakazi wanaofanyakazi kwenye sekta ya ufamasia katika masuala yanayohusiana na taaluma yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema kwamba kuna hoja ilitolewa ya Waziri kwamba hiki ni chombo cha watalaam kwa hiyo, masuala ya haki ya vyama vya wafanyakazi si lazima kuwakilishwa. Ningependa Bunge lako tukufu lifahamu kwamba Vyama vya Wafanyakazi ni Vyama vya Watalaam. Wafanyakazi wanaingia kwa kada zao, kwa utalaam wao kwa hiyo, kwa sababu ni Vyama vya Watalaam vya Wafanyakazi *by nature* na hapa tunaunda chombo cha watalaam naomba kulishawishi Bunge lako tukufu ili wafanyakazi wawakilishwe kwenye hili Baraza kwa ajili ya kulinda haki na maslahi yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yangu ya mwanzo nilisema siyo watalaam, wana taaluma na kwamba hili baraza ni baraza la wataluma. Kwa hiyo, kama makosa au ukiukwaji wa mwenendo itategemea

na maadili ambayo yameoanisha kwenye taaluma ile. Kwa hiyo, adhabu atakayopewa ni mambo ya kitaaluma. Hivyo naomba kama itakuwa masuala ya ajira hiyo atakimbilia kwenye vyombo husika kwenye chama chake ambacho ni *TUGHE*. Sasa sioni kwa nini watu hapa tunachanganya mambo ya wataalam na taaluma. Kwa kiingereza ile ni *professionalism* ya ma-pharmacists. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa tofauti kati ya *professionalism*, utaalamu na taaluma na yote haya. Ileleweke tunachokisema hapa kwa mujibu wa mamlaka ambayo baraza imepewa ina haki ya kumfuta mtu kwenye orodha, ina haki ya kumhukumu mtu kwa makosa, ukimfutia mfanyakazi kwenye orodha ya kuwa mfamasia hata kama ameajiriwa kwa nafasi yake ya ufamasia maana yake ni sawa sawa na kumfukuza kazi. Ni sawa sawa leo umuondolee dereva leseni yake ya udereva ni sawa sawa na kumfukuza kazi ya udereva hata kama hujamfukuza kazi ya udereva.

Sasa ukishaunda chombo ambacho kina mamlaka ya namna hii ni muhimu vyama vya wafanyakazi *by nature* kwa sababu vyama vya wafanyakazi ni *professionals*, vinagusa mambo yote wawili taaluma na utalaam yote mawili yako ndani ya vyama vya wafanyakazi. Kwa hiyo, bado nasisitiza kwamba ni muhimu sana haya marekebisho yakafanyika kwa ajili ya kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi. Sababu kwamba hili baraza liko chini ya Wizara kwa hiyo wafanyakazi watawakilishwa Serikali inawakilisha Serikali na wafanyakazi wanawakilishwa na vyama vyao vya wafanyakazi. Ni mamlaka mawili tofauti kabisa na yote ni ya msingi kwa Taifa letu. (*Makofi*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuwa usemi zamani ulitolewa na Karl Marx kwamba wafanyakazi wa dunia unganeni, hakuna mtakachopoteza isipokuwa minyororo yenu. *Workers of the world unit you have nothing to loose except your chains*. Kauli nzuri inavutia mdomoni. Lakini nafikiri tumsikilize Waziri vizuri anavyosema kwamba kwenye *professionalism* kwa mfano mimi wakili nimejiunga na chama cha mawakili na chama kile kina maadili ya mawakili. Sasa inawezekana mimi ni wakili lakini nimeajiriwa na mtu au nimeajiriwa na wakili mwengine. Sasa nitakapopelekwa kwenye nidhamu kwenye Baraza la Mawakili sitasema kwamba kwenye lile baraza kuwe na mwakilishi wa vyama vya wafanyakazi kwa sababu yule hatuna turufu kwenye mambo haya ya taaluma. Hiyo ndio tofauti Mheshimiwa Mnyika na mimi nakumbuka mwalimu alipokuwa na umri kama wewe alikuwa anasema kwa sauti hiyo hiyo. (*Makofi*)

Lakini sasa kuna mipaka ya haya mambo, kwa mfano kama taaluma anavyosema Mheshimiwa Waziri, taaluma ya wanafamasia tunachokuja kuzungumzia hapa ni mtu kwa mfano ameajiriwa lakini amepatikana kwamba mtu amekwenda kwenye duka la dawa amesema nipe *panadol* akampa au nipe *part one or part two poison* anampa au nipe zile dawa za kuongeza makalio hana cheti anampa. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa huyu anapelekwa kwenye hili baraza halafu unasema tunataka hili baraza liwe na mwakilishi wa wafanyakazi. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Mnyika hapa hakuna turufu hiyo isipokuwa sheria inazaliwa inaendelea inaishi, baadaye inakufa, baadaye inafufuka tena. Kwa siku za usoni pengine tunaweza kufikiria hivi kwenye

mambo mengine lakini kwenye hili mimi nakushawishi ndugu yangu kwamba tukubaliane na Mheshimiwa Waziri kifungu hiki kipite. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Kimsingi hoja ya Mheshimiwa John Mnyika Mbunge wa Ubungo ni hoja ya msingi sana ikizingatiwa kwamba *experience* inaonyesha mara nyingi kumekuwa na hoja kama ambavyo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, usije ukaanza kuchangia hebu kaa chini kwanza. Katika jambo hili lina pande mbili, kuna mto hoja ambaye amefuata utaratibu wote, ameleta na lile jedwali la marekebisho Mheshimiwa Mnyika kwa suala hili hapa tulipo. Lakini kuna mto hoja ambaye ni Mheshimiwa Waziri na yeze ana msimamo ambao ameuweka. Katika hatua hii ninayemwangalia ni Mheshimiwa Mnyika endapo haridhiki na maelezo ambayo yametolewa mimi napaswa sasa kulihoji Bunge ili liwaamue watu hawa. Lakini kama yeze ameridhika sijui utakuwa unanipa taarifa ipi. Kwa hiyo, hili suala ni la kwako kwanza tukishahojiana taarifa zako zitakuja baadaye. Asante.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naamini kwa mujibu wa kanuni mtu anaweza kutoa taarifa wakati wowote kwa mujibu wa kanuni. Ila niende moja kwa moja kwenye suala liliko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado sijaridhika. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nukta maana yake unanyanya mara mbili tu. Hii mara ya tatu ninachohitaji kama umeridhika au hujaridhika. Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba kuhoji sasa hapa tuelewane vizuri ninachohoji ni nini, ninahoji mabadiliko ambayo Mheshimiwa Mnyika anayapendeleza yaingie katika jedwali hili la wajumbe wanaounda hicho chombo. Anasema aongezeka mwakilishi wa kutoka chama husika nadhani *TUGHE* katika chombo hicho. Sasa wanaoafikiana na wazo la Mheshimiwa Mnyika kwamba huyu aongezeka waseme ndio.

(*Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yote*)

(*Bunge lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa.

Muswada wa Sheria ya Famasi wa Mwaka 2010 (*The Pharmacy Bill, 2010*)

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria

uitwao *The pharmacy Act 2010* kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake na kuukubali. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *The Pharmacy Act 2010*, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofit*)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofit*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Muswada umekwishesomwa katika hatua zake zote tatu na kwa hiyo, shughuli ya kuupitia Muswada wetu imekamilika vilivyo kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wanashiriki kwa mara ya kwanza kutunga sheria hizo ndizo taratibu ambazo tunazitumia katika zoezi zima la kutunga sheria kwa maana ya hatua zote ndani ya Bunge hili tukufu. Kwa hiyo, hatua iliyobakia ni safari ya Muswada huu kwenda kwa Mheshimiwa Rais ili kuweza kupata kibali chake ili uweze kukamilika. (*Makofit*)

Mimi nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa jinsi ambavyo mmetoa ushirikiano mkubwa kuanzia Kamati husika ya Huduma za Jamii na Wajumbe wake wote pamoja na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Margaret Sitta kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya ya kuupita Muswada huu. Mtaona kwa idadi ya marekebisho ya karibu kila kifungu kwa kweli Wabunge wa Kamati hii ni Wabunge makini kabisa. Ni kazi kubwa sana ambayo imefanyika. Lakini pia nimshukuru sana Waziri Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Katibu Mkuu na watumishi wote ambao wametoa ushirikiano mkubwa sana na Kamati ile katika kuupitia Muswada huu vizuri na maeneo ambayo yamehitaji marekebisho kwa kweli wametoa ushirikiano mkubwa sana na kazi hiyo imefanyika. (*Makofit*)

Lakini ndani ya Bunge hili Waheshimiwa Wabunge mmechangia kwa uwazi, mmechangia vizuri kabisa kwa nia ya kujenga chombo hiki kitakachosaidia usimamizi wa shughuli za mafamasia katika nchi yetu. Kwa hiyo, tunaitakia kila la heri Wizara katika safari ya Muswada huu na ukishapita tunawatakania kila la heri katika kusimamia jambo hili ambalo Watanzania tuna matumaini makubwa sana pamoja nanyi. (*Makofit*)

Naomba kusema tu kwamba shughuli zilizopangwa katika *Order Paper* ya leo zimekamilika zote na nirudie tangazo moja ambalo lilitangazwa asubuhi, nirudie kwa msisitizo kwa wale ambao hawakusikia nalo ni la ibada ambayo itafanyika kesho. Tangazo hili linatoka kwa familia ya Hayati Edward Moringe Sokoine aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania na *Edward Moringe Memorial Trust* ambao wanatutangazia Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi kwamba kesho tarehe 12 Aprili, 2011 siku ya Jumanne kwamba saa tisa alasiri kutakuwa na ibada maalum ya kumuombea Hayati

Edward Moringe Sokoine aliyefariki kwa ajali ya gari tarehe 12 April, 1984 Wami Dakawa, Morogoro. Ibada hiyo itafanyika katika Kanisa Kuu la *Roman Catholic* hapa Dodoma. Tunaomba wote mhudhurie, Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Baada ya tangazo hilo naomba basi kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi. Ahsanteni.

(*Saa 1.22 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 12 Aprili, 2011 saa tatu asubuhi*)